**10 NOVEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Kumi – Tarehe 10 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Tunza Malapo.

Na. 135

**Kuanzisha Mkoa Mpya wa Manonga**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaugawa Mkoa wa Tabora na kupata Mkoa mpya wa Manonga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzisha eneo la Utawala la Mkoa unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo baada ya Idhini/Kibali kutolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia Sheria inayohusu kuanzisha Mkoa na Wilaya, Sura Na. 397 na Mwongozo wa kuanzisha Maeneo Mapya ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kuanzishwa Mkoa mpya yanatakiwa kujadiliwa, kupitishwa na kuridhiwa kwenye vikao vya Kisheria ngazi ya Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya, Kamati ya Ushauri ya Mkoa kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya tathmini ya vigezo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhitaji mkubwa wa miundombinu na rasilimali nyingine katika mikoa iliyopo, Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu msingi kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swali moja la nyongeza, lengo la kugawa maeneo ya utawala ni kurahisisha huduma kwa wananchi, lakini hapa nchini kuna Majimbo mengi sana makubwa ikiwemo Jimbo la Mbeya Mjini, Tandahimba na sehemu nyingine; je, Serikali ina mkakati

gani wa kuyagawa Majimbo hayo ili huduma kwa wananchi ziwe rahisi? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lengo la kugawa maeneo mapya ya utawala yakiwemo majimbo ni kusogeza huduma za kijamii karibu zaidi na wananchi na Serikali inatambua uhitaji wa maeneo haya. Kwa hivyo kwa utaratibu uliopo, kwa mujibu wa mwongozo lakini na sheria, mamlaka husika wanatakiwa kufuata utaratibu huo kwa maana ya Vikao Ngazi ya Vijiji, Baraza la Madiwani, *DCC, RCC* na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI na pale ambapo Serikali itaona inafaa kugawa maeneo hayo ya utawala mapya basi taratibu zitafuata na maeneo hayo yatagawiwa katika utaratibu ulipo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa imefanyika sensa hapa hivi karibuni na ziko kata zimeonekana ni kubwa zaidi zinahitaji mgawanyo pamoja na tarafa ikiwemo Kata ya Mandewa na Kata ya Minga. Nataka kujua mkakati wa Serikali ni nini kifanyike sasa ili kuweza kuzigawa kata hizo na kusogeza huduma kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Mussa Sima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunafahamu kwamba kuna kata kubwa, kuna tarafa kubwa na Serikali inatambua inatambua umuhimu wa kugawa maeneo hayo kusogeza huduma za kijamii,

lakini utaratibu ni uleule tuanze kwenye Vikao vya Kisheria katika ngazi zetu za Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa kisha kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kufanya tathimini ya vigezo hivyo na kuona uwezekano wa kupata maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ukiona mchakato uliopo sasa hivi kufikia uamuzi huo ni mrefu sana. Kwa nini Serikali isiachie jukumu hilo katika *level* ya juu (Serikali Kuu) ndiyo ifanye maamuzi badala ya vikao vyote hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, utaratibu huu umewekwa kwa sababu kugawa maeneo ya kiutawala pia kuna hitaji ridhaa ya wananchi kutoka katika maeneo husika. Serikali hii sikivu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita, lakini hata Serikali zilizopita zinahitaji kuwashirikisha wananchi katika kugawa maeneo yao ya utawala ndiyo maana mfumo huu ni muhimu na vizuri sana utaratibu huu ukafuatwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kama alivyosema Mheshimiwa Kajege Sensa ya Watu na Makazi mojawapo ya jambo la kutusaidia ni kupanga Mipango ya Maendeleo.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutumia Taarifa na Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ikaona kabisa kuna maeneo yanahitaji kufanya mgawanyo *then* yenyewe ikashusha kwetu sisi wananchi na sisi tukasema ndiyo au hapana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato David Mchumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria ni sheria ambazo sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tulizitunga na lengo la sheria hizi kama nilivyotangulia kusema ni kuhakikisha kwamba tunawashirikisha wananchi katika kuamua mipaka, lakini pia kupata maeneo ya utawala.

Kwa hiyo nafikiri utaratibu huu ambao upo ni muhimu ufuatwe, lakini kama kuna maoni zaidi ya kuona ni namna gani tunaweza tukaboresha basi Serikali iko tayari kusikiliza maoni na kuyafanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana, kwa majibu yako. Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na.136

**Ujenzi wa Korongo la Starehe - Tarime Mji**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa mawe Korongo la Starehe ambalo linahatarisha maisha ya wananchi wa Kata ya Nyamisangara, Tarime?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itatenga shillingi millioni 280 kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* kwa ajili ya ujenzi wa Korongo la Starehe lililopo Mji wa Tarime.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika korongo lile zipo nyumba ambazo ziko jirani sana, wananchi na wakazi wa Mtaa ule wangependa kujua wale wananchi waliopo karibu na korongo zile kaya, je, Serikali ina mpango gani, watawafidia au itakuwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; korongo hili ni hatarishi sana; je, ni lini hasa Serikali itaanza ujenzi wa korongo hili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kembaki; la kwanza hili la nyumba zilizopo jirani na korongo hili. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Serikali itatenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili kwenye korongo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Mara kwa kushirikiana na Meneja wa *TARURA,* Wilaya ya Tarime kwenda kufanya tathmini katika eneo hili na kuona hizi nyumba ambazo Mheshimiwa Kembaki amezitaja zipo umbali gani kutoka kwenye *road reserve* ambayo imewekwa na kisha kuwasilisha taarifa hii *TARURA* Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, nirejee tena majibu yangu ya msingi kwamba Serikali itatenga fedha mwaka wa fedha 2024/2025 na fedha hii itakapotengwa ndipo

kazi hii itatangazwa na kuanza kujengwa daraja hili katika Bonde hili la Mto Starehe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.137

**Mpango wa kutoa chakula shuleni**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kutoa chakula mashuleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wadau mbalimbali wanaounga mkono jitihada za Serikali katika utoaji wa huduma ya chakula na lishe shuleni. Baadhi ya wadau hao ni kama vile Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP), United Nations Children's Fund (UNICEF), World Vision, Feed the Children, SANKU, GAIN Tanzania, Project Concern International (PCI), CiC, Save the Children.*

Mheshimiwa Spika, wadau hao hufanya kazi kwa kushirikiana na Serikali katika kuzijengea uwezo Kamati za Shule namna ya ushirikishwaji wa wazazi/walezi katika upatikanaji wa chakula cha wanafunzi shuleni, kutoa elimu ya uongezaji wa virutubisho katika chakula cha wanafunzi shuleni *(fortified foods);* kuhamasisha upatikanaji wa matumizi ya mazao lishe *(biofortified)* yakiwemo maharage, mahindi ya njano, kwa ajili ya uji wa wanafunzi; kushirikiana na shule zenye utayari wa

kuendesha shughuli za kilimo cha mazao ya chakula kwa kugawa mbegu za mahindi na maharage shuleni; na kuandaa miongozo ya utoaji wa huduma ya chakula na lishe shuleni.

Mheshimiwa Spika, mpango upo na unatekelezwa kwa kushirikisha wadau ili kuendelea na mpango wa kutoa chakula.

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Kirumba, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, licha ya hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; mradi huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo ni ukosefu wa miundombinu, maji safi na salama, ongezeko la shule mpya nyingi ambazo haziko kwenye mradi, zimepelekea watoto wetu wanapokuwa shuleni kukosa chakula.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wadau hawa wa Sekta ya Elimu wameelekeza watoto wanapokuwa shuleni wafundishwe namna bora ya kupanda mbogamboga na kupanda matunda ili yaweze kuwasaidia kupata mlo bora ambao utawatoa wasiweze kushindwa kupata udumavu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Santiel Kirumba; la kwanza, hili la ukosefu wa miundombinu mbalimbali hasa katika shule mpya ambazo zimejengwa hivi karibuni miundombinu kama maji na kadhalika. Tunashirikiana na Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na kadhalika katika kuhakikisha miundombinu muhimu inafika katika Taasisi zetu za Serikali kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo shule na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha huduma bora inatolewa katika shule zetu zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili; Kuna *club* mbalimbali katika shule zetu katika kuhakikisha kwamba upandaji wa mbogamboga unafanyika na kuendelea kufundishwa kwa wanafunzi wetu katika shule zile na Serikali itaendelea kutilia mkazo uwepo wa *club* hizi. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwaelekeza ma-*REO* wote na ma-*DEO* wote nchini (Maafisa Elimu Mkoa na Maafisa Elimu Wilaya) kuhakikisha kwamba *club* hizi za upandaji wa mbogamboga zinaendelezwa katika shule zetu za sekondari na shule zetu za msingi nchini kote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 138

**Maboma ya shule yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi Mbozi**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa maboma ya shule za msingi na sekondari yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa kukusanya takwimu za maboma yaliyojengwa na wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuweka mkakati na mpango wa ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashauri ya Mbozi ina maboma mengi ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Mwaka 2020/2021 kulikuwa na maboma 1,529

yakiwepo madarasa ya shule za msingi 1,513 na sekondari 86. Yaliyopo kwa sasa baada ya Serikali kwa kushirikiana na Wadau na wananchi kuyakamilisha ni ya shule za msingi 1,386 na sekondari 76 ambayo kati ya hayo 64 yamepauliwa. Aidha, maboma yaliyotengewa bajeti kwa kipindi cha 2023/2024 ni 18. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuyapunguza kadri inavyopata fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa wananchi wamejitolea kwa kiwango kikubwa sana katika ujenzi wa maboma haya na waliahidiwa kwamba Serikali itakamilisha na maboma hayo ni mengi sana, je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga bajeti maalum ili kukamilisha majengo hayo kuwaunga mkono wananchi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa katika maeneo mengi sasa hivi Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya, ni kwa nini Serikali isipeleke fedha kukamilisha haya madarasa ambayo yameshaanzishwa na wananchi badala ya kuanza madarasa mapya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, la kwanza kwa nini isitengwe bajeti maalum kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali na wananchi wenyewe katika kuhakikisha kwamba maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi nchini kote yanakamilishwa. Hivi sasa Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo katika mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuunga mkono jitihada za wananchi nchini kote waliojenga maboma yao ikiwemo kule jimboni kwa

Mheshimiwa Hasunga ambapo kuna maboma zaidi ya elfu moja na mia tano kwa ajili ya kwenda kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili; kwa nini hizi fedha zinazokwenda sasa kwenye kujenga madarasa, kwenye kujenga shule mpya zisiende kwa ajili ya kumalizia yale maboma?

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijenga shule na madarasa kupitia miradi mbalimbali, ambayo ni vigezo vya miradi ile kuhakikisha kwamba inajenga madarasa mapya inajenga shule mpya na kupimwa kulingana na matokeo yale yanayotokana na ujenzi ili tuweze kupata fedha nyingine nyingi zaidi kwa ajili ya kujenga shule nyingine nyingi na madarasa mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, nirejee katika majibu yangu ya swali lake la nyongeza la kwanza, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo katika mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za wananchi nchini kote waliojenga maboma ya madarasa. Vilevile kuna fedha ile ya maendeleo ambayo Halmashauri inatakiwa kutenga na ndiyo kazi yake hii, Wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanaunga mkono jitihada za wananchi kwa kutumia fedha ile ya maendeleo kwenye halmashauri zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Shule za msingi Kwai, Kweboma zimechoka mno; je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ukarabati katika shule hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita ilitenga zaidi ya bilioni 230 kote nchini kwa ajili ya ukarabati wa shule za msingi zilizochoka na ujenzi wa shule mpya za msingi, zikiwemo nyingine kule Jimboni kwa

Mheshimiwa Shekilindi. Hizi shule alizozitaja za Kwai na kwingineko Serikali itaendelea kutafuta fedha na kadri ya upatikanaji wa fedha itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mariam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 139

**_NEMC_ na _ZEMA_ kusajiliwa _GCF_**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha *NEMC* na *ZEMA* zinasajiliwa kwenye Mfuko wa *GCF*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mkakati uliopo ni kuhakikisha *NEMC, ZEMA* pamoja na taasisi nyingine zilizoomba au zitakazoomba usajili chini ya *GCF* zinapata usajili katika Mfuko wa *GCF*. Hivyo, kwa sasa Serikali inaendelea na mawasiliano, majadiliano na mazungumzo ya kuhakikisha usajili kwa taasisi mbalimbali za Serikali unakamilika.

Mheshimiwa Spika, *NEMC* tayari imeshaomba na kuanza mchakato wa usajili *(accreditation)* tangu mwaka 2021, na kwa upande wa *ZEMA* ilikuwa bado haijawasilisha maombi ya usajili

kwenye Mfuko wa *GCF*. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhakikisha taasisi zote zilizoomba usajili katika Mfuko wa *GCF* zinapata usajili ili kunufaika na faida za mfuko huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi swali la, *eh!* Ngoja nitaje na la katikati maana inaweza ikaenda kwa mtu mwingine. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni hatua gani zinazotumika mpaka uungwe kwenye Mfuko huu wa *GCF?*

Swali la pili, kutokana na uhitaji wa miradi ya mazingira Zanzibar; je, ni lini *ZEMA* wataanza mchakato wa usajili kwenye Mfuko wa *GCF?* Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dada yangu Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hatua zilizokuwepo ni kwamba taasisi mbalimbali nchini mwetu ambazo Ofisi ya Makamu wa Rais ni mratibu zinawasilisha nia hiyo na mwishowe mchakato huo unaenda sasa katika mfuko huo. Mwisho wa siku ni kwamba, taasisi hiyo baada ya mchakato utakapokamilika basi inakuwa imekidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kumekuwa na changamoto katika mchakato huo kwa sababu zaidi ya taasisi sita nilizozipeleka hivi sasa bado hazijafanikiwa. Kwa hiyo, tumeendelea kufanya kazi hii kubwa ya kuhamasisha jinsi gani wenzetu waweze kukubali maombi yetu, kwa lengo kwamba taasisi zetu ziweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, upande wa swali la pili ni kweli, upande wa Zanzibar kuna changamoto kubwa za kimazingira. Hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inaendelea kushirikiana kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ni kwamba hivi sasa tunatekeleza baadhi ya miradi. Kwa mfano, ukienda kule Sipwese - Pemba, tunajenga ukuta pale wa Bahari, ukienda Kaskazini A na maeneo mbalimbali. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaendelea kushirikiana lengo kubwa ni pande zote mbili za Muungano ziweze kupata fursa miradi maendeleo hususani katika hususan katika sekta hii ya mazingira, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako. Tunaenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 140

**Mashtaka katika Bodi na Mahakama za Rufaa za Kodi**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka mkakati maalum wa kumaliza mashtaka katika Bodi na Mahakama za Rufaa za Kodi?

**SPIKA:** Waheshimiwa mnisaidie anayefuata kujibu swali awe hapo ili nijue namuita nani, maana sasa inabidi nikae kimya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Oktoba, 2023 Bodi ya Rufani za Kodi ilikuwa na mashauri 889 yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi trilioni 6.46 na dola za Kimarekani milioni 4.66. Katika kipindi hicho, Bodi imesikiliza mashauri 167 yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi trilioni 2.66 na dola za Kimarekani 200,001. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi lilikuwa na mashauri 176 yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi bilioni 266.94, ambapo mashauri 91 yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi bilioni 166.32 yamesikilizwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Bodi ya Rufani za Kodi na Baraza la Rufani za Kodi zinaendelea kutekeleza Mpango Maalum *(Special Sessions)* ambapo kuanzia mwezi Novemba, 2023 hadi Juni, 2024 wanasikiliza na kumaliza mashauri ya kodi yaliyofunguliwa. Kupitia mpango huo, mashauri mengi zaidi yatasikilizwa katika Mikoa mbalimbali nchini kwa kuzingatia wingi wa mashauri haya ikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Ruvuma, Tabora, Mara, Manyara, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Songwe pamoja na Njombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha Taasisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi *(Tax Ombudsman)* ambayo jukumu lake kubwa itakuwa ni kupokea malalamiko na kutatua masuala ya kikodi yanayotokana na huduma, hatua za kikodi au utekelezaji wa sheria za kikodi kutoka kwa mlipakodi mbalimbali pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado kuna hela nyingi ziko pale kwenye hizi *TRAT* na *TRAB.* Kuna shilingi bilioni 600 zipo *TRAB* na shilingi trilioni 2.29 bado zipo *TRAT.*

(a) Je, Serikali mnatupa muda gani wa kuwa mmemaliza hizi hela zirudi kwenye Mfuko wa Serikali zikafanye kazi za maendeleo? *(Makofi)*

(b) Katika kuchelewesha huku na kusuasua, hamuoni kwamba tunaharibu mahusiano mema ya Serikali na

wafanyabiashara ambao ndiyo tegemeo letu la mapato? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia jambo hili ambalo ni muhimu sana na amejenga hoja za Kibunge. Niliyaepuka haya maneno ya *TRAT* na *TRAB* lakini kwa kuwa ameshayasema ngoja niyasema tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja; fedha zile ambazo zipo zinabishaniwa kabla hazijaamuliwa haziwi fedha za Serikali ni fedha zinazobishaniwa, na katika kubishaniwa kwake na hivi sasa tumeanzisha Ofisi hiyo ya Msuluhishi, kimsingi Serikali inataka kujenga mahusiano mazuri na walipakodi, kwa sababu Serikali ingenyoosha mkono tu kwamba hapa tunachokadiria sisi ndiyo tunataka ulipe, hiyo ndiyo ingeharibu mahusiano na walipakodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zitakuwa fedha za Serikali mpaka pale ambapo mkono mwingine *whether TRAB* ama *TRAT* itakaposema kwamba hii sasa ni fedha ya Serikali, lakini ikiwa bado inabishaniwa Serikali inatoa fursa ya haki kutendeka na vyombo hivyo vinaongozwa na watu ambao ni maarufu katika tasnia ya sheria. Kwa hiyo, tunaamini haki itaendelea kutendeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuharakisha ndiyo tumetengeneza utaratibu wa kuanzisha hizi *sessions* maalum ili haya mambo yasiwe yanakaa sana, kwa sababu yanaondoa utulivu katika ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, lingine kama ambavyo nimeweka kwenye jibu la msingi, uwepo wa ofisi hii ambayo wafanyabiashara wameitamani siku nyingi ya Msuluhishi wa Masuala ya Kikodi, tunaamini na yenyewe itaenda kupunguza mrundikano wa masuala yanayobishaniwa kwa sababu sasa maeneo ambako makadirio hawakuridhiana yataenda kwa mtu mwingine ambaye hayuko kwenye mfumo ule wa kukadiria.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 141

**Kukamilisha Jengo la Makazi ya Askari Polisi Buyekera - Bukoba**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha jengo la Makazi ya Askari Polisi lililopo Kata ya Buyekera Bukoba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu,

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni moja kutoka kwenye bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la makazi ya Askari Polisi lililopo Buyekera - Bukoba Mjini. Ujenzi huo unatarajiwa kuanza mara baada ya Wizara ya Fedha kuhamishia fedha hizo Jeshi la Polisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Waziri, jengo hili limeanza kujengwa tangu mwaka 2010 ni miaka 13 sasa.

Kwanza, niulize Serikali kwa nini imetelekeza jengo hili mpaka limekuwa gofu?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu Serikali imesema itatoa bilioni moja, mtupe *commitment* Serikali ili azma ya kujenga jengo hili iweze kutimia. Ni lini Serikali inakwenda kukamilisha jengo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakamilisha jengo hili? Nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba ni pale tutakapopata fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie tu Mheshimiwa siyo dhamira ya Serikali kuacha majengo kuwa magofu, majengo mengine yalitegemea uwepo wa fedha pale ambapo tulikwama na umesema ni miaka 10 iliyopita, ndiyo maana majengo mengi sasa hivi tunayakamilisha. Ukienda maeneo mbalimbali Geita Jengo la Polisi la Mkoa linakaribia kukamilika, Mara linakaribia, Njombe limekaribia kukamilika. Kwa hiyo, tuna imani Wizara ya Fedha itakapotoa fedha hizi ili jengo la Kagera pia tutalikamilisha. ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Eneo la Ikuti Wilayani Rungwe kijiografia lipo mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya ya Rungwe.

Sasa je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi maeneo ya Ikuti, ili kuwaepushia shida wanayoipata kwa sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, eneo la Ikuti ambalo ametuambia Mheshimiwa Mbunge lipo mbali sana na eneo Makao Makuu ya Wilaya ya Rungwe, anapendekeza tujenge jengo la Polisi pale na ndiyo dhamira ya

Serikali. Kama utakuwa umefatilia hotuba ya Waziri wa Fedha mwaka huu, tumesema tunataka kujenga vituo vya Polisi karibu kila Kata. Tayari Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imezungumza na TAMISEMI kuhusu mikakati ya kujenga vituo hivyo imeanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba, eneo hili la Ikuti - Rungwe ni moja ya maeneo yatakayonufaika na mpango huu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Je, ni lini sasa Serikali mtaendeleza kujenga nyumba za askari pale *Kilwa Road Barracks?* Kwa sababu majengo mengine yamejengwa lakini mengine bado hayajaendelezwa. Naomba kujua sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunatambua uchakavu wa baadhi ya majengo ya Makazi Jeshi la Polisi pale *Kilwa Barracks.* Ni mpango wa Serikali kama ambavyo tumeanza kujenga zile *flats* ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziona, dhamira ya Serikali ni kuendelea hatua kwa hatua kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, umesikia ikielezwa hapa kwamba tumefanya Dar es Salaam lakini maeneo mengine bado yanalia. Katika hali ya kutaka ku-*balance* kadri tutakavyofikiwa basi Dar es Salaam tutaiendeleza kadhalika pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri maadamu umezungumzia hapo mipango, tunarejea tena kwenye Tume yetu ya Mipango naamini Waziri atakuwa anatusikia popote alipo. Kwa sababu makazi ya Polisi kila mahali ni changamoto kubwa. Sasa ili huo ukarabati uende vizuri mkiwa na mipango basi na sisi huko maeneo yetu tunakuwa tunajua mwaka gani Polisi wataanza kukaa mazingira mazuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni vizuri mipango iwekwe kama ulivyosema kwa sababu upatikanaji wa fedha hazipatikani kila siku ama kila wakati, sasa zile zinazopatikana basi hapa mkifanya, mfanye tujue kuna eneo mmeshafanya mmemaliza mnahamia sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Busokelo, Kituo cha Polisi wanachotumia ni lililokuwa Jengo la Posta; ni lini mtaweka kituo kizuri ambacho kitasaidia huduma ya wananchi katika Jimbo lile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunafahamu changamoto ya maeneo mapya ya utawala ambayo yanaanzishwa kwa dhamira njema ya kusogeza huduma kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na huduma za usalama, ndiyo maana wakati maeneo haya yakianza wenyeji kwa maana ya wenye maeneo Wilaya husika walibainisha, kama tukianzisha Makao Makuu Wilaya mpya huduma hii itafanyikia wapi? Kwa kutambua changamoto hiyo, ndiyo maana Wizara ya Mambo ya Ndani imeshabaini Wilaya zote ambazo hazina vituo vya ngazi ya Wilaya vya Polisi na tunaendelea kujenga kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, ninakuahidi Mheshimiwa Mwakagenda kwamba, Busokelo litakuwa ni eneo pia litakalotiliwa maanani tunavyoendelea kutekeleza mpango wetu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa sijajua na leo unakaimu kwenye Wizara hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imejenga majengo mazuri sana ya Makao Makuu ya Polisi katika Mkoa wa Kusini Unguja, Tunguu na Mkoa wa Kaskazini Unguja na yamezinduliwa, tuliyashuhudia katika ziara ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa UWT Taifa. Je, ni lini sasa majengo haya yatapatiwa samani ili yaanze kutumika kutokana na uwekezaji mkubwa mliofanya Serikali wa zaidi ya shilingi bilioni tatu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Mbunge kutambua juhudi ambazo zimefanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutengeneza mazingira ya kutolea huduma za kiusalama yakiwemo majengo ya Polisi ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi ni hatua, kukamilisha majengo ni jambo moja na uwekaji wa samani ni jambo la pili. Hatua itakayofuata ni kuruhusu majengo yaanze kutumika na Jeshi la Polisi limejipanga vema katika bajeti yake ya mwaka huu kuyapatia samani majengo hayo, yakiwemo hayo ya Tunguu na Kusini Unguja. Nashukuru.

**SPIKA:** tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 142

**Fidia kwa wananchi waliopisha upanuzi wa eneo la Jeshi - Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi waliopisha upanuzi wa maeneo ya Jeshi 843 KJ Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Jeshi cha 843 JKT Nachingwea, kilichopo Mkoani Lindi kilianzishwa mwaka 1964. Kumbukumbu zinaonesha eneo husika lilikuwa ni moja ya mashamba ya karanga yaliyokuwa yanamilikiwa na Mzungu aliefahamika kwa majina ya John Molam. Shamba hilo baadae lilitaifishwa na Serikali na kutumika kwa matumizi ya Kijeshi kwa ajili ya kuimarisha Ulinzi katika mipaka ya Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1964 wakati Jeshi wanakabidhiwa eneo hilo, upande wa mpaka wa Mashariki kikosi kilipakana na Kijiji cha Naipingo, baadaye eneo la Jeshi katika mpaka wa upande huo lilikatwa na kuanzishwa Kijiji cha Mkukwe ambacho kilisajiliwa Mwaka 1999. Kwa sasa kikosi kinapakana na Kijiji cha Mkukwe katika upande huo wa Mashariki. Upimaji mpya wa kurekebisha mipaka uliofanyika mwaka 2021 na Hatimiliki yake imetolewa 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo hakuna upanuzi uliofanywa wa kuongeza eneo la kikosi, bali eneo la Jeshi ndilo lilipunguzwa na kuanzisha kijiji cha Mkukwe Mwaka 1999. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante, swali langu la kwanza la nyongeza ni kwamba Kikosi cha 41 KJ Nachingwea pia kuna maeneo yalitwaliwa na Jeshi. Ni maeneo ambayo wazee wetu waliyatunza miaka mingi sana.

Je, Serikali haioni haja ya kuwalipa fidia wazee hao?

Swali la pili, kwa kuwa wazee waliyatunza maeneo yote hayo kwa muda mrefu na ilikuwa ni tegemeo kwa maisha yao. Je, Serikali haioni haja kweli ya kuwalipa hata kifuta jasho kidogo ili maisha yaendelee? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa swali la msingi nililolijibu inaonesha kwamba hakuna mgogoro, lakini kwa swali la nyongeza aliloliuliza Mheshimiwa Mbunge Pathan, naomba nilichukue ili kuelekeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kikosi cha 41 KJ, walifuatilie na kuleta taarifa stahiki ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Oldonyosambu wamechukuliwa maeneo yao na Jeshi miaka 20 sasa imepita na zaidi. Je, ni lini itawalipa fidia wananchi wale ambao wametoa eneo lao katika Kata ya Oldonyosambu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwenye hili la Oldonyosambu pia ni suala jipya kwangu. Kama Naibu Waziri niliyeshikilia jambo hili, naomba nilichukue ili tuwasiliane na Waziri mwenye dhamana na chombo chenyewe cha jeshi, kuona uhalali. Kama ambavyo tumesema wakati wote, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, haiko tayari kuona wananchi wake wakidhulumiwa au kunyimwa haki wanayostahili.

Mheshimiwa Spika, ikithibitika kwamba wanastahili kulipwa fidia, basi hatua stahiki zitachukuliwa ili wananchi hawa waweze kulipwa inavyopasa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, pale Musoma Mjini kwenye Kata ya Makoko pamoja na Buhare kulikuwa na mgogoro kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi; Waziri aliyekuwepo, Mheshimiwa Bashungwa, alikuwa amekubali kwenda kuonananao, kwa bahati mbaya baada ya kuwa amebadilishwa, sasa nataka kufahamu, ni lini Waziri aliyepo atakubali kwenda kutatua ule mgogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri hilo uondokenalo. Ni mpaka Waziri atakapoulizwa ndiyo atakayeweza kujibu. Kwa hiyo, utampa jibu baada ya kufuatilia kwa Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu safari ya kwenda huko kwenye mgogoro.

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 143

**Uhitaji wa mabwawa ya maji, Singida Mashariki**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itachimba Mabwawa ya maji Kata za Kikio, Misughaa, Lighwa, Mungaa, Siuyu, Issuna na Mkiwa – Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ikungi ina jumla ya kata 28 zikiwemo Kata za Kikio, Misughaa, Lighwa, Mungaa, Siuyu, Issuna na Mkiwa. Vyanzo vikuu vya maji katika kata hizo ni maji chini ya ardhi kupitia visima vilivyochimbwa na kuwekewa miundombinu ya kutolea maji. Vijiji vyote vya Kata za Mungaa, Siuyu, Issuna na Mkiwa vinapata huduma ya maji kwa kutumia visima vilivyochimbwa kwenye vijiji hivyo. Aidha, baadhi ya vijiji katika Kata za Kikio, Misughaa na Lighwa bado havijapatiwa huduma ya maji ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira zinatosheleza katika Wilaya ya Ikungi Ikiwemo Kata za Kikio, Misughaa, Lighwa, Mungaa, Siuyu, Issuna na Mkiwa, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano kuanzia 2022/2023 – 2025/2026 wa kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua ili yatumike wakati wa kiangazi sambamba na kudhibiti mafuriko. Mwaka 2024/2025 itafanya usanifu wa kina na kubaini maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa katika kata hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa *coverage* ya maji katika Wilaya ya Ikungi ni asilimia 53 ambayo iko chini sana, kuna maeneo ambayo yana changamoto kubwa. Sasa nataka tu nijue, ni nini mpango wa Serikali wa muda mfupi kuwapatia maji wananchi wa Wilaya ya Ikungi kwa maana ya Kata za Kikio katika

Kijiji cha Nkundi, Lighwa katika Kijiji cha Mwisi na Issuna katika Kijiji cha Issuna A, Kitongoji cha Manjaru?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuna visima vilivyochimbwa ambavyo bado havijawekewa miundombinu. Nilitaka nijue kwamba, visima hivyo katika vijiji vya Msule, Mkinya, Mang'onyi na Mbwanchiki pamoja na Ujaire.

Ni lini sasa Serikali itatenga fedha ya kujenga miundombinu ili kuondoa adha ya maji katika maeneo haya niliyoyataja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mfupi kwenye kata na vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mtaturu, ni kwamba tutaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha tunakuja kuchimba visima.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu nimwagize *RM* Singida, ahahakikishe anakwenda kwenye hizi kata, wafanye usanifu ili kuona wapi tunaweza tukapata maji chini ya ardhi ili sasa waweze kupelekewa gari wakachimbe visima na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, lini tutatenga fedha kwa ajili ya miundombinu kwenye visima tulivyochimba; kwa utaratibu wa Wizara, tukishachimba visima kazi inayofuata ni usambazaji. Kwa hiyo, nina uhakika kama mwaka huu wa fedha kwa maana ya kuanzia leo mpaka Juni, Wizara tukawa tumepata fedha ambazo hazitoshelezi kuwafikia, mwaka ujao wa fedha lazima maeneo haya yote tuje tusambaze maji katika visima ambavyo tumevichimba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Mabwawa mawili, Bwawa la Luguru na Bwawa la Mwamapalala, Wilaya ya Itilima, Mkoa wa Simiyu yana hali mbaya, yamejaa tope: Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa mabwawa hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabwawa haya aliyoyataja niseme tu kwamba, tuko kwenye utaratibu wa kuona kama tutaweza kuendelea kuyatumia tuje tuweze kuyakarabati. Pia kwa Mkoa wa Simiyu tuna mradi mkubwa sana ambao unakwenda kutatua changamoto ya maji katika maeneo haya mengi. Kwa hiyo, huenda tusikarabati, lakini tukautumia mradi ule wa mabadiliko ya tabianchi kuhakikisha maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tunayapelekea maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mji wa Kisesa na Bujora una hali mbaya sana ya upatikanaji wa maji; na kwa kuwa Serikali imetoa fedha kujenga *tank* kubwa la *cubic meter* milioni tano: Je, ni lini usabazaji wa mabomba utaanza katika Mji wa Kisesa na Bujora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yapo kwenye mchakato wa utekelezaji wa mradi mkubwa ambao huu Mji wa Kisesa tayari mabomba makubwa ya nchi 10 yameshaanza kulazwa kama kilometa tatu hivi, lakini tayari mabomba ya nchi nane pia yako pale *site*. Kwa

hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge. Nimpongeze kwa kufuatilia, lakini hizi kazi tayari zimeanza, na amekiri *tank* kubwa linajengwa pale Bujora, na penyewe pia utaratibu unaendelea wa kuongeza mabomba ambayo yatatosheleza mradi huu mzima wa Kisesa na Bujora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kutokana na tatizo la maji katika Wilaya hizi za Mkoa huu wa Dodoma, naomba niulize swali kwamba ni lini Bwawa la Farkwa litaanza ujenzi kama ilivyo katika mkakati wa Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kusema nina furaha kubwa sana kwa sababu, sasa ujenzi wa Bwawa la Farkwa upo tayari kwenye *pipe*. Ni wiki iliyopita tu wameweza kusaini mkataba wa kazi hii kuanza na tutarajie kazi itakwenda vizuri kwa sababu ni mradi ambao tunautarajia sana katika kupunguza changamoto ya maji kwenye Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, sasa aulize swali lake.

Na. 144

**Kusambaza umeme Kata za Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme kwenye Kata za Kikeo, Kinda na Maskatl – Mvomero?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mvomero ina jumla ya vijiji 129 ambapo kati ya hivyo, vijiji 92 tayari vimeshapatiwa umeme. Vijiji 37 vilivyosalia ambavyo baadhi vinapatikana katika Kata ya Kikeko, Kinda na Maskati vitapatiwa umeme na mkandarasi ambaye yupo maeneo ya mradi anaendelea na kazi za ujenzi wa miundombinu. Mkandarasi huyu anatarajia kukamilisha kazi ifikapo mwezi Juni, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa Mvomero ni miongoni mwa Wilaya ambazo ziko vijijini; na kwa kuwa, Kijiji cha Madizini, Lusanga, Manyinga, Turiani, Kilimanjaro na Kichangani, havikuwahi kupata hadhi ya kisheria kuwa miji midogo; Mheshimiwa Naibu Waziri, huoni sasa kuna haja ya kutoa maelekezo wananchi wa vijiji hivi walipie umeme kwa shilingi 27,000 badala ya kulipia umeme kwa shilingi 321,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wananchi wa Tarafa ya Turiani wamekuwa wanapata adha kubwa sana ya kukatika kwa umeme: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, huoni sasa ni wakati muafaka kutenga bajeti ya kwenda kuboresha miundombinu hii inayotoka Morogoro kuelekea Turiani ya kupeleka umeme kwa sababu miundombinu hii ni ya muda mrefu na imechakaa kwa kiwango kikubwa sana? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas Zeeland, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Vijiji vya Madizini, Lusanga, Manyinga, Kilimanjaro, Kichangani na Turiani, vilitolewa tangazo, lakini havijaidhinishwa kama miji midogo. Kwa hiyo, niwaelekeze *TANESCO* Mkoa wa Morogoro kuendelea kuwa-*charge* wananchi 27,000 kwa maeneo haya yote ambayo hayajaidhinishwa kama miji kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la pili la *line* ya umeme inayotoka Turiani kwenda Kilosa na Gairo, mwaka huu wa fedha tumetenga bajeti ya matengenezo. Nikuahidi, kama matengenezo hayatakamilika, mwaka ujao wa fedha tutaendelea kutenga bajeti ili kuhakikisha tunaboresha miundombinu hii ili wananchi waendelee kupata umeme wa uhakika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona; ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vitongoji zaidi ya asilimia 70 katika Wilaya ya Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali tumeanza mpango wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote vilivyobakia 36,000. Kwa kuanza, tumeanza kwa miradiya ujazilizi ambayo tumeshaweka wakandarasi na vilevile tunategemea kuendelea kutafuta wakandarasi kwa Mradi wa Vitongoji 15 kwenye kila jimbo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vitongoji katika Jimbo la Kyerwa na vyenyewe vitafikiwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, lini wananchi wa Jimbo la Bunda watapata umeme wa *REA II C* kwa vijiji 147?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mradi wetu wa *II C* tumetenga vitongoji 17 na kwa mradi ujao pia, vitongoji 15 Jimbo la Bunda litapata. Kwa hiyo, kwa kuanzia wataanza na vitongoji 32, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, tulisema mpaka mwezi wa 12 mwaka huu, vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme na bado kuna vijiji kama Kiteto hatujapata umeme. Nini kauli ya Serikali kwa mpango huu wa mwezi wa 12 vijiji vyote vipate umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edward Olelekaita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Wakandarasi wote ambao tumewapatia mikataba ya kwisha Desemba 30, kupeleka umeme kwenye vijiji vyote, lazima wakamilishe kupeleka umeme kulingana na mikataba yao. Wale ambao walipewa ziada mpaka Juni, 2024 wata-*cross* kwenda 2024. Niwaelekeze

Wakandarasi wote, yeyote ambaye hatahakikisha anamaliza mkataba wake kwa muda, bila sababu za msingi, hatutasita kuchukua hatua na kuweza kutokuendelea na mkataba wake ikifika Desemba, 30 mwaka huu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa vitongoji vinavyopewa umeme ni vile ambavyo *line* za umeme kubwa tayari zilishapita, lakini kwenye jimbo langu kuna Kitongoji kama Nindi na Songeapori ambavyo viko mpakani na kuna changamoto kubwa za kiusalama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvisaidia vitongoji hivi viwili kwa jicho la kipekee? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vitongoji hivi viwili kwa kweli, vimekaa kimkakati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa awamu hii ya ujazilizi utaweka *addition scope* ili vitongoji hivi viweze kufikiwa na umeme kwa umahususi wake, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme wa *REA* katika Kata ya Nanjirinji na Kata ya Likawage, umekwama kwa sababu ya mgogoro kati ya *TFS* pamoja na mkandarasi. Nini Kauli ya Serikali katika kutatua mgogoro huu ili wananchi wapate umeme huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge nikuahidi, nitafuatilia suala hili ili kuhakikisha linatatuliwa kwa wakati na wananchi waweze kupata umeme katika maeneo yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji sita vilivyobakia kwenye Tarafa ya Mikumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkandarasi katika vijiji hivi yuko *site* anaendelea na kazi. Nimhakikishie tu, ifikapo Juni, 2024 vijiji hivi vyote vitakuwa vimepatiwa umeme, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Na. 145

### Ujenzi wa Chuo cha *CBE* Chwaka

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa aulize swali hili ameliondoa swali lake kwa maana ya kwamba, alishajibiwa na Serikali.

Tunaenda Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 146

**Athari za kuondoa *buffer zones* kwenye hifadhi na mapori ya akiba**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kupunguza athari hasi zitakazojitokeza kutokana na kuondolewa kwa *buffer zone* katika hifadhi na mapori?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kinga za hifadhi za wanyamapori husaidia wanyamapori kupata mahitaji yao ikiwemo malisho na hivyo kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza athari za kutokuwa na maeneo ya kinga, Wizara kupitia taasisi zake za uhifadhi *(TANAPA, TAWA* na *NCAA)* inatoa elimu kwa wananchi kuhusu kutokuanzisha shughuli za kibinadamu kama vile kilimo na makazi kwenye maeneo ya karibu na hifadhi ili kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na wanyamapori.

Vilevile kuwaelimisha kuanzisha shughuli rafiki kama vile ufugaji nyuki kwenye maeneo hayo. Sambamba na hatua hiyo, jitihada za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu zinafanyika ili kulinda wananchi na mali zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuondoshwa kwa maeneo ya kinga *(buffer zone)* kunasogeza zaidi wananchi karibu na hifadhi na kuwahatarisha na wanyama wakali na waharibifu: Je, Serikali haioni haja ya kuja na mikakati zaidi ya kutoa elimu ili kuwasaidia wananchi hawa kuwaepusha na hiyo hatari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa *buffer zone* kitaalam inalenga kuwatenga wananchi na maeneo ya hifadhi na hivyo, kupunguza vitendo vya uharibifu na vitendo vya uvamizi.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, utaratibu huu wa kuondoa *buffer zone* katika maeneo ya hifadhi haujirudii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu**.**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohammed Soud Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wizara inajielekeza sana kwenye kutoa elimu. Sambamba na hiyo, kwenye maeneo ya namna hii vilevile tuna mikakati ya kuwahamasisha wananchi kufuga nyuki kwenye maeneo hayo. Vilevile, kuendesha utalii wa kiutamaduni, kupanda au kutunza misitu ili waweze kuja na mfumo wa biashara ya uvunaji wa Hewa ya Ukaa. Tunaamini wananchi wakijielekeza kwenye maeneo haya, basi huo muingiliano utapungua athari zake.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, ni kweli kwamba maeneo haya ya *buffer zone* yanalenga kuwatenga wananchi na maeneo ya hifadhi ili kuwaondolea athari ya madhara ya

uvamizi na hivi. Pamoja na kutoa elimu, Wizara inajielekeza kwenye kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi na kutoa elimu kwa viongozi na wananchi. Imani yetu ni kwamba, elimu hii ikiwaingia wananchi na wakazingatia maelekezo haya, basi migogoro hii itaondoka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali kwa kifupi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wanyama hao walioko katika maeneo yetu ya uhifadhi, mara baada tu ya kuvuka kwenye *buffer zine* wanaingia kwenye ardhi za vijiji.

Je, Wizara au Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya Wizara kukaa na vijiji vinavyozunguka maeno ya hifadhi ili kwa pamoja waweze kuweka utaratibu rafiki wa namna ya kusimamia wanyama pori nje ya hifadhi za Taifa na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ole-Sendeka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikifanya jambo hili ambalo Mheshimiwa Ole-Sendeka amelishauri. Sambamba na hilo, tumekuwa tukishirikiana vilevile na Wizara ya Ardhi katika kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi. Tunaamini kwa kufanya hivyo tutaepuka changamoto tunazokabiliana nazo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 147

**Umuhimu wa kugawa mizinga ya nyuki Iringa**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kugawa mizinga ya nyuki ili kubadili shughuli za kiuchumi zinazoharibu mazingira kama kukata miti na mkaa Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa mizinga na vifaa vingine ni mojawapo ya mikakati ya Serikali katika jitihada za kuwezesha makundi mbalimbali ya kijamii kushiriki katika shughuli za ufugaji wa nyuki hapa nchini. Zoezi la ugawaji wa mizinga lina lengo la kuchochea ufugaji nyuki kwa jamii hasa zile zinazoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa ili ziweze kujipatia kipato na kuachana na shughuli zinazoharibu mazingira kama kukata miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha uhifadhi wa maeneo mbalimbali ambapo kupitia Mradi wa *REGROW* imetoa elimu ya Ufugaji nyuki kwa jamii ya Tungamalenga na kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kuwagawia mizinga 50 kwa kikundi cha Subira kilichopo Wilaya ya Iringa. Vilevile elimu ya ufugaji nyuki imeendelea kutolewa kwa jamii zinazozunguka hifadhi ambapo kupitia elimu hiyo wananchi wamefundishwa namna bora ya kufanya shughuli za ufugaji nyuki kwa tija.

Mheshimiwa Spika, mathalan kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitoa mizinga 269 yenye thamani ya shilingi milioni 26.9 kwa vikundi 19 vya wafugaji wa nyuki katika Wilaya za

Iringa, Kilolo na Mufindi. Vilevile Mfuko wa Misitu Tanzania umetoa ruzuku ya shilingi millioni 20 kwa vikundi viwili vya ufugaji Nyuki vilivyopo Wilaya ya Iringa. Pia, wadau wa maendeleo wametoa mizinga 260 kwa wafugaji nyuki katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na wadau wa maendeleo, itaendelea kutoa elimu ya uhifadhi na mbinu bora za ufugaji nyuki ili jamii iweze kufuga nyuki kibiashara. Aidha, Mfuko wa Misitu Tanzania umekuwa ukitoa tangazo na kupokea maombi ya ruzuku zitolewazo kwa wadau wa misitu na ufugaji wa nyuki. Hivyo, Mfuko unaendelea kupokea maombi ambayo yanachakatwa ili waombaji waweze kunufaika na ruzuku hizo ikiwemo kupatiwa mizinga ya kufugia nyuki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba sasa niwe na swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri umeyaeleza, vikundi vingi vilivyopewa mizinga hiyo ni vya Wilaya ya Iringa lakini kutoka Iringa Vijijini na Iringa Manispaa ni lango la utalii Kusini.

Je, mpo tayari sasa kutupatia na Iringa Manispaa ili angalau uoto wa asili urudi kwa kufuga nyuki? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara tutakapopata orodha ya vikundi vilivyoanzishwa kwa jambo hili, Wizara itaona jinsi ambavyo inaweza kushirikiana na hamashauri ili kuweza kuwapatia mizinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya

Uchukuzi, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 148

**Mkandarasi wa *SGR* kuajiri wananchi katika maeneo ambayo reli inapita**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, Mkandarasi wa *SGR* kipande cha Seke-Malampaka hadi Malya ameajiri wananchi wangapi wanaotoka maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRC* imeendelea kumuelekeza mkandarasi wa ujenzi wa reli ya *SGR*, kuendelea kutoa ajira kwa wananchi wanaopitiwa na mradi, sambamba na kufuata taratibu na sheria za ajira nchini. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa *SGR* kipande cha Mwanza - Isaka (kilometa 341), kinachojumuisha kipande cha Seke - Malampaka hadi Malya kama sehemu ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira; hadi kufikia mwishoni mwezi Agosti 2023, mkandarasi ameajiri jumla ya wananchi 6,793. Kati ya hao, wananchi 1,639 kutoka Mkoa wa Shinyanga, wananchi 1,973 kutoka Mkoa wa Mwanza, wananchi 525 kutoka Mkoa wa Simiyu, wananchi 352 kutoka mkoa wa Tabora na wanachi 2,304 kutoka mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kumsimamia Mkandarasi kuhakikisha kuwa anaajiri kwa kutoa kipaumbele

kwanza kwa wananchi wa maeneo husika kabla ya kutafuta ujuzi stahiki kutoka maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kuna malalamiko kwamba hata kazi ndogo ndogo kama za usafi, kufyeka na ulinzi, mkandarasi anatoa wafanyakazi maeneo ya mbali badala ya maeneo ya Seke, Malampaka na Malya. Je, Serikali inamshauri nini mkandarasi huyu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa pia kuna malalamiko kwamba mkandarasi ambaye ndiyo mwajiri hapeleki au anapeleka michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kusuasua, je Serikali inasemaje juu ya malalmiko haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, amezungumzia kuhusiana na watu wengi kutoka nje ya eneo la mradi. Moja, nimetoa takwimu ya watu ambao wameajiriwa kutoka kwenye eneo hilo katika Mkoa wake wa Shinyanga.

Pili, nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu ni wa Kitaifa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kumsimamiwa na kumsisitiza kwamba, anatafuta kwanza wafanyakazi kwenye eneo husika kabla hajepeleka kipaumbele kwenye maeneo mengine ya nje ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, hoja yake pili ni kuhusiana na michango ya *NSSF*, kwamba pengine mkandarasi anasuasua. Tunafahamu Sheria ya *NSSF (The National Social Security Act) Revised* ya 2018 *Cap. 50*, inamtaka mkandarasi au mwajiri kuhakikisha kwamba anapeleka makato hayo *NSSF* mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kuna changamoto kubwa sana kwenye upande wa mkandarasi huyu kwa sasa. Tayari tumeshaanza vikao kupitia wenzetu Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa ajili ya kukaa naye na kuweka *commitment*, mara tu anapolipwa fedha aweze kupeleka michango hiyo kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Pia, aweze kuwalipa na wazabuni mbalimbali wa ndani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, napenda tu kuongezea kwenye kile kipengele cha mkandarasi kutopeleka michango kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*.

Mheshimiwa Spika, nakiri kweli kuna madai ambayo mkandarasi anadaiwa na Mfuko umekuwa ukifatilia madai hayo na kuna makubaliano ambayo *NSSF* imeweka na mkandarasi ambapo tunataka madeni haya yakamilike ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, nimesimama pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kuna utaratibu ambao umewekwa kati ya *NSSF* na mkandarasi kwa wale ambao wanatakiwa kulipwa mafao yao sasa, kuna utaratibu maalum wa fedha zao kupatikana ili wasiathirike na malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba, kama Wizara ambayo tunasimamia mifuko ya hifadhi ya jamii, tutahakikisha kwamba madeni haya tunayafatilia ili haki za wafanyakazi zisipotee. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 149

***NHIF* kuzuia matibabu ya wagonjwa wenye Bima za Afya**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, kwa nini *NHIF* inazuia matibabu ya baadhi ya wagonjwa wenye Bima za Afya wakiwa hospitali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na zoezi la uhakiki wa uhalali wa wanufaika wa Mfuko wa Bima ya Afya. Zoezi hilo lilileta usumbufu ambao ungeweza kuzuilika kama wahakiki hao wangetumika wataalamu wenye miiko ya taaluma ya tiba. Wizara ilipopata malalamiko hayo ilifuatilia mara moja na kufanya maboresho ambayo yaliyoondoa usumbufu kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuielekeza Menejimenti ya Mfuko wa Bima ya Afya katika kipindi cha miezi mitatu, ihakikishe inaboresha mifumo ya TEHAMA itakayoweza kuondoa usumbufu na pia kudhibiti udanganyifu pasipo kuwa kero kwa wanufaika wa Mfuko, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba, jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri ni zuri sana. Ni jibu la ukweli na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza; kwa kuwa ni kweli kwamba baadhi ya watumishi wamelelewa kama watoto yatima lakini wamelelewa na watu ambao siyo *biological fathers* au *parents* na tofauti ya majina ndiyo iliyoleta shida ya kufutiwa hizo *NHIF*, ni utaratibu upi wa haraka unafanywa ili hao waliofutiwa waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wakati wa zoezi hili wako watu walinyang'anywa kadi hizi wakiwa hospitali na wale watumishi wakapelekwa polisi na kufunguliwa mashtaka. Ni nini kimefanyika Wizara ya Afya, kwanza kuwaachia wale watumishi lakini kufuta mashtaka hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Kanyasu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, anaelezea kwamba kuna watu ambao wamelelewa na wazazi ambao siyo wazazi wao *biologically* lakini ndiyo walezi wao ambao wamewalea. Kwa sababu sasa ndiyo tumepitisha juzi Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote na tunaenda kutengeneza kanuni na taratibu, mafikiri jambo ambalo amelizungumzia hapa litaenda kuangaliwa kwa kina na kuona ni namna gani linaweza likatatuliwa lisiweze kutokea tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia amezungumzia wale ambao wamekutwa wakiwa hospitalini na wamenyang'anywa na wengine wameshtakiwa. Mimi ninachoweza kusema kuna pande mbili. Kuna ambaye amenyang'anywa lakini kweli amelifanya hilo kosa, taratibu za kisheria zitachukua mkondo wake lakini kuna wengine ambao ni makosa mengine ya wataalam wetu kutoa kadi inayotofautiana jina na hali halisi iliyoko kwenye vyeti vyake. Hilo tutaenda kuangalia kwa *individual* na kuona jinsi ya kutatua. Kwa sababu, pia inawezekana kwenye jimbo lako kuna mambo yaliyotokea kama hayo.

Mheshimiwa Spika, tutaenda kuangalia *specifically* tuone namna gani tutatatua kwa pamoja na tutumie mfano huo

kutatua mengine, kwa maana ya nchi nzima. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa anayezungumza na simu tafadhali. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Nanchingwea, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 150

**Kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo wa madini - Nachingwea**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa leseni kwa wachimbaji wadogo wa madini Kata za Nditi na Kiegi – Nachingwea na maeneo mengine ya Mkoa wa Lindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini hadi Oktoba 2023, imetoa jumla ya leseni 2731 za uchimbaji mdogo wa madini katika Mkoa wa Lindi. Aidha, leseni zaidi ya 200 za Uchimbaji Mdogo wa Madini zimetolewa katika Vijiji vya Kiegei na Nditi Wilayani Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini itaendelea kutoa leseni za madini katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Wilaya ya Nachingwea na maeneo mengine ya Mkoa wa Lindi kadri itakavyokuwa ikipokea maombi ya leseni kutoka kwa wananchi ili kuwezesha ushiriki wao katika uchumi wa madini, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Ziko Leseni zimetolewa kwa ajili ya shughuli za utafiti kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Jimboni Nachingewa lakini wahusika hawajafanya shughuli hiyo iliyokusudiwa kwa muda mrefu sasa.

Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kupitia sheria yetu ili kuweza kuondoa utitiri wa hawa watafiti ambao kimsingi hawatimizi majukumu hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi baada ya kipindi hiki cha Bunge ili kwenda Jimboni Nachingwea kuona halihalisi iliyoko na kuwatia moyo wachimbaji wadogo wadogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Chinguile, Mbunge makini wa Nachingwea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu waliopewa leseni na wamezilaza hawazifanyii kazi; mwezi wa tisa na mwezi wa kumi tulitoa kama ndiyo kipindi cha mwisho, waweze aidha kufanyia leseni zao kazi au zifutwe. Tangu tangazo hilo litoke, zaidi ya leseni 7,000 zimeshahuishwa na kuna wale ambao hawajaweza kuhuisha mpaka tarehe 30 mwezi uliopita, mchakato wa kuzifutia hizo leseni unaendelea. Hatukuishia hapo, zilizokwishaharibiwa kwa kutofanyiwa kazi huko nyuma, maeneo zaidi ya 48 zimegawiwa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, hivyo hata katika jimbo lake, wale ambao watashindwa kuendeleza leseni kwa mujibu wa tangazo hilo la Serikali kupitia Wizara ya Madini, watarudisha hizo leseni na tutawapa wale ambao wako tayari.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, mimi niko tayari baada ya Bunge hili, nitampangia ratiba. Tutafika huko tuwatie moyo wachimbaji wadogo wanaofanya shughuli zao na

kuwahamasisha wengine watumie fursa zilizoko katika Wizara ya Madini kupata uwekezaji ambao utawainua katika Maisha yao. ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale sasa aulize swali lake.

Na. 151

**Ujenzi wa barabara ya Kahama – Nyang'hwale – Busisi**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, ni lini upembuzi yakinifu utakamilika na kuanza ujenzi wa barabara ya Kahama – Nyang'hwale – Busisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zabuni ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kahama, Nyang'hwale hadi Busisi yenye urefu wa kilometa 162.9, inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari 2024. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinatarajiwa kuchukua muda wa mwaka mmoja. Hivyo kazi zitakamilika mwezi Februari, 2025. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa sijaridhika sana na haya majibu, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mzabuni tayari ameshapatikana…

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja, hujaridhika kwamba ni majibu hayana..., yaani siyo ya kweli, hayana uhalisia ama? Kwa sababu kanuni zetu zinataka swali lijibiwe kikamilifu. Hujaridhika kwa namna gani?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, majibu haya hayana uhalisia.

**SPIKA:** Fafanua.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mzabuni tayari amepatikana na anaenda kupata Msanifu Mshauri na kuianza kazi hiyo mwaka 2024 na kumaliza 2025. Kwa nini nasema kwamba halipo sawasawa, fedha ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya usanifu kwa mwaka wa fedha 2021 na kutolewa mwaka 2022, fedha hiyo ilitengwa shilingi milioni 300 na kutolewa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuanza kazi hiyo mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, leo ananiambia anaenda kupatikana Msanifu mwaka 2024 na kumaliza kazi hiyo mwaka 2025, hapa majibu haya yanakinzana.

Mheshimiwa Spika, niendelee?

**SPIKA:** Sawa, ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri afafanue hiyo sehemu yako ya kwanza, ndiyo uulize maswali yako ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hata katika jibu langu la msingi, siyo kwamba Mhandisi Mshauri

amepatikana. Ila tayari zabuni ya manunuzi kumpata huyo Mhandisi Mshauri, ndiyo tunakwenda kutangaza.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya 2022/2023 tulitenga bajeti kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Hiyo bajeti ambayo imetupelekea sisi kuanza kutangaza na hata katika mwaka huu wa fedha pia kwenye vitabu vyetu vya bajeti, bado tumetenga katika kuendelea kufanya hiyo kazi ya usanifu wa kina wa barabara hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Sawa, hapo kwenye jibu lako panaposema hivyo, kazi zitakamilika mwezi Februari, 2025. Ni kazi zipi, hizi za usanifu ama za ujenzi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kazi za usanifu, kwa barabara ilivyo haiwezi ikafanyika…

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kazi zitakazokamilika 2025 siyo za ujenzi ni kazi hizi za usanifu unaoendelea ndiyo zitakamilika Februari, 2025. Haya uliza maswali yako mawili ya nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Mheshimiwa Spika, kwenye kikao cha ushauri wa barabara cha mkoa, mwaka 2022 niliambiwa zimeshatoka shilingi milioni 150 na kazi ya upembuzi yakinifu imeanza…

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassor, ngoja. Ili taarifa zetu zikae vizuri kule ulipoambiwa siyo Serikali Kuu inayokuwepo, ni nyinyi watu wa mkoa ule ndiyo mpo kule. Kwa hiyo nilitaka ufafanuzi huu ili taarifa zetu zikae vizuri, kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua kwamba kazi zitakazokamilika ni hizi zinazoendelea mpaka sasa.

Sasa kile kikao kule, wewe ulikuwepo ila mimi sikuwepo wala Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo hawezi kufafanua kuhusu kile ulichoambiwa kule. Kwa hiyo tuanzie hiki cha leo hapa Mheshimiwa, uliza maswali yako mawili ya nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, hata kwenye *Hansard* wakiangalia 2022 ni kwamba imeshatengwa fedha shilingi milioni 150 na kwenye vitabu vya bajeti ilionyesha kabisa kwamba zimeshatengwa na zimetolewa. Sasa hii leo wananiambia ni Msanifu anayeenda kupatikana 2024. Wakati kule tumeambiwa kwamba Msanifu ameshaanza kazi.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwa maelezo yako mwenyewe hapo unasema zimetengwa na zimeshatolewa kwenye bajeti.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kwenye bajeti, nafikiri huwa tunatenga ama?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, zilitengwa shilingi milioni 300 kwa 2020/2021 na mwaka 2022 ni kwamba tayari zikawa zimeshatolewa shilingi milioni 150.

**SPIKA:** Sawa, sasa kwa sababu kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, ametaja. Kwa sababu swali lako linasema, je ni lini upembuzi yakinifu utakamilika na kuanza ujenzi wa barabara ya Kahama - Nyang'hwale - Busisi, jibu la msingi linasema utakamilika Februari, 2025. Nilitaka kujiridhisha hapo uliposema, hujaridhika na majibu. Sasa uliza maswali yako ya nyongeza kuhusu hili ambalo umeliuliza kwenye swali lako la msingi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, basi swali la pili; kwa kuwa ahadi hiyo imechukua muda mrefu, mtoto amezaliwa na amefikisha miaka 14 tangu mwaka 2010 ahadi hii imeahidiwa na Viongozi Wakuu wa Nchi, mpaka leo hii tuna miaka 13 tunakaa tunaambiwa maneno haya. Sisi wana Nyang'hwale tunataka majibu ya Serikali. Hivi ni kweli 2024 unavyosema na 2025 namwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya Bunge hili twende akawaambie wananchi dhamira ya Serikali ya kukamilisha ahadi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri amesimama.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Bashungwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Hussein Amar, naomba hoja yake niichukue. Nimpongeze, juzi tulikuwa tuna kikao, Mheshimiwa Hussein Amar pamoja na Mheshimiwa Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, tulikaa na *Barrick,* kuna barabara ya kutoka Kahama kwenda Bulyanhulu kwenda Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amar, aliomba lami itakapofika kwenye geti la *Barrick* akaomba kipande cha kwenda Jimboni kwake tukae na *Barrick* ili kama kutakuwa kuna bakaa tujenge kile kipande. Kwa hiyo kaka yangu Mheshimiwa Amar naomba aendelee kuwa na *confidence* na Serikali. Hoja yake tumeichukua kwa kadri fedha zitakapopatikana na suala la usanifu tutaweka jitihada, lakini dhamira ya Serikali ni kujenga lami kwenye barabara zote ambazo upembuzi yakinifu umekamilika. Tupo pamoja Mheshimiwa Mbunge na nampongeza kwa namna ambavyo anapambana kwa wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 152

***TBC* kujiendesha kibiashara**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliwezesha Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kujiendesha kibiashara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* linatekeleza majukumu yake kikamilifu kama chombo cha utangazaji cha umma. Serikali ipo katika mkakati wa kukamilisha utungaji wa Sheria ya *TBC* ya mwaka 2023, itakayowezesha kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato. Aidha, *TBC* inazo chaneli za kimkakati kwa ajili ya kuongeza mapato ikiwemo *TBC2, TBC Online, TBC FM* na Radio za Jamii Dodoma na Arusha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuharakisha utungaji wa sheria hiyo, Ili shirika liweze kujiendesha kibiashara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha inalipatia magari shirika liweze kujiendesha na liweze kujitegemea ili liendane na soko nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza la Mheshimiwa Amina, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Shirika la Utangazaji *(TBC)* ambalo linaongozwa kwa *notice* ya Serikali 186 ya mwaka 2007 kutokana na Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2002. Serikali ipo katika mchakato huo wa kuhakikisha kwamba utungaji wa sheria ya mwaka 2003 unafanyika kwa haraka. Sasa tayari tupo katika hatua ya pili ya uchambuzi, baada ya kuwa tumepata maoni mahususi kutoka Wizara ya Fedha. Hivyo, utungaji wa sheria huu upo katika hatua nzuri na baada ya hapo tutafikisha katika Bunge lako tukufu kwa ajili ya utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tayari Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaendelea kuboresha vitendea kazi. Vitendea kazi ni pamoja na magari, ni kweli kabisa tunahitaji kuwa na *OB Van* za kutosha katika kanda zetu, lakini katika mikoa kulingana na ukubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari ametoa fedha kwa ajili ya kuboresha *studio* zetu za *TBC* kwa kiwango ambacho kinaendana na teknolojia ya sasa. Tayari ametoa Shilingi bilioni 3.235 kwa ajili ya *studio* iliyopo Barabara ya Nyerere, kwa ajili ya *TBC* Taifa na *TBC FM*. Vile vile alitoa Shilingi milioni 601.8 kwa ajili ya kuboresha *studio* yetu ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya, kwa sababu hiki ni chombo cha umma ambacho kipo kwa ajili ya kuelimisha, kuburudisha na kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 153

**Maboresho ya Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, rasimu ya Sera ya Taifa ya mwaka 1995, Toleo la 2023 liliwasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri, tarehe 18 Agosti, 2023. Aidha, Wizara imekamirisha maboresho ya rasimu ya sera kwa kuzingatia maoni ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata ni rasimu hiyo ya sera kujadiliwa katika Mkutano wa Kazi wa Baraza la Mawaziri kwa tarehe itakayopangwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kwa maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, nataka nijue Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa mtaridhia kama Wizara kuhamisha Mabaraza ya Ardhi kutoka kwenye wizara kwenda kwenye mfumo wa kimahakama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ili kuongeza ufanisi na usimamizi katika sekta ya ardhi nchini, je, ni lini Serikali itaridhia na kukubali kuanzisha kwa mamlaka ya maendeleo ya ardhi nchini kama zilivyo mamlaka zingine kwa mfano *RUWASA* na taasisi nyingine, ili kuendelea kuimarisha usimamizi na uimara katika kutatua migogoro nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni lini Mabaraza ya Ardhi yatahamishiwa kwenye mhimili wa Mahakama. Jambo hili lipo kwenye mchakato na linapitiwa na mamlaka mbalimbali ili kuona uwezekano wa namna ya kuhamisha mabaraza haya kuyarudisha kwenye mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuunda chombo maalum cha kuendeleza na kusimamia ardhi nchini, Wizara yetu ipo kwenye mchakato wa kuanzisha kamisheni ya ardhi ambayo itasimamia mamlaka hii ya ardhi kwa maendeleo ya Watanzania hawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 154

**Elimu ya madhara ya ukatili wa kijinsia kwa watoto**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kuhamasisha watoto wadogo kukua katika misingi ya kutambua madhara ya ukatili wa kijinsia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mwongozo wa Taifa wa uundaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto ya mwaka 2022, ambapo hadi Juni 2023, jumla ya Mabaraza ya Watoto 651 yameanzishwa kwenye ngazi za mitaa katika mikoa 12 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika mabaraza haya, watoto wamejifunza mbinu na stadi za maisha zinazowapa ufahamu na viashiria vya ukatili. Aidha, katika Mabaraza ya Watoto wanajifunza kujieleza, kujiamini na kujisimamia katika masuala yanayowahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imewezesha uandaaji wa mwongozo wa Taifa wa dawati la ulinzi na usalama wa mtoto, ndani na nje ya shule wa mwaka 2022. Mwongozo huu unahimiza watoto wenyewe kushiriki katika ulinzi wao na kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili vinavyotokea shuleni, njiani na kuelekea nyumbani na vyumbani, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.  Swali la kwanza. ukiacha mikoa 12 ya Tanzania Bara ambayo imefanikiwa kupata haya Mabaraza ya Watoto, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mikoa 14 iliyobaki nayo inapata mabaraza haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; suala la vitendo vya ukatili kwa watoto limekuwa likiendelea siku hadi siku kwenye jamii yetu. Je, Serikali haioni haja sasa yakuja na sheria kali itakayo komesha vitendo hivi?  Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanzisha mabaraza haya katika shule zote za vijijini na mitaani nchi nzima. Serikali pia imeshasambaza Mwongozo wa Taifa wa uwaandaaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto katika halmashauri zote nchini, ambapo utawasaidia kuendesha mabaraza hayo kwa kushirikiana na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Bunge lako Tukufu limeshapitisha sheria na adhabu kali za kukomesha vitendo vya ukatili kwa watoto. Niwaombe wananchi, waendelee kutoa ushirikiano kwa Maafisa Mahakama na kutoa ukweli pale wanapofika katika sheria. Niwasisitize kuwa, mahakama itaendelea kufanya kazi yake pale ukweli watakapoutoa katika sehemu za sheria, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Kabla hatujaendelea na ratiba yetu nitaleta kwenu matangazo niliyonayo hapa mbele na tutaanza na tangazo la wageni.

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika na tutaanza na wageni wangu ambao ni Ndugu Jarvis Matiya ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa *CPA;* Ndugu Joy Phumaphi ambaye ni Katibu Mtendaji wa *ALMA*; Dkt. Abraham Mnzava ambaye anatoka pia *ALMA;* Dkt. Samwel L. Nhiga kutoka Wizara ya Afya; na Ndugu Leah Ndekuka kutoka Wizara ya Afya, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 25 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawa ni wadau mbalimbali wa Vyama vya Siasa; yupo Mheshimiwa Jaji Francis Mtungi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Zitto Kabwe, Kiongozi wa Chama cha Siasa *ACT Wazalendo*, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa wageni mkipunga mikono tunakuwa hatuwaelewi kama mnapunga zile tano au mnapunga mkono kwa maana ya kusalimia. Haya ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dkt. Padri Charles Kitima ambaye ni Katibu wa Baraza la Maaskofu Tanzania *(TEC),* karibu sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Juma Ali Khatib ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza vya Siasa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa cha *ADA – TADEA,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Annamringi Macha, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi – Bara, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Doyo Hassan Doyo, Mwenyekiti Kamati ya Maadili ya Baraza la Vyama vya Siasa ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *ADC,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunae Abdul Mluya, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Siasa ya Baraza la Vyama vya Siasa, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *DP,* karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Juma Duni Haji ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa cha *ACT Wazalendo*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Askofu Benson Bagonza, ambaye ni Askofu KKKT Dayosisi ya Ngara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Askofu Emaus B. Mwamakula ambaye ni Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Vuai Alli Vuai, Naibu Katibu Mkuu Mstaafu CCM – Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Dorothy Semu ambaye ni Makamu Mwenyekiti Bara wa Chama cha Siasa cha *ACT Wazalendo*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Dkt. Lilian Badi, Mwenyekiti wa Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. Rose Reuben ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *TAMWA*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Ndonge S. Ndonge ambaye ni Mweka Hazina na Mwenezi wa Chama cha Siasa – *AAFP*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Rukia Kassim Ahmed, Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa la Chama cha Siasa – *CUF*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Shaffih Dauda ambaye ni mwanahabari, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Ahmed Ally, Meneja Habari na Msemaji wa *Simba Sport Club,* karibu sana. *(Makofi)*

Haya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae pia Ndugu Ally Kamwe ambaye ni Meneja Habari na Msemaji wa Yanga, ahsanteni sana na karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Haji Manara, mdau wa michezo, haya, ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Abdallah Mhomba ambaye anaitwa pia Mzaramo wa Simba, huyu naye ni mdau wa michezo, karibu sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Yohana Musa ambaye ni Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali wengine; tunao wageni nane wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika anao wageni wengine 17 ambao ni wajasiriamali wa Kata ya Bonyokwa, Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Diwani wa Kata hiyo Mheshimiwa Tumike Malilo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, hawa ni Waandishi wa Habari za Michezo kutoka *Global TV,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Mipango na hawa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge wawili kwa maana ya wageni 23 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Mheshimiwa Issa Mtemvu ambao ni walimu wakuu kutoka Halmashuari ya Manispaa ya Wilaya ya Ubungo, Mkoani Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa wanne wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hawa ni Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari Jimbo la Rufiji, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 67 wa Mheshimiwa Noah Ole Saputu ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) kutoka ngazi ya Kata Arumeru Magharibi, Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni jamaa zake kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambao ni walimu kutoka Lushoto, Mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mary Masanja ambao ni wadogo zake kutoka Dar es Salaam na Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ambao ni wapiga kura wake kutoka Bunda, Mkoani Mara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Jamani mmeona mavazi ya wapiga kura kutoka Bunda? Haya, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Masache Kasaka kutoka *RUWASA* Chunya, Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ndugu zake kutoka Songea, Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Pius Chaya ambao wafanyakazi wa *BSS Printing & Marketing* kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Daud ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Juliana Shonza, hawa ni waimbaji wa nyimbo za injili kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jonas Mbunda ambaye ni mwalimu kutoka Mbinga Mkoa wa Ruvuma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Mbozi na Momba, Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Tarimba Abbas ambao ni viongozi Chama cha Watumishi, naamni kipo sawa sawa kutoka Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambaye ni ndugu yake kutoka Karatu, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga ambaye ni jamaa yake kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Lucy Sabu ambao ni makada watiifu wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyo anayetembea huko juu sijui kama ni mgeni au ni Mtumishi wa hapa Bunge nikiwa nimesimama watu wote mnapaswa kuwa mmeketi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wageni 14 wa Umoja wa Vijana wa

Chama Cha Mapinduzi kutoka Kata ya Kikuyu, Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa watano kutoka *Tanzania Agriculture Visionary Youth Association (TAVYA)* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, anatutangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Rais wa Awamu wa Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amenunua magari mengi kwa ajili ya nchi nzima ambayo yanaenda kwenye majimbo yetu pia. Magari kwa ajili ya Maafisa Elimu Msingi lakini pia magari kwa ajili wa wagonjwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baadhi yenu mlishuhudia wakati Mheshimiwa Rais akianzisha zoezi hili na sasa limeshaanza zoezi la kupeleka haya magari kwenye maeneo yetu ya uwakilishi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tangazo hili ni kwa ajili ya kuwajulisha leo yatafanywa makabidhiano kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu zoezi haliwezi kufanyika lote kwa pamoja sehemu ya kupaki hayo magari itakuwa mtihani.

Waheshimiwa Wabunge, magari mengi yameshafika ninazo barua hapa ambazo Mheshimiwa Waziri amenilete, pia ameniletea orodha ya Wabunge ambao wataweza kutuwakilisha kwenye hili zoezi ili wao wakishachukua hayo magari halafu mengine yataendelea kuja kwa kadri muda unavyokwenda na yale ambayo yameshafika hapa si yote ambayo yatakabidhiwa leo, leo yatakabidhiwa ya mfano mengine yataendelea kuja kwenye maeneo yetu ya uwakilishi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nitumie nafasi hii pamoja na kwamba ni tangazo kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi hiyo nzuri ambayo ameifanya kwa ajili ya wananchi

kuhakikisha kwamba huduma zinavyoboreshwa za afya ni pamoja na kuhakikisha wagonjwa wanaweza kuzifikia hizo huduma. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa magari haya ambayo yataenda kwenye Halmashauri zetu na yatatumika naamini kwa kazi ile iliyokusudiwa ya kuwafanya wagonjwa wapate huduma kwa haraka. Pamoja na hayo naamini hii pia itatusaidia kwenye kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa zile takwimu tulizo nazo zitaendela kupungua, kwa sababu sasa wataweza kuwahishwa kwenye maeneo ya kutolea huduma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ukiacha hayo pia kwenye eneo letu la elimu, ninazo barua hapa na yenyewe magari yamenunuliwa na yataletwa kwenye Halimashauri zetu kwa ajili ya kuhakikisha wale Maafisa Elimu wanaweza kufuatilia ubora wa elimu kila mahala. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sote tumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya zoezi hilo ambalo ameendela nalo la kuhakikisha anatoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Seif Salim Seif ambaye anatoka Zanzibar, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Katibu mtakumbuka jana hoja ambayo ilikuwa imeahirishwa wakati tukijadili taarifa ya CAG hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro, iliwasilishwa jana hapa na nikaipa Serikali muda wa kwenda kutafakari lile andiko alilokuwa amelileta Mheshimiwa Mbunge, sasa nataka kumaliza hoja hiyo.

Sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge nilishampa nafasi jana, halafu nitasema baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi.*(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

## MAELEZO YA SERIKALI KUHUSIANA NA HOJA BINAFSI YA MHE. EMMANUEL L. SHANGAI, MBUNGE WA JIMBO LA NGORONGORO KUHUSU MIFUGO ILIYOKAMATWA NDANI YA HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo yako naomba kutoa Maelezo ya Serikali kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kuhusu mifugo iliyokamatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni Maelezo ya Serikali, kuhusu hoja zilizotokana na maelezo binafsi ya Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro, aliyowasilisha Bungeni, Tarehe 09 Novemba, 2023, kwa kuzungumza, Vilevile aliwasilisha kwa maandishi kwao na uliweza kunipatia ili tuweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la hoja hii linatoka na maombi ya Jinai Namba 10 ya mwaka 2023, ambayo yaliwasilishwa na Jamhuri katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma, ambayo Yalifafanua kama *Ex-Parte Criminal Application,* Namba 10 ya mwaka 2023, kwa lengo la kuiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma kutaifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara ng'ombe 806, kondoo 420 na mbuzi 100, waliokuwa wamekamatwa, tarehe 26 Oktoba, 2023 ndani ya eneo la Hifadhi ya Taifa Serengeti, kwa kuwa wamiliki wa mifugo hiyo hawakujitokeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma, kupokea maombi ya upande wa Jamhuri na kusikilizwa upande umoja au *ex-parte hearing*, mnamo tarehe 31 Oktoba, 2023 Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma iliamuru mifugo hiyo itaifishwe na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara. Baada ya amri hiyo ya Mahakama mifugo hiyo iliuzwa katika mnada wa hadhara, kama ambayo nilieleza jana na mnada ulifanyika Tarehe 1 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kupitia maelezo ya Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, aliyowasilisha Bungeni, tarehe 9 Novemba, 2023, ambapo tulisikia hoja mbalimbali alizowasilisha, ulitoa maelezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, iweze kuwasilisha maelezo kuhusiana na hoja ambazo Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai aliweza kuzitoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo tuliyoyapata kutoka kwa Maafisa wetu hifadhini, Wizara ya Maliasili na Utalii inaona ili kuthibitisha ukweli na usahihi wa jambo hili, upo ulazima wa kujiridhisha zaidi kwa kwenda uwandani kufanya uchunguzi wa kina ili kuweza kuchukua hatua stahiki dhidi ya yeyote atayebainika na kuthibitika kufanya uzembe, hila au maksudi juu ya suala hilo kuweza kuthibitishwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa sasa kuna Shauri la Marejeo, Namba 8 la mwaka 2023, au *Criminal Revision* Namba 08 ya Mwaka 2023, ambayo ilifunguliwa Mahakama Kuu Musoma na shauri hilo limesikilizwa Tarehe 08 Novemba, 2023, linatarajiwa kutolewa maamuzi leo hii Saa Sita Mchana katika Mahakama Kuu Musoma.

Mheshimiwa Spika, katika kesi hii ya Marejeo Namba 08 ya Mwaka 2023, kuna waombaji watatu, yupo Ndugu Oloomu Kulsas, Ndugu Sinjore Maitika pamoja na Ndugu Ndagusa Korosi, ambao wanadai kuwa ndiyo wamiliki wa mifugo hiyo iliyotokana na ile kesi Namba 10 ya mwaka 2023 na wamewasilisha katika Mahakama Kuu shauri hilo Namba 08 la mwaka 2023 ili kuweza kuiomba Mahakama Kuu Musoma, kuweza kufanya marejeo ya uamuzi wake wa tarehe 31 Oktoba, 2023 wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha kama nilivyoeleza, kwamba lengo letu lilikuwa ni kuweza kwenda uwandani lakini tunashindwa kwa sasa mpaka hapo tutakapopata hukumu ambayo inatoka leo hii Saa Sita ili kuweza kuendelea na taratibu zingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumesikia ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kwenye hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai alieleza hapa Bungeni kwamba kuna wananchi ambao mifugo yao imekamatwa, kwa mazingira ambayo nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameahidi hapa watachukua hatua za ziada pamoja na kuwa na kesi mahakamani. Kwa maana ipi?

Maelezo aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Mbunge yaliashiria kwamba mifugo ile baada ya kukamatwa wale wenye mifugo walienda kuifuatilia. Katika kule kuifuatilia, ukitazama mwenendo wa kesi unaashiria wenye mifugo hawajulikani. Sasa wakati huo huo Mheshimiwa Mbunge alieleza zile tarehe na akatoa taarifa za ziada kwamba walichukua hatua ya kufuatilia hizi kesi mpaka wakajua kwamba zimeenda Musoma na walipenda huko wakakuta hukumu imetoka na wao wakaenda Mahakamani kwa ajili ya kuiomba Mahakama itoe zuio la ule mnada, lakini mnada ulifanyika siku hiyo hiyo.

Kwa hiyo, mazingira yale kidogo yanatupa huo wasiwasi. Kwa maana ya sisi kama Bunge, hatuwezi kujadili hapa uamuzi wa Mahakama, kwa sababu ikiamuliwa kule, kama hukuridhika unapaswa kukata rufaa. Sisi hatuwezi kujadili kwa upande huo. Upande ambao tunaweza kujadili ni hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, wananchi wake kwa namna moja ama nyingine kama hawajatendewa haki, siyo na Mahakama; na upande wa wale wahifadhi. Hiyo ndiyo sehemu ambayo sisi kama Bunge tunaweza kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu nilishamsikiliza yeye hoja yake na aliileta pia kwa maandishi na jana nikawapa Serikali nafasi, na sasa wametoa ufafanuzi wao, katika huu ufafanuzi walioutoa Serikali, Waheshimiwa Wabunge tukubaliane nao kwa maana ya kwamba Serikali imeahidi. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri umesema mnasubiri leo hukumu itoke, hivyo viwili havina uhusiano. Kwa sababu mahakama itaamua kwa kutizama je, sheria ilifuatwa?

Kwa huu upande mwingine wa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, bado unahitaji Serikali iende huko kuangalia mazingira

ya namna jambo lilivyojitokeza, lakini pia ili Serikali iweze kuona namna bora ya kushughulika na hii mifugo inayokamatwa hifadhini, ama wakati mwingine kunapokuwa na huo mkanganyiko wa taarifa kwamba mifugo haikuwa hifadhini lakini imefuatwa kule ilipokuwa, pengine ilikuwa inakaribia ama watu wakaona itafika tu hii, kwa hiyo, ngoja tuifikishe kabisa. Mazingira kama hayo Serikali mkienda kutazama mtapata majibu ya hoja kama hizi ambazo Wabunge huwa wanazileta hapa ndani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ole-Shangai kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, watakapokuja kule, basi utoe ushirikiano ili Serikali ipate maelezo mazuri kutoka kwa wale wanaohusika ili nao wafanye uchunguzi kwa sehemu yao. Naamini kesi hii itatusaidia kuboresha huko mbele mahusiano kati ya Serikali na wafugaji wa nchi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nilimwona Mheshimiwa Hussein Amar ameomba Mwongozo, halafu tutaendelea na ratiba yetu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuomba mwongozo kwa Kanuni ya 76. Kwanza nitoe maelezo, halafu niombe mwongozo.

Mheshimiwa Spika, leo nina mwaka wa 13 kwenye jengo hili, sijawahi kubishana na Kiti hata siku moja. Kwa hiyo, naomba unisamehe kwa mabishano ambayo yalitokea kwenye kipindi cha swali langu Na. 151.

Mheshimiwa Spika, imefikia kubishana kidogo na kutoridhika na yale majibu kutokana na majibu ya Serikali. Majibu haya yameleta mkanganyiko kwa sababu, vikao vinavyofanyika kwenye wilaya zetu, mikoa yetu kuna wawakilishi walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tunapokaa kuyajadili pale mbele ya kiongozi aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais, ni kikao kizito.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, najaribu kuangalia hawa watendaji wetu wa Serikali walioko kule wanapokuwa wanatoa majibu ambayo hayana uhakika, basi wanatuchonganisha sisi pamoja na wapiga kura wetu. Mfano, swali hili la upembuzi yakinifu nilijibiwa kwenye Kikao Kikuu cha Ushauri cha Mkoa na Mwenyekiti alikuwa na Mkuu wa Mkoa. Mwaka 2022 niliuliza swali na Meneja wa *TANROADS* akanijibu kwamba tayari kuna fedha ambazo zimeshatolewa. Tulikuwa tumetengewa shilingi milioni 300 lakini hivi sasa tumepokea shilingi milioni 150 na kazi ya upembuzi imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitoka pale na kwenda kuwaambia wapigakura wangu, kwenye mikutano niliyozunguka, nikawaambia Serikali tayari imeshatoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara yenu. Wananchi wakashangilia. Leo hii linatoka jibu kama hili, wananiweka kwenye hali gani mimi na wananchi na wananchi na Serikali yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watendaji wote walioko huko kwa wawakilishi wote wa nchi nzima wajitahidi kutoa majibu ambayo ni sahihi ili kuepuka kutuchonganisha na wananchi. Leo hii wananchi wa Nyang'hwale wamekuwa ni watazamaji kwenye runinga na kusikia miradi mbalimbali ya barabara za lami zikijengwa maeneo mbalimbali. Sisi leo hii tumeahidiwa barabara hiyo tangu mwaka 2010. Kiongozi mkuu wa Awamu ya Nne aliahidi, kiongozi mkuu wa Awamu ya Tano aliahidi, Waziri Mkuu Pinda aliahidi, Mheshimiwa Majaliwa aliahidi, Kinana na viongozi wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, tabia hii Serikali inaichukulia hatua gani kwa watendaji wa kule chini kwa kutoa majibu ambayo siyo sahihi?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo huo utakuwa wa mwisho. Tuna ratiba ndefu kidogo leo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba mwongozo. Bila kuathiri maamuzi uliyoyatoa, wala bila kuingilia uhuru wa Mahakama uliopo kwa mujibu wa sheria, lakini nataka niombe mwongozo wako, baada ya kupata Taarifa ndani ya Bunge lako tukufu kwamba ng'ombe 806 pamoja na kondoo wapatao 420 na mbuzi 100 wameuzwa kwa bei ya shilingi isiyozidi milioni 100; kwa wastani wa shilingi 124,000 bila mbuzi kuweka pembeni. Kwa hiyo, kila ng'ombe ameuzwa kwa bei ya kama shilingi 120,000 jambo ambalo haliwezekani. Hata mbuzi aliyeacha kunyonya jana ndiye anauzwa bei hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka niulize, kwa kufanya uchunguzi na kwa kujua kwamba Mahakama imetimiza wajibu wake wa kutoa *ruling* kuruhusu dalali akauze, lakini dalali asubuhi anafahamika, amekwenda na watu wa kuwauzia...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, ukiomba Mwongozo, unataka kujua jambo lipi linaruhusiwa ama haliruhusiwi? Kwa hiyo, jielekeze huko. Naona unaleta taarifa ambazo siyo sehemu ya Taarifa zetu Rasmi za Bunge kwa asubuhi hii.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilikuwa naomba Mwongozo kwamba kwa hali hiyo iliyojitokeza kwa mujibu wa taarifa ya jana iliyohamia leo, uchunguzi ukifanyika dhidi ya bei ambayo ng'ombe wameuzwa ili kuhakikisha pia kwamba Serikali inatendewa haki na baadaye mali ile ikija kununuliwa tofauti iweze kulipwa kwa thamani halisi ya mifugo.

Je, uchunguzi ukifanyika na Serikali au na chombo chochote kitakachoundwa, itakuwa ni kuingilia uhuru wa Mahakama katika jambo hili?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa kwanza umeombwa na Mheshimiwa Hussein Amar kuhusu swali lake namba 151 ambalo lilitolewa majibu na Serikali na akaeleza

kutoridhika kwake na majibu hayo, halafu mimi nikamwuliza maswali.

Mheshimiwa Hussein, kwanza usijisikie vibaya kwa sababu mimi ndiye niliyekuuliza, kwa hiyo hakuna hoja kwamba umeleta mabishano. Hakukuwa na mabishano, nilitaka kuelewa hoja yako kwa sababu kanuni zetu zinataka swali lijibiwe kikamilifu. Kwa hiyo, Mbunge akisema hajaridhika, nataka nijue halijajibiwa kikamilifu ama hajaridhika kwa namna gani ili niweze kuzisimamia vizuri kanuni zetu. *(Makofi)*

Kwa maelezo uliyoyatoa hapa ukasema Serikali itawachukulia hatua gani wale kwa taarifa walizozitoa; kwa namna nilivyolitazama jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri ambalo amelisoma hapa na hoja ambayo Mheshimiwa Hussein umeitoa, hili jibu uzuri wake halina maneno mengi, limeeleza tu tarehe kama ambavyo swali liliuliza ni lini upembuzi yakinifu utakamilika? Serikali imeeleza lini. Imetaja hapa tarehe kwamba Februari, 2024 wanatarajia kukamilisha huu mchakato wa kumtafuta huyo mhandisi mshauri ili afanye huo upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mbunge, wewe umeeleza kwamba kule ulipokuwa kwenye kikao, walisema kwamba fedha zimeshaletwa shilingi milioni 150, na hili jibu halibishi kwamba pesa ziliIetwa. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba fedha ziliIetwa, lakini ule mchakato pengine ndiyo hoja yako kwamba imechukuwa muda mrefu. Kwa sababu hili jibu halipingani na maelezo unayoyatoa kwamba pesa zilipelekwa ama pesa ziliIetwa kwenye jimbo lako.

Kwa hiyo jibu hili lililotoka hapa lipo sahihi, lakini kwa maana ya ule ucheleweshaji sasa ambapo ndipo hoja yako ilipo, pengine Mheshimiwa Naibu Waziri angekuwa ameulizwa kuhusu uchelewaji pengine angejieleza tofauti. Isipokuwa kwa maana ya swali hii lilivyoulizwa na majibu yaliyotolewa hapa Serikali ipo sahihi kwenye hoja hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo limeombewa mwongozo, ameomba mwongozo Ole-Sendeka kupitia Kanuni yetu ya 76. Kanuni ile inataka Mbunge ajielekeze kuuliza jambo lililotokea hapa ndani kama linaruhusiwa ama

haliruhusiwi lakini hata hivyo hoja aliyoieleza hapa nikitaka mimi kuijibu hapa na tumeambiwa kesi ipo Mahakamani, itakapofika kule watapewa fursa hawa ambao wamepoteza hiyo mifugo yao kujieleza kwamba mifugo haiuzwi bei hii. Kwa hiyo, ni kesi ya madai. Kesi za madai zinaruhusiwa kabisa.

Kwa hiyo, kwa huu utaratibu uliokwenda, wao watafuata pia utaratibu mwingine, lakini nisingependa kulipeleka Bunge kwenye mazingira ambayo litaanza kujadili bei ya mifugo ni kiasi gani na mambo kama hayo. Kesi hiyo ikishaamuliwa kwamba iliuzwa isivyo sawa sawa, utaratibu wa kawaida utachukuliwa. Kesi ikiamuliwa kwamba utaratibu ulifuatwa, bado ile hoja ya Bunge kwamba Serikali iende ikalitazame hilo jambo ipo pale pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada mitano imesomwa kwa mara ya kwanza na kama ilivyo ada, Miswada hii itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika kama mlivyosikia, ni sheria za aina mbalimbali.

Kwa hiyo, zipo sheria ambazo zitaelekea kwenye Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria na pia ipo sheria hapa itakayoelekea upande wa Kamati yetu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na naona hapa kuna sheria nyingine pengine itaelekea TAMISEMI.

Kwa hiyo, imeshasomwa hii Miswada kwa Mara ya Kwanza na sasa nitaielekeza kwenye Kamati zinazohusika muda utakapofika. Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Mipango.

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudia Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, lakini majina tunayo mengi sana hapa mbele na kwa hiyo, itakuwa ngumu kidogo kila Mbunge kuchangia dakika kumi. Kwa hiyo, inabidi tukubaliane kupunguza muda ili Wabunge wote walioomba nafasi ya kuchangia wapate fursa hiyo. Kwa muda tulionao na majina tuliyonayo hapa mbele, kila Mbunge atachangia kwa dakika saba.

Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ziara yake ya Mkoa wa Singida hususan Singida Mjini, tulimpa heshima ya kuwa Mama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kaka zangu; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa kazi ambayo wanaifanya, ni kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita sana kwenye sekta ya kilimo, lakini niruhusu nifanye rejea ndogo ya nchi ya Korea ya Kusini. Korea Kusini Mwaka 1960 tulikuwa wote sawa kwenye suala la maendeleo, lakini kupitia Rais wao Park Geun Hye aliamua kwa dhati kuweka mpango wa kuwekeza kwenye utafiti na maendeleo *(research and development)*. Utafiti na maendeleo ndiyo uliomwezesha kuwa na sera ya *importation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kawa kifupi sana, kwa sababu nimeamua eneo hili la kilimo wenzetu wa Korea Kusini walikuwa na uhaba wa *natural resources.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana kwa sababu nimeamua eneo hili la kilimo, wenzetu wa Korea Kusini, walikuwa na uhaba wa *natural resources*. Lakini nizungumzie eneo dogo tu la ardhi ambayo aliitumia kwenye kilimo, ni asilimia 30, asilimia 30 hii waliyoitumia kwenye kilimo ilikuwa ni *substance* ya *agriculture* kwa maana ya kilimo cha chakula. Kiliwawezesha wao kuchangia kwenye pato la Taifa *(GDP)* asilimia 12 lakini iliwasaidia kwenda kwenye *agrarian economy*. Kwa maana ya kilimo biashara na kiliweza kuchangia asilimia 30 mpaka 40 kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nafanya rejea hii? Nafanya rejea hii kwenye maeneo mawili. La kwanza, mpango wetu unatakiwa kujikita kwenye utafiti na maendeleo. Hili ndiyo eneo ambalo nilitarajia tujikite zaidi, tuwekeze zaidi hapa ili tuweze kukamilisha malengo mengine yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili hapa, wenzetu wakati kasi ya uchumi wao inakua na kasi ya umasikini inapungua. Sasa nirejee kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, alisema kasi ya uchumi inakua lakini kasi ya umasikini inaendelea kubaki palepale. Maana yake haviendani, uchumi unakua lakini umasikini ume-*stack*. Sasa wenzetu uchumi ulikuwa unakua lakini na umasikini pia unaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limefanya niende mbali kidogo, kwa nini, sisi tunabaki kwenye umasikini wakati uchumi unakua. Inawezekana kabisa, mimi nitajielekeza sana kwenye mazao, kwenye mazao huku, watu wanauza mazao ghafi. Kwa sababu hatujawekeza, hatujajielekeza kwenye *processing industry* ili kuwafanya hawa watu mazao yao yawe na thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa kilimo, hasa kwenye zao la alizeti. Kwa mara ya kwanza Tanzania tumeweza kuzalisha alizeti tani 1,140,000 haijawahi kutokea, naipongeza sana Wizara ya Kilimo. Kutoka tani 400,000 hadi 1,140,000, hili ni jambo kubwa sana ambalo Serikali sasa ina kila sababu ya kuwekeza hapo, lakini kuna changamoto mbili zinazojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza, sasa hivi soko la alizeti limeshuka. Gunia sasa hivi ni 65,000 na kadri siku zinavyokwenda soko linashuka. Wananchi hawa ambao walihamasishwa, wakapewa mbegu bure na wakapewa ruzuku. Hawawezi kuwa na hamasa hiyo hiyo mwaka huu, wakaweza kuzalisha tena alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali, naiomba Wizara ya Kilimo sasa waamue kwa dhati kwenda kununua mbegu hii kwa wakulima ili kuwapa unafuu waweze kuzalisha zaidi. Kwa sababu nchi yetu leo inahitaji mafuta kama tani 600,000. Tumeweza kuzalisha tani 1,140,000, inaweza kwenda kwenye mafuta tani 400,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali kwenye hiyo, lakini pia iwekeze kwenye viwanda vidogo vidogo kwa wakulima, ama kwa makundi ama kwa mtu mmoja mmoja. Waziri ameeleza vizuri hapa, kwamba sasa wanajielekeza kwenye *rural social economic development*. Kama tunaenda kwenye suala la maendeleo vijijini, kwenye uchumi wa maendeleo vijijini, hapa tunayo changamoto kubwa. Pamoja na sekta zingine alizozitaja, moja wapo ni sekta ya kilimo. Kwamba, wataendelea kutoa mbegu bora, wataendelea kutoa ruzuku, lakini miradi ya umwagiliaji itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwongezee tu kwamba, tunahitaji pia ambapo tayari Wizara ya Kilimo wamefanya vipimo vya afya ya udongo. Ongeza pale vipimo vya afya ya udongo, wenzetu wameshafanya hii kazi, sasa tuwape hiyo *support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ninaiona, tunatekelezaje haya wakati msimamizi mkuu ambaye ndiyo mtaalam kwenye hii *Local Government,* kwenye *rural area* ni Afisa Ugani. Afisa Ugani bosi wake ni Mkurugenzi. Mkurugenzi akiamka, jukumu lake la kwanza ni kukusanya mapato. Tumewapa maafisa ugani kuweza kuwa na pikipiki kila mmoja. Pikipiki sasa zinatumika katika kukusanya mapato. Maana yake huu mpango tunaouweka, huyu afisa ugani yuko huku TAMISEMI anafuata malengo mengine, mpango ambao umewekwa na *Local Government* lakini sisi huku mipango yetu tunasema itatekelezeka. Haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri hapa, Mheshimiwa Waziri kaka yangu Profesa Mkumbo alikuwa Katibu Mkuu hapa wakati pia na sisi tunachangia tulishauri kwamba, Idara ya Maji kutoka Halmashauri iende kwenye mamlaka ya maji na jambo hili likafanyika. Tukashauri suala la *TARURA* na leo inajitegemea. Inashindikanaje maafisa ugani kuwatoa huku waliko kwa Mkurugenzi ama kwenye *Local Government,* tukawapeleka kwenye Tume ya Umwagiliaji. Hili linaweza kusaidia mpango ambao mmeuweka na kuboresha kilimo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kwenye Tanzania *Development Vision* ya 2050. Hapa mwelekeo wa Tanzania 2050,

nataka kujikita kwa watu waliowengi wanapojishughulisha. Asilimia 80 ya Watanzania wapo kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji. Natamani dira hii ijikite hapo. Nataka nitoe mfano mdogo wa wenzetu wa kilimo, wanaandaa leo Tanzania *Agricultural Transformation Master Plan.* Kama unaandaa mpango kabambe wa mageuzi kwenye kilimo nchini, tunatarajia kuona ule mwelekeo wa Tanzania ya 2050. Kuna kuwa na *chapter* ambayo inaelezea mpango huu kabambe ili kuwasaidia wenzetu na kuwasaidia Watanzania kwa sababu sehemu kubwa ndiyo wamejiajiri hapo… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mezani kwetu. Kwanza, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwa kuja na hotuba nzuri ambazo zimetupa mwelekeo wa kule tuendako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeza Mheshimiwa Rais kwa miongozo ambayo ameitoa kwa Wizara hizi na kuepelekea kuletwa kwa hotuba hiyo ambayo tunajadili sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo mawili. Nianze na Sekta ya Gesi Asilia. Naipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri ambayo inaifanya, lakini nina ushauri katika mambo matatu. Kwanza ni kuhusu mradi wa *LNG*, nimesoma kwenye mapendekezo ya mpango, kuna mikataba imeshaanza kusainiwa. Ni jambo zuri lakini wamekwenda mbali, kwamba kuna kampuni ya *TPDC Likong'o LNG Company Limited* imeanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, shughuli hizi za *LNG* zifanyike kwenye eneo husika. Likong'o ni mtaa au ni kijiji katika Manispaa ya Lindi. Siyo busara sasa shughuli hizi zikaendelea kufanyika Dar es Salaam na Arusha, wakati eneo la mradi lipo. Kwa hiyo, naomba sasa Shughuli za *LNG* zihamie katika eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni kuhusu Ujenzi wa Vituo vya *CNG*. Wote ni mashahidi sasa bei za mafuta duniani hazitabiriki. Sasa hivi kuna mpango mkubwa au kuna uhamasishaji wa watu tutumie gesi asilia katika vyombo vya usafiri lakini vituo hivi ni vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali sasa, kwanza naipongeza *TPDC* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwenye suala hili na *EWURA*. Sasa naomba Serikali itoe vivutio maalum kwa watu ambao wanataka kujenga vituo hivi ili viongezeke. Kwa sababu kwa sasa nafikiri tunavyo vinne tu. Kuna makampuni zaidi ya 30 wameomba, tuwe na *special incentive* ili hata kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuwe na vituo vya *CNG*, kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kuwe na Vituo vya *CNG* na maeneo mengine. Tutoe punguzo maalum, tutoe vivutio ili sasa wawekezaji wajikite katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu ni usambazaji wa gesi viwandani na majumbani. Naipongeza *TPDC* kwa kazi ambayo wanaifanya vizuri, lakini *TPDC* hawapewi fungu la kutosha. Naomba mpango ujielekeze kwamba utatoa fedha za kutosha ili usambazaji huu sasa uende kwenye mikoa yote. Isiwe Mtwara, Lindi na Dar es Salaam tu, gesi asilia sasa iende kwenye mikoa yote. Niipongeze Wizara ya Nishati, imesaini mkataba jana wa kupeleka hii gesi kwenda Uganda, sasa ielekee Uganda lakini na mikoa ambayo bomba hili litapita inufaike na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu suala la elimu. Naipongeza Serikali kwamba imeidhinisha matumizi ya Sera Mpya ya Elimu ya 2014. Sera hii ya elimu ya 2014, kama mtakumbuka ilizinduliwa huko nyuma na imekaa

miaka nane kabla ya utekelezaji wake kwa sababu ya kukosa *funding*. Naomba sasa Serikali ijielekeze katika ugharamiaji wa hii sera mpya ya elimu ambayo inakuja na mambo mengi sana ambayo yatabadilisha uendeshaji na usimamizi wa elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwakani tunaanza kutekeleza mtaala mpya kwa wanafunzi wa darasa la tatu. Kwa maana hiyo, Mtihani wa Darasa Saba mwaka 2027 hautakuwepo. Kutakuwa na kitu kinaitwa *National Assessment,* lakini kwa sasa hivi kwa takwimu zilizopo kila inapofanika mtihani, wanafunzi takribani asilimia 25 hawaendelei na kidato cha kwanza. Tutakapofanya *National Assessment* ina maana wanafunzi wote wataingia kidato cha kwanza kwa hiyo, kuna mahitaji mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano wa watahiniwa mwaka huu, tulikuwa na watahiniwa 1,397,370. Sasa asilimia 25 ambao kwa matokeo ya kawaida ya mtihani ni kama watoto 350,000 hivi hawataingia kidato cha kwanza. Tutakapoanza utekelezaji wa sera mpya, hawa 350,000 wataingia kidato cha kwanza. Tutahitaji madarasa mapya, walimu wapya na tutahitaji matundu ya vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wanafunzi hao 350,000 tunahitaji madarasa ya ziada 8,733, siyo mapya, ni ya ziada ukiacha haya yaliyopo sasa hivi. Tutahitaji matundu ya vyoo 17,497. Kwa hiyo, lazima mpango wetu ujikite katika *education financing,* tutapata wapi fedha za kugharamia huu mfumo mpya wa elimu, elimu isigharamiwe kama kawaida. Tukifanya kama tunavyotenga bajeti ya kawaida hatutaweza kujenga shule mpya za ufundi ambazo zinatakiwa. Kwa sababu kwa maelekezo ya mtaala wetu mpya, tutakuwa na mikondo miwili; ule mkondo wa kawaida wa taaluma na mkondo wa amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkondo wa taaluma na mkondo amali ina maana kwamba sasa huku kwenye amali ni kitu kipya. Tutahitaji walimu wapya wa michezo, wa ufundi na walimu wapya wa sanaa. Hao walimu wanahitaji ajira, yaani itatakiwa

ajira mpya ili waingie katika mfumo huu. Sasa pasipokuwa na fedha za kutosha hatutaweza kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wanahitaji maabara ambazo zimesheheni, siyo maabara ambazo kuna *Bunsen burner* na *test tube*. Inabidi tuwe na maabara ambazo mwanafunzi akiingia ajue kweli ameingia maabara. Kwa hiyo, hilo linahitaji uwekezaji, siyo hivyo tu, tunahitaji *in service training* kwa walimu. Hao Walimu sasa tunawaambia kwamba mtoto akiingia darasa la kwanza anafika *form four*. Hao waliopo kazini lazima tuwe na mafunzo kazini, tuwawezeshe kwenye mbinu mpya, tuwape maarifa mapya na tuwape ujuzi mpya. Tukigharamia kama tunavyofanya sasa hivi hatutaweza kutekeleza mtaala huo mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Jambo hili limekuwa likisumbua Taifa letu kwa muda mrefu sana, kama tunakumbuka huko nyuma Wizara za Kisekta zilikuwa zinapanga mipango yao yenyewe bila kuratibu, lakini leo hii Mheshimiwa Rais, ametuletea Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu kwamba Wizara zote za Kisekta sasa zinakwenda kuratibiwa na mipango itakoyoanzishwa na Wizara ya Mipango na Uwekezaji, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kupata uteuzi huo. Niombe sasa kama kuna mipango ambayo tayari hapo nyuma ilikuwa imejikita kwenye sekta na haipo kwenye mipango kwa maana ya Wizara ya Mpango na Uwekezaji. Nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Mipango, ashirikiane na Wizara hizo za Kisekta, mathalani Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini leo hii wamekuja na mpango wanaita *vision 2030*. Sasa ukijiuliza *vision* tuliyonayo leo hii ni 2025 - 2030 imetoka wapi? Sasa wanahitaji kusaidiwa kwa sababu wanakimbia sana, wao wanakimbia sana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Madini, *all starts well ends well my brother*, umeanza vizuri. Sasa naona kasi yako ni kubwa, nikuombe ushirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, hiyo *vision 2030* uje uilete kwenye Wizara ya Mipango ili sasa muwe na *common understanding* katika safari yako hiyo unaweza kufanikiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, naomba tufanye marejeo ya huu mradi wa *BBT* tufanye mapitio. Hofu yangu kwamba leo hii kijana aliyemaliza Chuo Kikuu, umempa shamba la hekari tano, ameshaomba ajira benki, akafanya *interview,* benki wamesema tunakuajiri akabaki na hizo heka tano, aache *white collar job*. Nani atakaa juani? Kwa hiyo, nadhani tutafute namna bora juu ya hili jambo. Mimi nilikuwa naona nia ni njema, lakini ni namna gani tutakwenda kutekeleza mkakati wetu ili vijana wape ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye eneo hili la Kilimo. Ili kilimo kiwe kilimo biashara lazima tuwe na ardhi inayofaa kwa kilimo. Lazima tuwe na mitaji, umwagiliaji na pembejeo. Taarifa na maoni ya Kamati Ukurasa wa 25, narejea Maoni ya Kamati, wanasema; "kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga bajeti kupitia taasisi za kifedha shilingi trilioni 2.6, lakini fedha hizi asilimia tatu tu ndiyo zilizotumika kwenye uzalishaji wa Sekta ya Kilimo. Asilimia 93 zote zilikwenda kwenye mauzo ya bidhaa za Kilimo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lipo wapi? Naomba niseme tatizo, kwa nini kwenye uzalishaji zimekwenda asilimia saba na siyo asilimia nyingi? Kwa sababu wananchi wakitanzania, wakulima wakitanzania hawakopesheki. Leo hii ukiuliza wakulima wetu wengi wale wadogo, wakati na wakubwa; wengi wao hawana hati miliki. Miongoni mwa vitu ambavyo vinafanya mkulima akopesheke ni hati miliki, kama *collateral.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo maana *rate* ndogo ya waliokopa benki na hiyo nadhani ni muhimu sasa Wizara ya Ardhi, unasikia sababu alizosema Mheshimwa Waziri wa Mipango; kuratibu Wizara ya Ardhi, Kilimo na Biashara. Biashara ishughulike na masoko, Ardhi ishughulike na masuala ya upatikanaji wa wa ardhi inayofaa kwa kilimo na kuwapatia wananchi hati miliki. Pia, Wizara ya Kilimo yenyewe ijikite kwenye umwagiliaji na masuala ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili likifanyika naamini tutakwenda kukifanya kilimo sasa kiende kuwa kilimo biashara. Nakumbuka hapa miaka 20 iliyopita, kilimo ilikuwa ndiyo sekta inayochangia asilimia 20 kwa maana ya mauzo ya nje, lakini leo hii tunaona madini ndiyo inakwenda zaidi. Kwa nini kilimo kimesimama. Kuna kazi ya kufanya kwenye Sekta ya Kilimo ili tuone sasa tunaweza kuuza mazao ya kilimo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalilojielekeza ni eneo la halmashauri zetu nchini. Hivi kuna dhambi gani halmashauri zisi-*graduate*. Kwa nini halmashauri ziendelee kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu? Nchi zote duniani, majiji na halmashauri zinajitegemea, kwanini Tanzania ni wapi tunakwama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila halmashauri kuna fursa za uwekezaji, mathalani mimi nitoe mfano pale Mlimba. Sisi tuna shamba la miti hekari 1,500, tunaamini miaka 10 ijayo tutaanza kuvuna, tumeona fursa ni kupanda miti. Pia, tuna shamba la mikorosho hekari 150, baada ya miaka kadhaa tutaanza kuvuna korosho tutauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kupitia Wizara ya Mipango, ni muhimu sasa tufikiri tofauti, halmashauri zote zianze kuwekeza. Zianze kufukiria kujitegemea, ku-*graduate* ili kupunguza mzigo kwa Serikali Kuu. Sisi Mlimba tunajenga vituo vya afya vitatu kwa mapato ya ndan, Ilala, Dar es Salaam na Arusha hawawezi, kuna shida gani? Sisi Mlimba tunajenga vituo vitatu vya afya kwa mapato ya ndani na viwili tumefungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu mifano hii ikasomwa hapa na ninasema kitu ambacho kinafanyika. Kwa hiyo, hakuna sababu za kufanya halmashauri isi-*graduate* na zijitegemee kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuendelea kuchangia Wizara hii ya Mipango. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuandaa au kuunda Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. Nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, katika manispaa yangu Januari mpaka Desemba nilikuwa siwezi kujenga hata kituo kimoja au kuchimba choo cha matundu manne kwa manispaa, tumeletewa Mkurugenzi, kwa kweli huyu kijana lazima nizungumze hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeletewa kijana huyu ndani ya wiki mbili amekusanya zaidi ya milioni 160, ndani ya wiki mbili. Kwa hiyo, nampa pongezi Mkurugenzi Nyange na aendelee sasa kututengenezea Jimbo letu la Mtwara na Manispaa yetu ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mipango lazima tuzungumzie kilimo. Nataka nijikite kwenye eneo hili la kilimo hasa kwanza nimpongeze Waziri wetu Bashe, kwa kazi kubwa anayoifanya. Wenzetu China waliamua kufanya mageuzi ya makusudi hasa kwenye maeneo ya vijijini, Serikali iliamua kuandaa mpango wa kuwawezesha vijana ili kwenda kutengeneza mfumo wa kilimo na kujipatia chakula cha kutosha na chakula kingine cha kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwamba sisi kama watu wa Mtwara, tuna maeneo makubwa sana ambayo ni mapori na kwa kuwa Mheshimiwa Rais, amefika mahali akaamua kwenye

Sekta hii ya Kilimo kutoa fedha nyingi sana. Niombe kwenye mipango hii tuelekeze sasa tuachane na vijana kwenda kucheza *pool table,* twende tuwapeleke sasa kwenye maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza mipango, tunazungumza na Pato la Taifa. Nimekuwa mara nyingi nikiishauri Serikali, kutoka Mtwara kwenda Mji wa jirani wa *Mozambique*, tunachukua takribani kilometa kama 60 na hilo nalizungumza Waziri wa Mipango, alisikilize vizuri sana nadhani inawezekana lina tija kwake zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa nane ya Mozambique wanatumia Bandari ya Beira. Kutoka kwenye mkoa wa mwisho kwenda Beira zaidi ya kilometa 2,000 au 1,800. Kutoka kwenye Mkoa wa mwisho kuja kwenye Bandari ya Mtwara wanatumia kilometa 770. Ninachotaka kukizungumza tufungue mpaka ule ili tufanye biashara sasa kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wenzetu wa Mozambique wanashughulika na masuala ya gesi lakini wanashindwa gesi yao kwenda nayo kwa wakati, hawana njia ya kutumia kwa sababu wale wawekezaji Bandari ya Beira kuja mpaka Palma kuja mpaka Mchimbo Naplaya, kwenye maeneo ya gesi wanashindwa kutokana na *mileage*. Kwa hiyo, niombe Wizara hii iliangalie hili kwa mapana na marefu, tunakwenda kufungua nchi na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo linawezekana kama Tanzania tukaenda kuungana nalo la viwanda. Bila viwanda hatuwezi ku-*move* hata siku moja, lakini tukiangalia maeneo mengi tunazungumzia Mbeya, Pwani, Lindi na Mtwara, yako maeneo makubwa ambayo kuna rasilimali, *materials* na kila kitu. Tunashindwaje kuwaleta wawekezaji waje waweke viwanda na tunapozungumza viwanda ndani ya nchi tunazungumza ajira ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila kijana anaye-*graduate* kwenye Chuo chochote kile mawazo yake yote anakwenda kupata ajira. Katika mfumo wetu wa elimu hatuwafundishi na hatuwajengi hawa vijana watoke kwenye Vyuo waje

wajitegemee, mawazo yao yote kwamba sasa wanakwenda kutafuta elimu ni vyema tukawatengenezea vijana hawa ambao wanakwenda kumaliza elimu yao waje wafanye kazi kwenye mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo naliomba kwamba Sekta hii ya Uwekezaji twendeni tukawalete Wawekezaji wa kutujengea viwanda. Tunazungumza tuna madini, lakini leo ukienda maeneo ya Lindi na Mtwara utakuta toka miaka ya 80 yuko Mwekezaji amechukua leseni ya madini zaidi ya heka 600 au 700 na hawaonekani. Hiyo leseni kila ukigusa unaambiwa hapo kuna mwenyewe, lakini madini hayachimbwi zaidi ya miaka 30, tunazungumza mipango bila fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo naomba liangaliwe kwa sababu nazungumza nikiwa na ushahidi wa jambo hili. Rasilimali ni ya kwetu, mtu amekuja amechukua leseni na kwenye leseni ile sasa hivi amefika zaidi ya miaka 30 hajawahi kuchimba hata siku moja. Kama hajachimba hata siku moja faida yake ni nini na mipango ipi ambayo tunaiweka kwa sababu tunazungumza mipango kwenda kutafuta fedha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Mipango, hili nalo waliangalie kwa mapana na marefu kwamba wale wote waliopata leseni wana zaidi ya miaka 20 au 30 na hawajachimba, watumie sheria ambazo inawezekana wanaziweza wawaondoe hawa watu, wananchi wetu waende wakachukue hayo maeneo ili wachimbe madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sasa nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli kwenye Jimbo langu natembea kifua mbele, Rais, amefanya raha kubwa sana kunisukumia fedha kwenye Jimbo langu. Mungu ambariki sana na aendelee sasa kusogeza miradi kwenye Jimbo la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, akifuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ambayo ipo mbele yetu. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake na maelekezo yake kwa wasaidizi wake katika kutaka kulipeleka Taifa hili katika nchi ya asali na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Lameck Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Sisi ni mashuhuda, Mpango waliouleta ni mzuri lakini mwelekeo wa bajeti ni mzuri, tunaamini kabisa ukifuatiliwa tutaweza kufanya mambo makubwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii katika mchango wangu kuishauri Serikali, niende moja kwa moja kwenye suala la kilimo. Zanzibar au Tanzania kupitia Zanzibar ni nchi ya nne duniani katika zao la karafuu, lakini Mkoa wa Morogoro umebahatika nao kuwa Mkoa ambao tunaweza kuzalisha zao la karafuu na linaweza kutuletea pesa nyingi za kigeni huko tuendako. Zanzibar inazalisha wastani wa tani 500,000 za karafuu duniani, lakini Mkoa wa Morogoro katika kipindi kifupi tu tumeweza kuzalisha tani 2,200 ambazo zimeweza kuleta uchumi kwa Wanamorogoro karibu bilioni 39 kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mkoa kama mkoa umefanya jitihada za dhati, tumekwenda mpaka Zanzibar, tumeweza kujifunza kama Halmashauri ya Morogoro Vijijini tumepeleka Madiwani na Wakulima, wameweza kufanya mambo hayo tulipofikia.

Ombi langu kwa Serikali kupitia zao hili la karafuu, naamini tunaweza tukapata uchumi mkubwa Mkoa wa Morogoro ukazalisha hadi tani 10,000, kwa sababu Mkoa wa Morogoro

kuna Halmashauri ya Morogoro Vijijini, Mvomero, Kata ya Kibati, Gairo na Nongwe, kuna uwezekano mkubwa sana wa kulima zao hili na kuleta mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi wa Mkoa chini ya Mkuu wa Mkoa wetu Mheshimiwa Adam Malima, umefanya kazi kubwa katika kuhamasisha zao hili. Sasa ombi langu ni kwamba, muda muafaka kwa Serikali Kuu kupitia Wizara ya Kilimo ichukue jambo hili ambalo linaenda kuleta uchumi mkubwa kwa Taifa hili katika kusaidia kupanga zao la karafuu, tunafikaje mbele ya hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii katika kuzungumzia suala la utalii. Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa katika *Royal Tour* kutangaza utalii, lakini utalii lazima tutakubaliana wote hapo tulipo uko mkubwa sana katika Nyanda za Kaskazini. Kupitia Mradi wa *REGROW*, ambao upo katika Uboreshaji au Uimarishaji Utalii Nyanda za Kusini ambapo kuna Mkoa wa Katavi, Morogoro na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro kupitia Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, niombe Serikali kupitia Mradi wa *REGROW*, ukaboreshe Kiwanja cha Ndege cha Matambwe, kwa sababu ndiyo lango kuu la kuingilia lakini ukaboreshe madaraja na barabara ndani ya hifadhi hiyo ili kuweza kupitika katika maeneo yote na kuweza kuongeza watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kupitia Wizara ya Ujenzi. Barabara ya Bigwa - Kisaki tayari imeshapata Mkandarasi, bado inasubiriwa kusainiwa. Twende tukasaini Barabara ya Bigwa - Kisaki twende tukasaini barabara ya Ubena - Zomozi – Ngerengere kujengwa kwa kiwango cha lami ili kurahisisha wataliii waweze kufika katika Hifadhi ya Mwalimu Nyerere na kuweza kuendelea kuleta pesa nyingi Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nizungumzie suala la umeme. Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, umefikia asilimia 84.35 hadi kufikia sasa hivi. Ombi langu kwa Serikali sisi mashuhuda tumeendelea kuona kukatika kwa umeme. Serikali ikaweke jitihada za dhati kuhakikisha kwamba Mkataba wa Ujenzi

unakamilika kwa wakati ili umeme uweze kurudi na kuweza kusaidia Taifa lisonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwa na umeme wa uhakika, maana yake tutakuwa na uhakika wa uchumi wa viwanda. Tutakuwa na uhakika wa uchumi kwa watu wetu katika viwanda vidogo vidogo, lakini katika hilo suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere, sisi wananchi wa Morogoro, wanachi wa Mkoa wa Pwani tuna sikitiko kwa Serikali yetu, hadi tunapozungumza sasa hivi *CSR* ambayo ni haki ya mikoa hiyo miwili haijapatikana hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa tumetengewa bilioni 10 Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini kuna wenzetu wengine ambao hawahusiki japokuwa kwamba mradi huu ni wa kimkakati, lakini wamepelekewa bilioni 80 ambazo naamini kabisa kwamba hatujatendewa haki. Mheshimiwa Mwigulu, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Waziri wa Nishati, watupe Wanamorogoro na Wanapwani haki yetu ya kimsingi kama vile mkataba unavyosema, ili tuweze kufikia hapo tunapokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mpango huu wa Maendeleo. Awali ya yote nimpongeze Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa kutuletea Mpango huu ambao kwa kiasi kikubwa inaonyesha namna gani ya kutekeleza na kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika watu ambao nilichangia katika Bunge lililopita mwaka jana ilikuwa ni kwamba tuwe na Tume ya Mipango. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuamua kwa dhati kabisa tuwe na Tume ya Mipango, lakini

dhana na dhima ya Tume ya Mipango ni kuwa na dira kubwa na kuangalia namna gani Taifa tunalotaka kwenda katika vipaumbele vyetu na katika kujiimarisha zaidi kiuchumi. Nataka nimshauri Waziri wa Mipango, kwamba sera zetu zijielekeze katika kutatua matatizo na kuyamaliza badala ya kuwa na sera za jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa Mkoa wa Dodoma, tunaishukuru Serikali sasa ni Makao Makuu ya Nchi, kazi tuliyonayo ni kwamba tunajenga Mji huu, lakini ukiangalia kwa sasa Dodoma haina viwanda umebaki Mji wa Kiserikali, umebaki mji ambapo mzunguko wake wa fedha sio mkubwa kwa sababu hatuna viwanda, Umebaki ni mji wa mwisho wa mwezi, ikifika mwisho wa mwezi mzunguko wa fedha unakuwa mkubwa na tarehe zinavyoisha, unaona kabisa uchumi na watu hawajachangamka. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Dodoma huoni bidhaa zinazotoka Dodoma ziende Iringa, Arusha, Kanda ya Ziwa, bado tuna shida ya viwanda. Kwa hiyo, Dodoma inahitaji sera madhubuti kwa namna gani iwe *hub*…

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya kuwa na uchumi wa kuweza kuzalisha katika ili kuhudumia mikoa mingine …

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ni wapi inatajwa taarifa?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, hapa Dodoma mnacho Kiwanda cha *Wine* au hicho sio Kiwanda? Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kutoka kwa Ustadhi, kwa kujua hili suala la *wine*, naipokea taarifa ni kweli kiwanda tunacho na kwenye hili bado tuna changamoto, lakini tunaendelea kuweka jitihada zaidi kukuza zao la zabibu. Nakushukuru sana Ndugu yangu Mheshimiwa Taletale. Nilichotaka kusema ni kwamba mji huu unahitaji uwe na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliseme hususani kwa Mkoa wa Dodoma, Waziri amesema habari ya kwamba umaskini unaenda kupungua, lakini kwa Mkoa wa Dodoma, bado kuna shida. *Nature* yetu ni kwamba Mkoa wetu una ukame, hilo wote tukubaliane, kwamba Mkoa wetu na maeneo yetu ya Kanda ya Kati, ni maeneo kame na umaskini bado ni mkubwa kwa sababu moja, wananchi wengi wanategemea kilimo, lakini jitihada za kuondoa umaskini kwenye suala zima la kilimo na kama nilivyosema namna ya kuweka viwanda, bado hatujakaa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na Sera za Kitaifa, Mipango ya Kitaifa, wenzetu kwa mfano Nchi ya Nigeria walikuwa na sera kwa ajili ya maeneo kame, mipango kwa ajili ya maeneo kame. Naishauri Serikali na namshauri Waziri wa Mipango, tuwe na sera mahsusi katika kuinua na kuleta uchumi kwenye maeneo kame ikiwemo Dodoma. Sawa tunapokea *skills* za umwagiliaji, lakini bado haitoshi, wananchi wengi wa maeneo yetu kwanza idadi ya watu inaongezeka, ardhi ya kulima inapungua ni lazima Serikali iangalie uchumi wa maeneo haya kame tunafanya nini, hili nataka niliongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu wanafunzi wanaosoma Vyuo Vikuu na Vyuo vya Juu. Kutokana na umaskini tulionao kwenye maeneo yetu hasa Kanda ya Kati, watoto wengi hawawezi kwenda kwenye vyuo wakalipiwa ada kwa sababu uwezo wa wazazi wao haukidhi. Nalisema hili kama Mbunge, changamoto ninazozipata kwa sasa, kila mtoto ameshindwa kwenda shule na wanasema Mbunge tusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kama inaweza kwa nini tusiondoe ada kwenye Vyuo Vikuu tukopeshe watoto kwa ajili ya chakula, fedha ya chakula. Serikali itoe ada kwenye Vyuo Vikuu kwa watoto wa Kitanzania ila kama ni *foreign students* hao ndiyo walipe ada. Nataka niulize Serikali inapata faida gani kulipisha watu wake kwenye ada za Chuo Kikuu? Naomba sana jambo hili tulitafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini ni mkubwa, watoto wetu hawawezi kwenda vyuo na wengi wanaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kupeleka fedha nyingi sana kama tumetangaziwa hapa sasa hivi kupata magari ya elimu, lakini pia na afya na miradi mingine inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, wajukuu zangu Wanyiramba kwa kuaminiwa kupata nafasi muhimu sana. Mheshimiwa Profesa, wenzetu ni watafiti, nchi hii haina upungufu wa maandiko na makabrasha yapo mengi na Mheshimiwa Rais, sisi Wabunge na Watanzania tunataka matokeo ya Mipango ambayo inapendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mpango umeletwa lakini pia kuna makisio ya fedha ambazo zitaenda kukusanywa katika vyanzo mbalimbali kuletea Watanzania maendeleo ili waendelee kukiamini Chama Cha Mapinduzi, kiendelee kushika dola katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye eneo la *software,* wenzangu wamezungumza maeneo mengine. Unapozungumza utakusanya fedha ya shilingi trilioni 47.4, ni vizuri pia tukakumbushana kwamba Watumishi wa Umma wana malalamiko mengi sana kuhusu kikokotoo ambacho kinawekwa 1/540 kikaondolewa kikaja 1/580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili hizi fedha zote na mipango hii hawa watumishi wa umma ndiyo wataalam wetu wataenda kusimamia, lakini wana manunguniko na malalamiko. Katika Mipango ya Serikali, ni vizuri Serikali ikaonyesha matumaini kwamba maombi yao yanaendelea kufanyiwa kazi na walikutana Mheshimiwa Rais, nakumbuka Mapolisi, Walimu katika Kanda mbalimbali akawaahidi kwamba atalifanyia kazi. Jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tukifanya ziara maeneo mbalimbali wanaomba la kwanza warudishe *formular* ya moja chini ya 1/540 lakini umri huo wa kuishi urudishwe pale ulipokuwa 15.5 badala ya 12.5 lakini wapewe fedha zao kwa mkupuo asilimia 50 ili kupunguza mawazo, msongo wa mawazo na wengine wamepoteza maisha katika eneo hili. Hilo ni muhumu sana ili kuboresha utumishi wa umma, kusimamia miradi na ukusanyaji fedha ambazo zipo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunao watumishi wa umma kwa maana ya Madiwani wetu katika Kata mbalimbali, Wenyeviti wa Vijiji pia Wenyekiti wa Serikali za Mitaa. Nimefuatilia wenzetu majirani wa Kenya hawa viongozi wanalalamika sana wamepewa posho ya shilingi 350,000 tangu mwaka 2012 mpaka leo, lakini nimeenda Kenya Machifu ambao ndiyo Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji hapa kwetu wanajitolea, Kenya wale Manaibu Chifu wale wanalipwa 540,000, Machifu yaani Wenyeviti wenyewe wanalipwa 720,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wa Tanzania posho ya mwezi wanalippwa 350,000, lakini Madiwani wa Kenya wanalipwa tena siyo posho ni mshahara 2,592,000. Hii maana yake ni nini? Miradi yote hii ya Mheshimiwa Mama Samia na bajeti ya makisio mnaleta hapa hawa viongozi kwenye mitaa, kwenye vijiji, Madiwani wataenda kusimamia na kusimamia vizuri ili kwenda kuangalia *value for money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu ambao wananung'unika, wanalalamika ni vizuri pia kupitia mpango wa Serikali na makisio 2024/2025 wakaona kwamba Serikali inaenda kuwakumbuka, kuboresha maslahi yao ili waweze kukidhi maisha katika maeneo hayo. Wanawatuma Wabunge wao hapa tuwasemee kwamba ni vizuri jambo hili likapokelewa, katika bajeti ijayo tuone *projection* na *item* ya kuonesha kwamba kuna angalau kuonesha uwezesho Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji, Waheshimiwa Madiwani ili malalamiko haya yapungue au kuondoka kabisa ili wakasimamie miradi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu. Ukisoma Azimio la Arusha ukienda kitabu cha Mwl. Nyerere cha Uongozi wetu na Hatma ya Tanzania ukaenda Tujisahihishe, historia ya Mwalimu nenda kwenye ile tunaita *MPH* ambayo ilianzia China ikaenda mpaka Singapore, wenzangu wamezungumza habari ya Korea Kusini lakini Wachina hawa na Singapore ilikuwa ni Dunia ya Tatu katika uchumi leo ni Dunia ya Kwanza katika uchumi! Walifanya maamuzi magumu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapo Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, tutapiga *mark time* sana kama hatuwezi kufanya maamuzi magumu. Kwanza tunapataje watu wetu sahihi katika nafasi? Profesa amem- *quote* huyu aliyekuwa Waziri Mkuu Singapore kupata watu sahihi wa Serikali katika maeneo sahihi. Kwamba uchukue mtu pasipo *bureaucracy* uchukue mtu kwa *merits* mwenye uwezo. Pili unafanya sera na maamuzi sahihi na tatu ni lazima tuwe na *zero tolerance* kwenye mambo ya *corruption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa stori ya maliasili hapa, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kwa kweli sisi ambao tunaotoka maeneo ya ukanda ule na Watanzania wengine lazima tukubaliane hiki kizungumkuti cha kufanya maamuzi ya kuuza ng'ombe za watu tofauti na mpango wa kupata fedha tuwawezeshe Watanzania wapate maisha bora. Lakini hawa ambao ng'ombe zao zimeuzwa wanapaswa kusomesha, hao wenzao ng'ombe zimeuzwa wanatakiwa wajenge nyumba bora, hawa ambao ng'ombe zimeuzwa wanatakiwa wapeleke watoto Vyuo Vikuu. Huu ndiyo uchimi wao na hawana namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu sijaona Mpango wa Serikali wa kupunguza migogoro kati ya wananchi na hifadhi, mpango wa kuwalipa fidia waliopo karibu na hifadhi wakatafute maeneo mengine lakini pia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waheshimiwa Wabunge wanasimama kwenye Bunge hili wanazungumza eti wangapi wameuwawa, wangapi wamepata ulemavu wa kudumu, hii haiwezi kuwa sawa, lazima Serikali iwe na mpango wa kufanya Watanzania wote wafurahie maisha kwa kupata huduma za kimaendeleo lakini na kutendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inategemea tusipokuwa na watu sahihi katika maeneo mbalimbali unaweza ukawa na mtu yuko mahali anasimamia wenzake kumbe na yeye anatakiwa asimamiwe na wewe unasubiri matokeo. Umemuweka mtu amekaa mahali anatakiwa asimamiwe wewe unafikiri anasimamia wenzake kumbe anahitaji msaada. Kwa hiyo, tuangalie *modality* ya kupata viongozi katika maeneo yetu. Mimi nilifikiri kwamba kule kwangu Serengeti, Bunda, Tarime, Mbarali tumwambie Mheshimiwa Makonda afanye ziara pale halafu apige simu kwa Waziri wa Maliasili atolee maelezo kwa wananchi pale. Hii hali haiwezi kupokelewa kule vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mnapozungumza hapa na kupanga sisi kwenye maeneo yale tupo kwenye kitimoto, tupo kwenye kiota lazima tutengeneze mazingira mazuri kauli ya Serikali, kuwasikiliza tumetoka mbali tunajua, haya mambo

Mheshimiwa Waziri lazima muingize kwenye mipango. Ifike mahali Wabunge humu tusipeane taarifa hawa watu wangapi wamekufa, tusipeane taarifa ng'ombe ngapi zimeuzwa. Tuseme tumeboresha huduma na Watanzania wanampenda Mheshimiwa Rais kazi ni nzuri na kazi iendelee mimi niwatakie kila la kheri viongozi wangu lakini ni muhimu tuweke haya katika mipango yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi fursa na mimi nitoe mchango wangu katika mapendekezo haya ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali yetu kwa mwaka unaokuja wa Serikali wa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe Mheshimiwa Rais wa Mabunge yote ya dunia hii, hongera sana tunayo imani kubwa sana na wewe na dunia imeona. Ushindi huo umeonesha kwamba Bunge hili ni Bunge bora kabisa katika Mabunge ya Dunia, kwa hiyo nakupongeza na nakutia moyo tuko pamoja na wewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambae ameona umuhimu wa hii mipango kuwa na Wizara, leo tuna Wizara ya Mipango ambayo inaongozwa na Profesa mbobezi kabisa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo damu ya Singida hiyo, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanavyosema wenzangu hapa ninyi hapo mapacha wawili mmekabidhiwa eneo nyeti sana, mmekabidhiwa uchumi wa nchi ili mtuokoe, mtuvushe

mtutoe hapa tulipo tusonge mbele kiuchumi, nchi yetu isonge kiuchumi. Ninayo imani kubwa na ninyi na ninao uhakika mtatusaidia na mtahakikisha nchi yetu inabadilika kiuchumi. Nimpopngeze pia Rais wetu tena kwa miradi mingi ambayo ametuletea kwenye maeneo yetu, katika tangazo ulilotoa la yale magari na mimi Jimbo langu tumepata gari la kubebeba wagonjwa ambalo nimekuwa nikiliimba sana hapa Bungeni mara kadhaa, leo namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu ametusikia hivyo wananchi wetu wanaenda kupata nafuu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na hii isiishie hapo, tuendelee kufanya hivyo ili kuendelea kuokoa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *agenda* yangu kubwa hapa ni sekta ya mifugo ambayo imekuwa ni agenda *hot* sana hapa Bungeni na kwenye nchi yetu kwa ujumla. Kimsingi bado hatujawa na mpango mkakati kwa ajili ya kuepusha wafugaji nchini kuwa digidigi katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa ni watu wa kukimbia kimbia, kufukuzwa fukuzwa isivyo halali. Sasa mimi hapa nilikuwa najaribu kutazama, hivi hatujaona bado athari zinazotokana na migogoro kati ya wafugaji na wakulima hadi tunapoteza maisha ya wananchi wetu. Hatujaona athari kwenye jamii zetu kati ya wafugaji na hifadhi, bado hatujaona athari iliyopo kati ya wafugaji wakati mwingine na Kambi za Jeshi. Hawa watu bado hatujaweka mkakati ipasavyo, mkakati madhubuti wa kuhakikisha nao wanafanya kazi zao vizuri na kwa uaminifu. Naomba kwa Mpango huu tulionao sasa wa mwaka huu tunaokwenda wa fedha 2024/2025, niombe sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo atuletee mkakati wa kuhakikisha wale wazazi wake waliomsomesha kwa kuku, kwa ng'ombe waache kukimbia kimbia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu wengi tuliopo hapa Bungeni tumetoka vijijini na wengi tumetokana na mifugo kama siyo mifugo basi ni kilimo, tuwatazame hawa watu. Wale mshahara wao ni ng'ombe, mshahara wao ni mbuzi, tunapokosa mipango mikakati ya kuwawekea mazingira mazuri tunawaumiza wanateseka, mwisho wa siku wanakuwa ni maskini wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana eneo hili liletewe mikakati endelevu ya kudumu ili watu hawa wafanye kazi zao kwa staha, wafanye kazi zao ipasavyo ili waingize katika Pato la Taifa inavyosapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa ufupi sana kwenye eneo la viwanda ni muhimu sana tuje na mkakati wa kuongeza thamani kwenye mazao yetu kwa kupitia viwanda. Tuje na viwanda ambavyo vinakwenda kule kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi hii haina vijiji tena umeme unapatikana kila kijiji cha nchi hii bado maeneo machache tu, ninaomba sana umeme huu usitumike kuwasha tu nyumbani, utumike kwa ajili ya viwanda, hili litawezekana endapo sisi tutaacha kusafirisha malighafi zetu kuzipeleka nje. Tuhakikishe tunakuwa na *processed goods* ambazo tutazipeleka nje, tupeleke bidhaa nje badala ya kupeleka *raw material* nje ya nchi, hii itaongeza kwanza fursa za uwekezaji na itaongeza hata ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tutoke hapa tusiwe kila siku tunaongea hayo hayo tunayarudia, Waziri afanye *research,* Wizara hii ya Mipango ifanye *research,* waajiri watu wazuri kwa ajili ya kufanya tafiti kwenye maeneo haya ya uwekezaji, viwanda, ili tuondokane na masuala haya ya kila siku tunakuja hapa tunalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna mifuko, tunasema tunayo mifuko kila mahali lakini ngozi zinatupwa, ngozi zinaharibika, ngozi hazina thamani ni kwa sababu tumeacha viwanda vyetu vya bidhaa za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna mkakati muhimu sana ambao tunatakiwa tuuzingatie na tuurudie, mkakati wa kuhakikisha yale maeneo ya uzalishaji. Leo tunasema hapa tuna kiwanda, maeneo kama ya *central zone* tuna mazao tunayoyazalisha, tuhakikishe tuna viwanda vyake, ametoka kusema hapa Mheshimiwa Keneth Nollo wa Bahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Magharibi wanayo mazao wanayoyazalisha tuweke viwanda vinavyofanana na mazao wanayoyazalisha hii itarurahisishia sisi kuhakikisha mazao yetu tunaya-*process* kwenye maeneo husika na tunatoa tunapeleka nje ya nchi bidhaa badala ya kupeleka *raw materials.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine la muhimu ni kuendelea kuimarisha na kuboresha miundombinu ya usafirishaji. Bado tunayo changamoto kubwa sana ya miundombinu ya usafirishaji, barabara zetu hasa zile za vijijini ambapo ndiko tunapotoa kule *raw materials*, tunapotoa bidhaa bado hatujaweza kuziboresha ipasavyo, ninashauri tuendelee kuziboresha barabara zetu za vijijini, *SGR* yetu pia tuendelee kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Haya asante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru hii Idara ya Mipango imerudi tena kwa sababu ilikuwepo baadae ikatoka Mheshimiwa Rais ameirudisha tena na ametupatia Waziri kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote au hata ngazi ya familia pasipokuwa na mipango thabiti siyo rahisi kabisa kufikia malengo makubwa ambayo familia hiyo au nchi hiyo imejipangia. Tanzania tulikuwa na usemi ambao naamini bado

tunaendelea nao kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Mimi naamini kwamba bado tunaendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa asilimia zaidi ya 80 au ikishuka sana asilimia 75 bado tunaendelea na suala la kilimo na wananchi wengi ni wakulima. Bado sijaona jitihada kubwa sana ya kuhakikisha tunakuwa na kilimo chenye tija. Pamoja na kuongeza bajeti kwenye Wizara hii bado kilimo chetu hakiendani na ufasaha kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilizungumzia kuwa na kilimo cha kimkakati na safari hii tulizungumzia zao la alizeti, wananchi wakahamasika, wakaanza kulima alizeti, mpaka sasa alizeti imejaa kwenye maghala bado imeshuka bei wananchi wamebaki wanashangaa, kwa sababu tunafahamu kwamba mkulima anapolima lazima anakuwa na malengo yake. Leo hii kama tunakuwa na maghala alizeti imejaa na bado tunaingiza alizeti nyingine toka nje inabidi tujue mipango kama Taifa tunataka nini. Tumewaambia wakulima walime alizeti wakati huo huo tunaingiza alizetu toka nje lazima soko litayumba na anayeumia zaidi ni yule mkulima ambaye yeye kodi inambana na yule anayeleta toka nje ana unafuu wa uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la alizeti nimelisema lakini tunalo zao la parachichi. Tunaita parachichi ni dhahabu ya kijani, leo hii mkulima wa parachichi anahangaika na zao hili, analima lakini mwisho wa siku bado hatujapata masoko ya parachichi. Jirani zetu wa karibu wanakuja wananunua kwa bei ya kutupa kwa mkulima kule chini lakini wanavusha nje ya nchi, wakienda kwenye nchi zao wanaotuzunguka wana-*brand* kama yale maparachichi yametoka katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Taifa lazima tumtetee mkulima tuhakikishe zao hili anapolima liwe lina tija na limletee faida yeye na familia yake lakini mwisho wa siku Taifa lipate faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na kilimo kisichokuwa na masoko, tunakuwa hatujamtendea haki Mtanzania, ni lazima tutafute masoko. Leo hii Tanzania imekuwa nchi ambayo wanalima alizeti, wanalima ufuta, wanalima mazao kama hayo

lakini mwisho wa siku wanakuja kununua madalali na kwenda kuuza nje wakati sisi bado tunayo nafasi. Nimesema kilimo cha tija, leo hii ukienda kwa nchi zetu jirani heka moja ina uwezo wa kutoa magunia 40, sisi tukitoa magunia mengi ni magunia 10! Lazima tubadilike katika kuhakikisha tunatetetea mazao ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumepata wito wa kulima mbaazi, tunafahamu sote miaka mitatu iliyopita tulitangaza mbaazi kwamba ina soko Nchi ya India na wananchi wakalima, mwisho wa siku tuliambiwa tule kama mboga, haiwezekani! Ni lazima tuwe na mikakati ambayo inamsaidia mkulima wa kawaida akiambiwa anaiamini Serikali yake kwamba ninachokifanya kinaenda kutimia kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya kuyaangalia, kwa mfano migogoro ya ardhi pia, hatuwezi kuwa na nchi yenye mipango wakati huo hatuwezi kuitumia vema ardhi yetu. Leo hii kila siku tunazungumzia migogoro. Hakuna namna bora ya kuwasaidia wananchi hasa kwenye mambo ya ardhi, mkulima ajue ana ardhi yake kiasi gani, lakini mfugaji nae aelekezwe ni sehemu gani atasimamia, tutaishia kukaa kwenye migogoro na kuweka miongozo na kulalamika kama Wabunge wakati Wizara husika ipo tunaomba muweke msisitizo katika utunzaji wa ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TMA* wametuambia habari ya mvua, kwamba kuanzia Oktoba mpaka Disemba tutakuwa na mvua. Mimi ninaiomba Serikali ihakikishe inanunua mazao kwa wingi. Tunafahamu mna uwezo wa kununua tani milioni tatu, lakini maghala mliyonayo yanaweka tu tani laki tano na inayobaki tani milioni mbili na laki tano ni kwa watu binafsi. Ni hatari sana kutegemea watu binafsi katika uhifadhi wa chakula wakati Serikali ipo. Tunaomba mnunue chakula kama haya majanga yataendelea na sisi tunamwomba Mungu yasitokee yashindwe, lakini mwisho wa siku lazima tujiwekee akiba na akili ya kuhifadhi chakula chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kama mvua itaendelea kusumbua mwisho wa siku tutakosa chakula hapo mbele kwa

maana mazao yatakuwa hayawezi kuwa sawa sawa, lakini kwa sehemu zile ambazo mvua haijaharibu tunaomba mbolea iende kwa wakati, wananchi waweze kulima mapema labda itaenda kutuokoa kwa hiyo nafasi iliyobaki. Mheshimiwa Waziri husika wa Mipango hakikisha unamlinda mkulima na kumuwekea mipango thabiti ambayo itamsaidia katika ukulima wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunategemea kilimo hatujajitoa kwamba sisi ni mabepari, bado sisi ni wakulima, sisi ni wafugaji na asilimia zaidi ya 70 ni watu ambao wanaendelea kwenye kilimo. Ninaomba utuwekee mkazo uthabiti katika kulinda haya. Hili suala la mvua ambalo linaendelea na ambalo tumeambiwa na *TMA* tusilidharau, tuhakikishe tunaongeza idadi ya kununua chakula kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba majibu Mheshimiwa Waziri atakapokuja tunaongeza kiasi gani cha tani cha ununuzi na kujenga miundombinu ya kuifadhi maghala ya chakula. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka utafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mpango wetu wa Taifa kwa maendeleo pamoja na Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii ya leo na nichukue nafasi hii ya pili kukushukuru wewe kwa jinsi unavyoendelea kuliongoza Bunge letu, kwa namna ya pekee nitakuwa mwizi wa fadhila katika kipindi hiki ambapo dunia inakabiliwa na misukosuko mikubwa ya kiuchumi inayotokana na athari za janga la UVIKO-19 na yanayotokana na vita vya Mataifa makubwa kama Urusi na Ukraine, lakini nchi yetu imeendelea na uchumi wake umeendelea kuwa stahimilivu chini ya Uongozi wa Jemedari Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambae amekuwa ni tulizo na Faraja kwa

Watanzania kutokana na mipango mizuri ya kiuchumi anayoiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa jinsi anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika suala zima, siyo tu la kuweka mipango, lakini kukusanya kodi ambayo leo tunaona fahari, hata leo tutakapotoka kuhitimisha kikao hiki, tutakwenda kupokea magari ambayo ni matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya baada ya kupokea kilio changu cha wananchi wa Kata ya Kitwai katika Wilaya ya Simanjiro ambapo walinielekeza kukutana na Mawaziri wa Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maji pamoja na uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango uliowekwa na Mawaziri hawa kutekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, hivi sasa ni faraja kwa wananchi wa Kitwai na nitakwenda Simanjiro kifua mbele nikijua kabisa tunakwenda kuweka mpango shirikishi utakaotekeleza malengo na maombi ya Serikali katika eneo lile na utakaojali maslahi na mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu ya Kitwai B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu pia kwamba siwezi kukaa tena, baada ya kazi nzuri iliyofanyika hivi karibuni ya kusainiwa kwa mikataba ya zaidi ya kilometa 2,000 za *EPC+ Finance,* kazi ambayo ni mfumo mpya uliobuniwa chini ya Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Prof. Mbarawa akisaidiwa na Mtendaji Mkuu wa *TANROADs* na Kitengo cha *EPC+ Finance*, Eng. Kitahinda na baadaye maeneo yetu ya Mkoa wa Manyara ikiwemo Wilaya ya Simanjiro, Wilaya ya Arusha kwa Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Kiteto na baadhi ya maeneo mengine ikiwemo Kongwa kwa Mheshimiwa Ndugai ambapo tutapata barabara ya kilometa 453.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Waziri wa Miundombinu wa wakati huo pamoja na Waziri wa Fedha ambao wamefanya kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niazime maneno machache ya Prof. Kitila Alexander Mkumbo aliyoyatumia katika ukurasa wa tisa aliyokuwa anazungumza akisema hivi: "Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia usuli huo, ninapendekeza kuwa shabaha kuu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo Mwaka 2024/2025 na miaka ijayo, iwe ni kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi ambao ni jumuishi na unaopunguza umaskini, unaozalisha ajira kwa wingi, unaotengeneza utajiri na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kama tukijipanga vizuri katika kuendeleza kujenga uchumi wetu kwa namna jumuishi na kushughulisha na umaskini wa watu wetu kwa kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ya mazao yanayotokana na ufugaji, thamani ya mazao yanayotokana na kilimo, thamani ya mazao yanayotokana na uvuvi, thamani ya mazao yanayotokana na misitu na madini, nina hakika uchumi wetu unaomgusa mwananchi wa kawaida utaweza kukua na kila mmoja ataona faida yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mantiki hiyo, rai yangu ni kwamba, ni vizuri tukawa na maendeleo jumuishi kwa nchi nzima. Tunapofikiria juu ya maendeleo ya nchi ni lazima tuangalie na baadhi ya jamii nyingine ambazo historia na jiografia imewaweka mahali pabaya na hasa ukizingatia kwamba kesho kutwa kwa maana ya mapema mwakani au katikati ya mwaka tutakaa na kupitisha bajeti ya 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua, mara nyingi tunapopitisha bajeti, tunazungumza habari ya asilimia 65 ya ajira za watumishi ambayo inalipa mishahara ya watumishi, uendeshaji wa Serikali na asilimia 35 ya maendeleo. Nataka niseme wazi jambo hili lieleweke vizuri, kwamba zipo jamii katika nchi hii ambao hawako katika mfumo wa ajira rasmi za Serikali kutokana

na historia, kuchelewa kupata elimu, lakini wote leo wamesoma na hawamo kwenye mfumo wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza, Serikali ije na mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba hakuna jamii inayobaki nje ya uzio wa ajira rasmi ya umma ili kuhakikisha kwamba nchi nzima tunaitendea haki. Kutokufanya hivyo, jamii nyingine unaziacha zikiwa nje kabisa, hawapo kwenye utumishi wa umma na hili sio jambo zuri katika umoja na mshikamano wa Taifa letu kama ambavyo sote tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni rai yangu kwamba tunapofikiria jiografia katika maeneo mengine kama ya kwetu ambapo umbali kati ya kijiji na kijiji ni kati ya kilometa 40 mpaka 70 na shule za kata tunazo, hakuna mwanafunzi anayeweza kutembea kilometa 50 kwenda huko, ni lazima shule zile zote zingekuwa ni za *hostel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni Serikali ilikuwa imetenga fedha kwa ajili ya kusaidia shule hizo za bweni za msingi na sekondari, lakini sasa hivi imepunguza fedha hizo. Nataka niwaambie kwa kupunguza fedha hizo kwa upande wa Wizara ya TAMISEMI, mnatuingiza katika hali mbaya zaidi ya maendeleo ya watoto wetu katika shule hizo za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naiomba Serikali yangu sikivu na hasa Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI, mwone uwezekano wa kukamilisha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliahidiwa mabwawa yapatayo manne katika Wilaya ya Simanjiro lakini mabwawa mawili ambayo ni Kopokyoo na Anaryoo katika Kata ya Comoro na Kijiji cha Naruchugin na hiyo ya Kopokyoo iko katika Kijiji cha Lerumo Kata ya Ruremit. Tuliahidiwa kwamba mabwawa haya yangeweza kujengwa, lakini sasa ni mwaka wa tatu fedha hazitoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi sana kama Wizara ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba itashirikiana na Wizara ya Mifugo ili fedha zile za mabwawa hayo mawili yaweze kutoka hata kabla

ya yale mengine mawili ambayo hayajaweza kuwekwa kwenye bajeti ya miaka iliyopita. Ni ombi langu kwa Waziri mwenye dhamana ili hali hiyo iweze kushughulikiwa na mifugo yetu iweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofikiria maisha ya wafugaji kutoka ufugaji uliozoeleka kwenda katika ufugaji wa kisasa wenye nyama nyingi na maziwa mengi, pia tunazungumzia haja ya kuweka miundombinu rafiki kwa maana ya kupata maji, kwa maana ya kupata majosho, pia kwa maana ya kupata mbegu bora za *Sahiwal, Friesian, Jersey, Ayrshire* na *Simmentals* ambazo zitasaidia wafugaji hawa kufanya mapinduzi ya kuwa na ng'ombe wa kisasa wenye tija kubwa zaidi lakini miundombinu lazima irekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima na watoa hoja wajiandae.

Mheshimiwa Ole-Sendeka, umeshazima kisemeo?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshazima muda mrefu sana, mtafuteni aliyejisahau.

**MWENYEKITI:** Haya, sawa. Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza niungane na wenzangu kukupongeza sana kwa kuwa na hiki kiti kipya, Rais wa Mabunge ya Dunia, kwa kweli umekuwa ni mfano wa kuigwa na Watanzania tunajivunia sana. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili yako wewe *mwananunu*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi

Watanzania wakiwemo Jimbo langu la Nyasa. Pia nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wa Mipango, pamoja na Fedha kwa jitihada kubwa wanazozifanya kutika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda vizuri kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupongeza pia ni kuwatia watu moyo. Nawashukuru sana, Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa wa Ruvuma, Mheshimiwa Kanali Laban Thomas na Mkuu wangu wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Sanga, kwa kweli wanajituma sana. Mwenyezi Mungu awasaidie pamoja na wengine wote wanaowasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo jambo langu litajikita hasa kupitia mipango hii katika eneo la maendeleo jumuishi na hapo naangalia katika maendeleo endelevu ya mwaka 2030 lengo la tatu la afya pamoja na kuleta ustawi wa watu. Katika mipango hii inayoletwa mbele yetu, watu ndiyo kiini, watu ndiyo jambo kubwa kuliko jambo lingine lolote lile. Kwa hiyo, napenda kujikita hapo, na kwa sababu mipango inapendekeza kuangalia maendeleo jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nijikite katika suala la lishe. Nimejiuliza sana, mimi siyo mtaalam sana katika masuala ya afya, lakini kama mtu ambaye huwa napenda kulisikia jambo na kulifanyia mkazi, napenda kujiuliza sana, katika mikoa ambayo inaongeza kwa udumavu ni ile mikoa ambayo inaongoza kwa kilimo au kutoa chakula katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia mikoa hiyo nauona Mkoa wa Ruvuma upo ndani, Iringa upo ndani, Mbeya upo ndani, Njombe upo ndani, Katavi, Rukwa, hasa maeneo haya ya magharibi, sijui wenzetu wa Kigoma safari hii wameponapona vipi; Mtwara na wenyewe wapo kule kusini japo hawapo nadhani ni kwa ajili ya kula korosho na mbaazi, lakini najiuliza ni kwa nini mikoa ambayo inazalisha sana ndiyo inakua na udumavu uliopitiliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imeanza kuzungumzwa siyo leo, toka miaka ya 2010 tumeanza kupata taarifa hizo. Nimefuatilia,

tunapata majibu tu kwamba hawali mchanganyiko wa vyakula na nini. Najiuliza, mbona nikifika hapa Dodoma tunakula tu vile vile, tunafanana fanana? Tofauti ni nini? Nikaona pengine kuna suala lingine ambalo halijapata majibu na halijafanyiwa kazi. Mimi nimeanza kuunganisha udumavu na ukosefu wa miundombinu ya uhakika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia upande huu wa magharibi ya nchi yetu kwa muda mrefu suala la miundombinu na mipango ya kimkakati ya kimaendeleo kidogo ilikuwa inaenda siyo sawa na maeneo mengine katika nchi. Kwa hiyo, inawezekana hiyo ikawa ni sababu. Nikiangalia sasa hivi hata tunapozungumzia reli, mchuchuma; reli itoke Mtwara mpaka *Mbamba Bay* hiyo tunaizungumza na msishangae tukafika miaka bado tunazungumza tu. Bandari ya *Mbamba Bay* tunazungumza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda huu wa kuunganisha kutokea *Mbamba Bay* unakuja mpaka Ludewa mpaka Mbeya ambao ni nzuri sana kwa utalii ingeongeza uchumi, upo tu, hakuna barabara huko. Ndiyo maana maeneo hayo yote yamedumaa. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kumwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, hebu tuangalie kwa kina, hili suala la udumavu katika mikoa hii niliyoitaja unatokana na nini? Ni kweli kula chakula tu? Kama ni chakula, ni kwa sababu gani huko tu ambako sisi tunazalisha zaidi? Kwa hiyo, iko haja ya kutafuta mambo mengine ya kina ya kusaidia mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nategemea katika mpango wa maendeleo unaokuja, suala la udumavu litawekewa mkakati maalum ili kuhakikisha kwamba Taifa hili linatendewa haki kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia hata kwa watu ambao wamebahatika kupata ufadhili wa Benki Kuu wa kwenda kusoma. Nikisikiliza majina, kwa sababu ya ufaulu mkubwa nakuta majina hasa yanakuwa ya upande mmoja. Tunafurahi kwamba wachukuliwe waliofaulu vizuri, lakini yawezekana maeneo mengine huu udumavu ndiyo umechangia hata hawawezi kupata hiyo nafasi. Kwa misingi hiyo, hilo ni suala la hatari katika

nchi. Ni lazima tupate jibu la uhakika kwa nini udumavu unaendelea kuwa katika mikoa hiyo hiyo miaka yote na siyo katika mikoa mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimejiuliza hata kule Kagera, nao kwenye kiwango cha umaskini kila mwaka wanatajwa, lakini akina ushomire ndio wanatoka huko, kwenye udumavu pia wapo. Sababu ni zipi? Hatuwezi kuendelea kuwa na majibu rahisi. Ni lazima tuangalie kwa kina mikoa hii ambayo kila siku inatajwa kuwa ina udumavu, ipate majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunasema kwamba tunaanglia wananchi wetu waweze kuwa na ustawi wa afya njema, lakini pengine hizi shida zinatokea toka kwenye kuzaliwa kwao. Tumejitahidi tumejenga vituo vya afya vya kutosha, sasa hivi na watumishi tunapeleka, lakini suala la kujifungua haliishii tu kujifungua salama kwamba mama ana mtoto, mama yuko mzima wakati wa kujifungua. Anajifungua mtoto wa aina gani? Kuanzia tumboni mtoto aangaliwe lakini pia hata kwenye kujifungua, wapo wakunga. Sasa hivi tunapoajiri tunafanya kwa ujumla, *nurse* anaajiriwa kama *nurse,* lakini pengine hatuangalii wale wakunga. Ndiyo maana wakunga wa jadi bado wana heshima zao kwa namna wanavyowasaidia akina mama kwenye kujifungua na kuondoa changamoto kama hizo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba katika mfumo wetu wa utumishi uangalie Mkunga ana nafasi gani katika ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexender Mkumbo.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/2025 ulioletwa mbele yetu na Wizara ya Uwekezaji na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muumini wa mipango. Tangu niingie katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimeongea sana kwa habari ya mipango ya muda mrefu kama njia pekee ya kulipeleka Taifa mahali ambapo linapotakiwa kuwa. Naomba kuzungumza mambo machache ambayo hasa yamekaa kiushauri hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ili useme mipango mahali popote katika nchi, *data* ya kwanza au takwimu ya kwanza ya muhimu ni takwimu ya *population*. Takwimu ya idadi ya watu ndiyo inaongoza mipango yoyote katika nchi. Idadi ya watu, siyo tu kujua idadi ya watu, ni kuwa na uwezo wa kufanya *simulation* kwamba kufikia 2050 kwa tunavyoongezeka kwa kuzaana sasa hivi, tutakuwa watu wangapi? Kutokea kwenye *simulation* hiyo, ndiyo tuweze kupanga mipango ya tunakoelekea baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee hasa kwa habari ya muundo *(structure)* wa hii Wizara ya Uwekezaji na Mipango. Nafikiri hii Wizara ni ya muhimu sasa kuliko Wizara zote kwa maana hii; kwenye utangulizi wao wameongea kwa habari ya maandlizi ya dira mpya ya Taifa ya 2050. Ina maana tunataka kutengeneza *vision* au maono ya nchi ya kufikia 2050, lakini ili watengeneze maono haya kwanza kama nilivyosema ni lazima wafanye *simulation*. Wawe na uwezo wa ku-*imagine, for the rate of population,* idadi ya watu inavyoongezeka wawe na uwezo wa ku-*foresee* au kufanya *simulation* 2050 Tanzania itakuwa imefikia idadi ya watu wangapi ili *vision* wanayoiweka kwa ajili ya nchi waiweke kwa kuangalia idadi ya watu itakuwa imefikia kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pia wawe na uwezo wa kufanya *simulation* ya *technology*. Maisha tuliyonayo leo ni tofauti na maisha tutakayokuwa nayo 2050. *Technology* iliyopo leo, ni tofauti kabisa na teknolojia itakayokuwepo 2050. Kwa hiyo,

wanapopanga mipango, ni lazima wawe na uwezo wa ku-*foresee* kwamba ile *vision* ya 2050 tunayotaka kuiweka katika nchi ita-*match* na kiwango cha teknolojia na maisha watakayokuwanayo wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nigusie kidogo tu kuhusu *artificial intelligence* au ufahamu bandia. Mwaka jana 2022 nilikuwa Uholanzi. Kule kuna gari zisizo na dereva, kuna ma-*lawyer robot* lakini ni *lawyer*. Nilikuwa Japan, ma-*waiters* wengi kwenye hoteli wanawekwa kuwa *robot*, marubani sasa hivi kwa sababu ya kuepuka ajali, wanaweka *robot,* wanasheria wanaweka *robot*, walimu wanaweka *robot*. Sasa kwenye kupanga mipango ya Taifa, nasi tuweze ku-*foresee* kwamba tunapopanga mipango ya Taifa tuweze kuona ulimwengu huo tunaouendea wa *artificial intelligence (robot):* Je, kwa mipango hii tunayopanga leo, itatosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikafikiri muundo wa Wizara hii ya Mipango, unatakiwa kuwa tofauti kabisa na muundo wa Wizara nyingine. Kwa mfano, ndugu yangu Kunambi amezungumza hapa akasema kwamba, watu wa madini wamekuja na mpango wao wa 2030, wameutoa wapi? Kwa mfano, ili Wizara ya Mipango ipate mipango yake haitakiwi mtu mmoja au watu wawili au watatu au wataalam wa Wizara hiyo kujifungia ndani na kuanza kupanga mipango ya Taifa ya miaka 2050 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa kufanyika, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wataalam wake inaandaa mpango wake wa miaka 50; Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi, inaandaa mpango wake wa miaka 50; Wizara ya Kilimo inaandaa mpango wake wa miaka 50; Wizara ya Maji, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Uchukuzi wanaandaa mipango yao ya miaka 50 na Mipango hiyo inapelekwa kwenye Wizara ya Mipango. Halafu Wizara ya Mipango inakuwa inagema kwenye hiyo mipango, inatupa mpango wa mwaka mmoja kama mpango iliyoleta, ili kwamba siku zijazo nchi nzima tuwe na mipango inayofanana na mipango isigongane. Leo tunayoita mipango, siyo mipango bali ni mtiririko wa matukio yanayotokea kwa mpangilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano kwamba mimi niko Wizara ya Ardhi Maliasili na Utalii. Tunahangaika na Wanyama, wanatoka nje ya hifadhi kwa sababu wanasema maeneo mengi ambayo wanyama wanapita, shoroba zimejengwa. Kwa sababu hiyo, shida ya wanyama kutoka nje ya hifadhi inakuwa kubwa sana kwa sababu shoroba zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shoroba zimejengwa na nani? Ukienda Mvomero pale, Halmashauri ya Mvomero imejenga kwenye ushoroba. *UDOM* hapo imejengwa kwenye ushoroba, *KIA Airport* imejengwa kwenye ushoroba na hizi ni taasisi za Serikali zilijenga kwenye ushoroba zikiwa ziomepata *building permit*. Hii ni kwa sababu ya kukosa maono ya pamoja, kwa hiyo, kama tukipanga maono ya pamoja, tutaondoa *contradiction* kati ya Wizara hii na Wizara ile na tutaifanya nchi ianze kwenda kwa pamoja kama nchi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri sana Wizara ya Ardhi inapeleka maono yake ya miaka 50 Mipango, Wizara ya Fedha inapeleka maono yake ya miaka 50 Mipango, Wizara ya kilimo pia. Halafu Wizara ya Mipango inatoka na *vision* ya miaka 50 ya nchi yote, inakaribisha na *stakeholders* wengine ambao ni wataalam wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nadikiri kuwa Wizara ya Mipango inatakiwa kuwa na muundo wa tofauti kabisa na Wizara nyingine ili iweze ku-*accommodate* maono na *vision* ya nchi kwa pamoja ili tuweze kwenda tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabu ya nchi yetu ni kila mtu ana *speed* kwa mwelekeo tofauti. Narudia tena, tabu ya nchi yetu ni kila mtu ana *speed* kwa mwelekeo tofauti. *Shakespeare* aliwahi kusema, una-*speed* kubwa sawa sawa lakini je, mwelekeo wako ni sawa? Una *Speed* kubwa lakini una uhakika wa kufika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yetu ni hiyo kwamba, tuna *speed* kali sana lakini kila mtu kwa mwelekeo tofauti. Kwa mfano, ukiangalia Ripoti ya CAG ina *leakage* kubwa sana ya fedha za Serikali ambazo kama zingelindwa ingekuwa ni rahisi sana

kwenda kule ambako tunataka kwenda sawa sawa na ambavyo tumepanga kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidokeze kidogo halafu nimalize…

**MWENYEKITI:** Dakika moja malizia, kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna idadi ya Wizara 26, kila wizara ikipeleka mipango yake kwenye Wizara ya Mipango, tutakuwa na mipango 26 ya mpaka 2050 iliyoletwa kwa pamoja na hiyo ndiyo itazaa mpango mmoja mmoja wa mwaka ili tuelekee tunakokwenda. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimekwishasema watoa hoja wajiandae. Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kukushukuru wewe na wasaidizi wako kwa maana ya Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mwenyekiti wa Bunge na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo Mwenyekiti wa Bunge, kwa jinsi mlivyoendesha mjadala huu kwa umakini na uwazi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuwashukuru Kamati ya Kuumu ya Bunge ya Bajeti, kwa uchambuzi wao makini na jinsi walivyoibua maeneo mapya katika mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote na hususani Wabunge takribani 116 waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea ndani ya ukumbi huu, kwa maandishi na wale ambao walitoa taarifa. Nilikuwa nahesabu katika mjadala huu kulikuwa na Taarifa 29 na yenyewe ni michango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli binafsi hizi siku tano nilikuwa darasani. Nimejifunza mengi na kubainisha vema zaidi kuhusu kile ambacho watanzania kupitia Waheshimiwa Wabunge, wanataka kutoka kwa Rais wao, Serikali yao na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu mimi ni mwalimu. Lazima nikiri kwamba, kupitia mjadala huu nillikuwa nafahamu lakini nimefahamu zaidi kwamba, una Wabunge makini sana. Una wabunge mahiri sana na humu ndani kumesheheni kila aina ya utaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana haujawahi kutoa takwimu, jana nilikuwa nafanya uchambuzi kidogo. Nadhani sasa Watanzania wajue kuwa Bunge hili ni tofauti sana. Limejaa watu wenye weledi tofauti na elimu zao ni elimu nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge katika hatua hii. Kwa sababu kwa kweli kazi yetu leo kama Serikali ilikuwa ni kusikiliza na kupokea ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tumefanya. Kwa hiyo, sikusudii kujibu hoja moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika mjadala huu sisi kama Serikali tumeweza kubaini vipaumbele vya nchi yetu. tulikuja navyo lakini kupitia michango ya Waheshimiwa Wabunge unaweza ukaona kabisa watanzania wanataka vipaumbele gani. Naomba nikupe takwimu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji huu mpaka jana, Waheshimiwa Wabunge wameongelea mambo 307. Katika mambo haya mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo: -

(i) Miundombinu ya usafirishaji ndiyo inayoongoza. Imeongelewa mara 68 kama asilimia 22.

(ii) Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Sekta hii imeongelewa mara 65.

(iii) Nishati imeongelewa mara 36.

(iv) Utalii na Hifadhi mara 38.

(v) Viwanda, Mara 33.

(vi) Biashara na Uwekezaji, mara 25.

(vii) Sekta binafsi, mara 12.

(viii) Afya, Elimu na mengine, mara 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, unaweza ukaelewa kwamba, kimsingi katika mipango yetu kwa vyovyote vile lazima tuzingatie maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mjadala wetu tumeendelea pia kubaini baadhi ya kero za wananchi. Tumezipokea na tutazizingatia. Kwa kipekee naomba niwambie wananchi wa Mbalali kwamba, kupitia Mbunge wao makini Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, tumewasikia. Aidha, tumewasikia wananchi wote wanaoishi karibu na hifadhi mbalimbali nchini. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais na viongozi wetu wengine wakuu na kwa niaba ya Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, niwaeleze wananchi kwamba, Rais wetu anathamini maendeleo ya watu kuliko chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu tunachokifanya nia na lengo letu ni hatimaye mwananchi mmoja mmoja, Jamii na nchi yetu kwa ujumla inufaike. Hii ni Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na sifa nyingine, Rais wetu ni muungwana na mpenda haki. Rais wetu ni Mama mwenye huruma na mapenzi kwa watu wake. Rais wetu ni mwadilifu na mzalendo. Maelekezo yake kwetu ni kwamba, tuwatumikie wananchi na siyo kuwaumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote, hii ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Kwa asili yake, panapotokea mgongano kati ya maendeleo ya Vitu, utu na maisha ya watu, CCM siku zote hukaa upande wa utu na Maisha ya watu. Naomba nirudie, zaidi ya yote hii ni Serikali ya CCM, kwa asili yake, panapotokea mgongano kati ya maendeleo ya vitu, utu na maisha ya watu,

siku zote CCM hukaa upande wa utu na maisha ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunao mwongozo, na katika jambo hili tutakaa na kujipanga ili kuona kwamba Hifadhi zetu haziwi kikwazo au kugeuka mateso kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zetu lazima zithamini maisha ya wananchi ili wananchi wazithamini. Tutajipanga na tutakuja na jibu endelevu katika suala hili. Hata hivyo, lazima pia tuombe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba, nchi yetu tayari tumekwishaamua kwamba, ni nchi itakayoongozwa kwa mujibu wa utawala wa Sheria. Tuombe sote tuzingatie Sheria, kama kuna Sheria zina shida ndiyo maana Bunge linakaa kila siku, tuje tubadilishe ili Sheria zitutumikie na siyo sisi kuzitumikia Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala huu Waheshimiwa Wabunge wamebainisha na kusisitiza baadhi ya maeneo mapya ya kipaumbele ambayo kwa kweli katika mpango ama hayakuweko ama hatukuyapatia uzito wa kutosha, tutayazingatia. Mambo haya ni pamoja na yafuatayo: -

(i) *Artificial intelligence,* naomba nitamke hivyo kwa sababu wataalamu wa Kiswahili bado hawajawa na jibu sahihi la *what is artificial intelligence in Kiswahili?*

(ii) Uchumi wa gesi.

(iii) Fursa za kijiografia kwenye kutafuta maendeleo.

(iv) Fursa za mabadiliko ya Tabia ya nchi hasa suala la hewa ya ukaa.

(v) Haja ya kuanzisha mamlaka ya ufugaji na uvuvi, hili limejitokeza. Pia, kwa kweli katika nchi yetu karibu kila sekta ina chombo kinachoisimamia. Hata hivyo, suala la ufugaji na uvuvi nadhani ni eneo la kuliangalia kwa umakini sana.

(vi) Imejitokeza haja ya kuanzisha mamlaka ya maendeleo vijijini. Haya ni mambo ambayo tutayaangalia na kuyazingatia katika kuandaa Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza na kutolea ufafanuzi kidogo kwenye maeneo mawili anbayo yamesisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni maendeleo vijijini na nashukuru na kufurahi kuona kwamba Waheshimiwa Wabunge wameunga mkono na kuweka uzito mkubwa katika eneo hili. Kimsingi tayari tunao msingi wa maendeleo vijijini yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *TARURA* mtandao wa barabara vijijini umongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni; kupitia *REA* vijiji vingi sana vina umeme, kupitia *RUWASA* huduma ya maji imeendelea kusambazwa. Aidha, huduma za Afya na Elimu zinazidi kusambaa katika vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, watu wetu wakishakuwa na afya, wakapatiwa elimu, wakapata maji na umeme na wakaunganishwa katika mtandano wa barabara, tunahitaji kutumia yote haya kama nyenzo ya kuchochea uzalishaji ili hatimaye wananchi wetu huko vijijini wapate fursa za kiuchumi na kutengeneza vipato. Ndiyo nia yetu ya kusisitiza umuhimu wa kuvutia uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo vijijini kwa ajili ya kufanya *primary processing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, umuhimu wa kujenga muafaka wa kitaifa. Wataalamu wa maendeleo wanakubaliana kwamba, moja ya kikwazo cha maendeleo katika nchi yoyote ile, ni pale ambapo panakuwa hakuna muafaka kuhusu Mpango na vipaumbele vya maendeleo miongoni mwa wananchi na hususani watu wenye sauti katika jamii, wakiwemo viongozi wa makundi mbalimbali, wasomi, wafanyabiashara, wanasiasa nakadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ni muhimu sana kushirikishana ili tukubaliane sote. Tukubaliane tunakwenda wapi? Kama ni kubishana tubishane njia ya kwenda, kama safari yetu ni

Mwanza wote tuelekee Mwanza. Mwingine aseme nakwenda kwa gari, ndege, helikopta nakadhalika lakini tunakwenda wapi? Tuwe na mwelekeo mmoja ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kujibu swali moja ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliuliza na lenyewe je, nilipozungumizia kwenye hotuba yangu nilizungumzia umuhimu wa kuwa na watu wazuri kwenye Serikali. Pia, Waheshimiwa Wabunge wameuliza, je, tuna watu wazuri katika utumishi wetu wa umma? Jibu langu ni ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema ndiyo, narejea na ninaangalia walimu zaidi ya 250,000 ambao wanafundisha na kulea watoto wetu sisi tukiwa hapa. Ninapozungumzia watu wazuri, ninazungumzia zaidi ya madakatari na manesi zaidi ya 48,000 wanaotibu watu wetu katika zahanati na vituo vyetu vya afya kwa kiwango ambacho leo Tanzania ndiyo nchi yenye vifo vichache vya wakinamama kusini mwa jangwa la Sahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia zaidi ya mafundi 9,000 ambao wanasambaza maji vijijini. Ninazingatia uadilifu, uzalendo na umakini wa Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Baraza lake la Mawaziri. Ninazungumzia umakini wa viongozi wangu wakuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na kwingine. *Of course,* ninapouzungumzia kwamba tunao, ninazungumzia umakini, uzalendo na umahiri wa Spika wangu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, wote hawani watu wema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachopaswa kufanya ni kuimarisha mifumo yetu ya uwajibikaji na kuendelea kujenga uwezo wa watu wetu kwenye utumishi wa umma. Hatuwezi kukata mwembe wote kwa sababu ya kuoza kwa maembe mawili. Tuyaondoe maembe mawili yaliooza lakini lazima mwembe ubaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kusema, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuhusu umuhimu wa

kuzingatia maadili kwa watoto wetu. Hata hivyo, tunapoendelea kuelimisha vijana wetu kuhusu maadili, tusije tukawaondolea haki yao ya kuwa watoto. Ni muhimu watoto wakabaki kuwa watoto, kwa sababu bila hivyo watakuja kufanya utoto wakiwa watu wazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzingatie kuwa utoto wa watoto wetu hauwezi kuwa utoto ulivyokuwa utoto wetu sisi. Utoto wa watoto wetu mazingira ni tofauti na tukitaka wawe kama tulivyokuwa sisi, tutakuwa tunawakosea. Tuache watoto wawe watoto, tuwape maadili lakini ni muhimu wawe watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo niseme tena kuwa, sisi kama Serikali tumepokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tutayazingatia katika kuandaa Mpango wa Maendeleo ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana kwa fursa hii. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, naye aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuhitimisha hoja ya upande wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mtangulizi Kaka yangu Profesa Kitila, kama Serikali katika hatua hii na kama Kanuni zetu zinavyotutaka, tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Tumewasikiliza na tutakuwa na kazi katika ngazi ya Serikali kufanyia kazi maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika maandalizi ya bajeti ambayo itakuja mapema mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii nikushukuru wewe pamoja na Kamati na Wabunge wote kwa maoni waliyoyatoa kwa wingi na uzito mkubwa. Waheshimiwa Wabunge,

tumewasikilza, tumeyapokea na kwa kweli sisi tuliokuwa tunawasikiliza, tuwahakikishie wapiga kura wenu kwamba wana Wabunge makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa tumepokea, katika kuhitimisha naomba niseme mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo la kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa amefanikiwa kubadilisha kwa kiwango kikubwa kubadilisha kumbukumbu za Bunge na michango ya Wabunge katika kipindi cha sasa katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Naibu Waziri katika Serikali ya Awamu ya Nne na nimekuwa kwenye Baraza Serikali ya Awamu ya Tano. Michango mingi ya Wabunge katika Bunge lako Tukufu yanapokuja masuala ya bajeti ilikuwa ni Wizara ya Fedha inakwamisha Wizara nyingine kwamba, fedha haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kila Mbunge anakiri kupokea fedha nyingi sana za miradi ya maendeleo katika majimbo yenu. Kila mmoja, kila wilaya na hata panapokuwepo na mikutano ama vikao vya Wakuu wa mikoa ama Wakuu wa Wilaya, kila Mkuu wa Mkoa anakiri kupokea fedha nyingi katika maeneo yao ya utawala. Hizo ndizo kazi anazozifanya Mheshimiwa Rais anapokesha na anapozunguka huku na kule, nchi na nchi, bara na bara anatafuta fedha na zinamiminika katika miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja pekee kwenye upande wa bajeti ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu usimamizi wa fedha zinapokwenda kwenye miradi hii ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Mheshimiwa Rais alilitambua mapema tu. Alipoapishwa na wakati anaapishwa na kwenye Baraza la Mawaziri mara nyingi amekuwa akielekeza kuhusu usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua ambazo zimechukuliwa ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziongelea kwa kiwango kikubwa ambazo zinahusisha namna bora ya kusimamia fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya Serikali na ngazi ya Wizara ya Fedha masuala haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasemea, sisi tutaendelea kuyazingatia. Mheshimiwa Rais alielekeza tuimarishe nguvu ya Wakaguzi wetu, *CAG* pamoja na Mkaguzi wa Ndani ili wakague thamani ya fedha katika miradi yetu. Jambo hilo linafanyika na fedha zimeendelea kuongezewa kwa ajili ya Wakaguzi wetu ili wakague miradi ya maendeleo. Nitoe rai kwa viongozi wote Serikalini wakiwemo Maafisa Masuuli tufuatilie kwa ukaribu na tuchukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya utawala wa sheria ni kufuata utaratibu. Natamani hata mimi niende kama ambavyo maoni ya wananchi wengi na hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliliona kwamba lazima panapotokea jambo pachukuliwe hatua pale pale, lakini gharama ya utawala wa sheria ni lazima taratibu zifuatwe. Kwanza panafanyika ukaguzi, pili, panafanyika majibu kutoka kwa Maafisa Masuuli waelezee hoja zile zilizokuwa zimetolewa na hatua zinazofuata panatakiwa pafanyike uchunguzi na baada ya uchunguzi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Hiyo ndio gharama ya utawala wa sheria. Rai yangu watendaji wote Serikalini katika ngazi zao wachukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa nchi yetu ni mzuri sana. Ukienda ngazi ya Wilaya ambako ndiko miradi inatekelezwa pana muundo mzima ule ambao uko katika ngazi ya Kitaifa, pale kwenye mradi pana Mkuu wa Wilaya kama ni ngazi ya Wilaya, pana Kamanda wa TAKUKURU, pana Kamanda wa Polisi, pana Idara, pana Upelelezi, pana Mahakama, pana wa kukamata na pana Magereza. Kila kitu kipo palepale mradi unapokamilikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatuna haja ya kusubiri ziara za Viongozi Wakuu ili tuchukue hatua kwenye maeneo ambayo mradi haukutekelezwa vizuri. Kwa kweli kama darasa

limejengwa vibaya, tukataka tusubiri Rais aje mpaka kwenye kijiji achukue hatua kwenye darasa ambalo lilijengwa vibaya, tutakuwa hatumtendei haki Rais ambaye ametutafutia fedha zimekuja na eneo ni letu na mradi ni wetu, lakini tumeshindwa kuusimamia na kuchukua hatua ama kuchukuliana hatua katika eneo husika. Kwa hiyo nitoe rai ngazi zote zinazosimamia miradi wasimamie ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii ya uandaaji wa Bajeti, hoja zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge tumewaelekeza Maafisa Masuuli wote wazingatie miradi inayoendelea, tuitengee fedha kama kipaumbele miradi inayoendelea ili tusiwe na matumizi mengi ya fedha zinazotumika nje ya bajeti au kuwa na miradi ambayo haina fedha katika bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la fidia, tumelizingatia, maeneo yote ambayo hayana mizozo, tutaendelea kulipa fidia. Tumeelezea habari ya maeneo ambayo yamechukuliwa kwa ajili ya *EPZA*, tumeelezewa maeneo ambayo Serikali imeyachukua kwa matumizi tofautitofauti kwa miradi ya maendeleo. Tutaendelea kulipa fidia kwa maeneo hayo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri. Haya ni maeneo ambayo Taasisi zetu za Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimechukua maeneo kwa ajili ya maendeleo, lakini kuna maeneo ambayo wananchi wanapisha miradi ya maendeleo ama kuna maeneo ambayo tunajenga miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo ambayo tunajenga miradi ya maendeleo mathalani tumeenda tunajenga mradi wa umwagiliaji katika eneo lao, kama tumeondoa nyumba ya mwananchi atalipwa fidia lakini kama tunajenga Mradi wa Umwagiliaji katika eneo ambalo wananchi wale watalima kisasa wale ambao eneo lile unajengwa mradi wa umwagiliaji mathalani bwawa watapewa maeneo ya kulima. Watapewa maeneo ya kulima washiriki kwenye mradi ule wa umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusije tukakwamisha Miradi ya Umwagiliaji tukarudi kenye utaratibu wa kutegemea mvua kwa sababu ya kubishana kuhusu wapi tujenge mradi wa umwagiliaji. Hii ni teknolojia, ni ulimaji wa kisasa, unatuhitaji wote tujitoe kwa ajili ya kukamilisha hilo. Kwenye maeneo haya niliyoyasema ambayo yanachukuliwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo nilimsikia Mbunge wa Segerea akiongelea fidia yao ya eneo la Kipunguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishafika eneo lile na tuliwatangazia wananchi kwamba tunataka tuanze kulipa mwezi Septemba. Kilichotuchelewesha kama ambavyo Mbunge ameongea kwa hisia si kwamba fedha ilikosekana ya kulipa fidia hiyo, isipokuwa ilipofanyika uhakiki iligundulika kati yao miongoni mwao kuna ambao tayari walishapewa maeneo mengine lakini majina yao yalikuwepo tena kwenye fidia kwa maana hiyo ingeweza kuwa kulipa fidia mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine tuliposema tunataka kuanza kulipa, wakawa hawajaridhika na fidia inayotakiwa kulipwa, kwa maana hiyo ilibidi ufanyike utaratibu wa kuweza kulimaliza hilo ili masuala ya kulipa yaweze kuendelea. Kwa hiyo tutaendelea kulipa, tunaamini kwamba baada ya kuwa tumeshamaliza mzozo huo ndani ya mwezi mmoja ama mwezi mmoja na sehemu hivi tutaenda kwenye utaratibu wa kulipa hili likiwa linahusisha Kipunguni pamoja na maeneo mengine ambayo yalikuwa na kesi ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliongelewa pia jambo la masuala ya mifumo tumeshapokea, kazi inaendelea, sasa hivi tunaweka *automation* kwenye masuala ya mifumo ya upande wa Forodha, tutaendelea na mifumo kwenye upande wa kodi za ndani na tutaendelea na mifumo kwa upande wa makusanyo mengine ili maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanayohusisha mifumo yaweze kutekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia, mwenzangu mtangulizi wangu ameongelea suala la kilimo na amegusia pia na masuala ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, kuna hili suala la suala la mifugo. Naomba tukubaliane kwamba mambo yamebadilika sana na jambo hili halihitaji taharuki katika kulishughulikia. Sote tunakubaliana kwamba hatuwezi kudiriki kutangaza kwamba ufugaji katika nchi yetu ni jambo la hatari, wote hatuwezi tukadiriki kufanya hivyo. Ufugaji na mifugo ni mali na ni utajiri wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wengine sisi tuliotokana na jamii hizi za kifugaji tunajua, mifugo inakuwa sehemu ya familia na mifugo ina majina mengine yana majina ya mjomba, wengine shangazi ni sehemu ya familia na mtu akichukua mifugo ni kama vile ameteka watoto wako ni kama vile ameteke sehemu ya familia yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hatuwezi tukatangaza nchi hii kwamba itakuwa ya mifugo tu, utaratibu tuliokuwa tunatumia kufuga zamani, sasa hivi unaendelea kuwa mgumu na tunakokwenda utaendelea kuwa mgumu zaidi. Kwa hiyo ni lazima tukubaliane tena bila taharuki utaratibu mpya ambao tutatumia kulima, utaratibu mpya ambao tutatumia kufuga na utaratibu tutakaotumia kujenga. Hivi vitu vitatu kwa sababu uwingi wa watu unaongezeka, uwingi wa mifugo unaongezeka, mahitaji ya kulima yanaongezeka, hivi vitu vitatu kwa uchache wake lazima vyote viweze kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi nikichunga ilikuwa ukiamka ukishakula, wewe ni kupiga mluzi tu na kuwahimiza, tulikuwa tunaongea tunaelewana na mifugo, ukiamka tu hapa unasema *wochage mapembe bije,* ukishafungulia mlango unaachilia siku nzima mpaka mkishaona mmechoka jua linaelea, mnarudi tena lakini sasa hivi mazingira hayo yanaenda hayawezekani. Kwa hiyo ni lazima tuwekeze kwenye ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu vitu vingi vizuri tunavifanya kwa kuonesha. Ukienda kwenye Maonesho ya Nanenane ukaiona mifugo ile, ni mifugo ambayo inapatikana na kwingine kote duniani. Ukishamaliza maonesho imeisha hiyo,

ukienda kwenye kilimo hivyohivyo, vitu unavyoviona kwenye maonesho ni bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kukabiriana na huku kupungua ama kuongezeka kwa mpambano wa matumizi ya ardhi, ni lazima hivi vitu ambavyo huwa tunavionyesha kwenye Maonesho ya Nanenane ndiyo uwe mtindo wa maisha. Maana yake tutapata wingi uleule kwa ubora, tutapata mahitaji yaleyale kwa kiasi kidogo lakini kwa ubora mkubwa, hiyo itatusaifdia katika matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea na wenzetu wa Wizara ya Mifugo na tumeongea na wenzetu wa Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Rais ametoa hayo maelekezo. Tuwawezeshe wenzetu hawa wa hizi sekta ili kuweza kufanya hizo *transformation* ambazo ndio itakayotoa majawabu ya moja kwa moja ya kupunguza huu ushindani wa matumizi ya ardhi. Hizi sekta zote ni za muhimu katika nchi yetu na ni sekta za kihistoria na vilevile tunaendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Ardhi kuangalia pia mjengo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kujenga huu mjengo tunaotumia kwa huu mtawanyiko mkubwa, sasa hivi kwa sensa hii tuliopewa ukiongeza miaka 20 miaka 30 ijayo tutaelekea milioni 200, kwa mjengo huu tunaoenda nao kwanza *mkumbo singalila*, kama majani yale yanayotambaa hayaendi juu. Hii nchi yote itakuwa na maeneo ya makazi. Tutakosa maeneo ya uzalishaji, hatutakuwa na eneo la kulima, hatutakuwa na eneo la kufugia. Kwa hiyo ni lazima na hilo na lenyewe tumeendelea kuongea huko tunakokwenda mbele tuendelee kuliwekea utaratibu ambao utasaidia kukidhi mahitaji makubwa yanayohitajika ya matumizi ya ardhi, huku ukiruhusu shughuli nyingine za kimaendeleo ziendelee kufanywa na wananchi wetu kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge, tumepokea yale yaliyokuwa yanahusiana na Majimbo yenu, hatuwezi kutaja mmojammoja, kila Mbunge ametaja baadhi ya mambo ambayo yanahusu miradi inayoendelea na mahitaji ya fedha katika sekta za huduma za jamii, miundombinu

pamoja na maeneo mengine. Mchango wa kila mbunge tumeuchukua na tulikuwa tunaongea hapo na Waziri wa TAMISEMI, tumeyachukua na tukishamaliza Bunge hili hiyo ndiyo itakayokuwa kazi tutakayoenda kuifanya ili kuweza kuhakikisha tunapokuja Bunge la Bajeti tuweze kutoa taarifa hiyo ya utekelezaji wa maeneo hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa mara nyingine na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa ngazi hii huwa tunamaliza kwa sura hii ambayo Mawaziri wetu wamehitimisha hapa jambo lililokuwa mbele yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linarejea.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Kabla hatujaendelea sana nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kuishauri Serikali. Kwenye eneo hili la mapendekezo ambayo waliyaleta kwetu na ninyi mmeweka mapendekezo yenu na kama Mawaziri wetu wawili walivyozungumza hapa wameyachukua mawazo ambayo mmeyatoa. Tunaamini watakapoleta sasa ule Mpango utakuwa bora zaidi na pia maelezo mengine yatafuata huko, tutaendelea kuisimamia Serikali na pia kuendelea kuishauri, lakini wamehitimisha vizuri kwamba wameisikiliza michango yenu na wanaenda kuyafanyia kazi hayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kitila Mkumbo, pamoja na mambo mengine wewe kazi yako ni kubwa zaidi ya kuzifanya Wizara zote mipango yake isomane kwa sababu tunazungumza hapa kuhusu hii migogoro. Tunatamani kwa sababu sasa Tume imerejea, lakini pia siyo Tume tu imerejea kuna Waziri anayehusika na jambo hili, tunaamini haya mambo tuliyokuwa tunayapitia huko nyumba ya migogoro yatakwisha. Kama yanakuja basi yatakuwa yanakuja si kwa sura iliyopo sasa kwa sababu lazima mipango kama nilivyosema isomane, hata haya tunayozungumza ya maliasili na wananchi. Hii nchi ina ardhi pamoja na hizi changamoto lakini ina ardhi, ina *ranch* nyingi sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo ukifikiria ule uharaka ambao huwa mifugo inabidi iuzwe wakati nchi ina maeneo hii, kwa nini mifugo hiyo isipelekwa huko, kwenye hizo *ranch* za Taifa, kama watu hawajajitokeza basi iwe mifugo ya Taifa, halafu *ranch* zetu ziwe na hiyo mifugo. Kwa hiyo, kwa kweli tunakutegemea sana kwenye eneo hili na tunaamini mawazo ya kuanzia ambayo Wabunge wameyasema kwa sababu na wao walijielekeza kwenye Mpango huu ambao mlikuwa mmeuleta, tunaamini mengine yataendelea kutolewa na mtaendelea kuyatumia huko baadaye kwenye kuandaa Mipango ya muda mrefu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na ratiba yetu wakati ikisomwa Miswada ya Sheria ya Serikali kuna Muswada mmoja ulirukwa Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Kwa hiyo, nitatoa fursa ili huo Muswada usomwe kwa mara ya kwanza ili uingie kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge ili ninapouelekeza kwenye Kamati uwe hapa Bungeni umekwishasomwa.

Kwa hiyo, nitatoa fursa hiyo kabla hatujaendelea sana na tutaendelea na ratiba yetu, nitatumia Mamlaka niliyonayo kwenye Kanuni ya 34, kwa hiyo tutakaa hapa mpaka tumalize kazi iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Katibu kwa ajili ya kutusomea Muswada ambao ulikuwa umerukwa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huo umesomwa mara ya kwanza, kwa hiyo utaingia kwenye orodha ile tuliyokuwa tumeisoma mwanzo na nitaielekeza kwenye Kamati zinazohusika ili iweze kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA BINAFSI ZA WABUNGE**

**Hoja ya Kuazimia Kuwahamisha Maafisa Ushirika katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa Ugani chini ya Wizara ya Kilimo**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunayo hoja binafsi ya Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, sasa nimwite aje awasilishe hoja yake hapa mbele kwa muda wa dakika 15. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE**: Mheshimiwa Spika, Hoja ya Kuwahamisha Maafisa Ushirika katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa Ugani chini ya Wizara ya Kilimo. Chini ya Kanuni ya 60(2) na Kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa mwaka 1998 Serikali ilifanya mabadiliko ya muundo wa Serikali na kufanya uamuzi wa kugatua madaraka kwa Kiingereza *Decentralization by Devolution (D by D)* kutoka Serikali Kuu na kuyashusha katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji. Uamuzi huo ulikusudia pamoja na mambo mengine kuboresha kupeleka huduma kwa wananchi na kuwashirikisha katika maamuzi ya huduma zinazowahusu. Chimbuko la mabadiliko hayo ni andiko la kisera *Policy Paper on Local Government Reform* lilioandaliwa mwezi wa Oktoba, 1998. Mabadiliko hayo yalifanywa kwa nia ya kuboresha na kuongeza ufanisi kwa kupeleka zaidi vipaumbele kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ugatuaji wa madaraka ulihusisha kupeleka rasilimali fedha na wataalam wa aina zote katika ngazi za Mikoa, Halmashauri wakiwemo Warajisi Wasaidizi wa Ushirika katika ngazi ya Mikoa na Maafisa Ushirika ngazi ya Wilaya, aidha, mabadiliko hayo yaliwahusu pia Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ugatuaji wa madaraka kwa utaratibu uliopo sasa, umesababisha Maafisa Ushirika waliopo kwenye Wilaya na Maafisa Ugani kwa sehemu kubwa kuwa watumishi wanaowajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Aidha, katika ngazi ya Mkoa kuna Mrajisi Msaidizi wa Ushirika wa Mkoa ambaye anawasimamia Maafisa Ushirika wa Wilaya waliopo kwenye Halmashauri, Mrajisi Msaidizi wa Mkoa ambaye naye ni sehemu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya 2013 ambapo kwa mujibu wa Sheria hiyo Tume ndiyo yenye wajibu wa kusimamia, kuendeleza ushirika nchini na Muundo wa Tume hii ulipitishwa na Rais mwaka 2015 ambapo Warajisi Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika ngazi ya Wilaya ni sehemu ya Tume ya Ushirika ya Maendeleo. Hii inafanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria. Hata hivyo, watumishi hao waliopo kwenye Ofisi za Katibu Tawala za Mikoa na Halmashauri mtawalia, ni waajiri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI ambao wakuu wao wa kazi na mamlaka zao za nidhamu ni Katibu Tawala wa Mkoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 14(3) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya 2013, majukumu ya Tume yanayohusu usimamizi na uhamasishaji wa ushirika yanatekelezwa na Tume kupitia Maafisa Ushirika wa Wilaya. Msingi wake unajengwa kwa uhalisia kwamba Afisa Ushirika wa Wilaya ndiye msimamizi wa karibu kabisa wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14(2) cha Sheria kinaipa Tume uwezo wa kutoa maelekezo kwa Maafisa hao au kuomba taarifa kutoka kwao kwa mujibu wa Kifungu cha 16 cha Sheria. Hata hivyo, utekelezaji wa sheria hiyo umekuwa na mapungufu na umeonesha ugumu mkubwa katika eneo hilo kwa kuwa Tume haina uthibiti wa moja kwa moja wa watumishi hao na maelekezo ya Tume yasipofuatwa Tume haina mamlaka ya kuweza kuwawajibisha watumishi husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia; Kifungu cha 14(2) cha Sheria kinaipa Tume uwezo wa kutoa maelekezo kwa Maafisa hao au kuomba taarifa kutoka kwao, kwa mujibu wa Kifungu cha 16 cha Sheria. Hata hivyo, utekelezaji wa sheria hiyo umekuwa na mapungufu na umeonesha ugumu mkubwa katika eneo hilo kwa kuwa, Tume haina uthibiti wa moja kwa moja wa watumishi hao na maelekezo ya Tume yasipofuatwa Tume haina mamlaka ya kuweza kuwawajibisha watumishi husika.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Nina taarifa kuwa mwezi Machi, 2023 Tume ya Ushirika ilifanya uchunguzi wa Vyama vya Ushirika 20 kuhusiana na mwenendo wa uendeshaji wa Vyama hivyo. Uchunguzi huo ulibaini kuwa kulikuwa na mapunjo ya bei kwa wakulima kwa zaidi ya shilingi milioni 74. Kufuatia mapungufu hayo, wakulima walikatwa makato zaidi ya ilivyotakiwa karibu kwa shilingi 1,700 kwa kilo ya kahawa. Aidha, wakulima wanachama walikatwa fedha shilingi milioni 116 ili kurejesha mikopo ambayo ilikopwa na watu binafsi. Vilevile, Tume ilibaini kuwepo kwa malipo hewa ya kiasi cha shilingi milioni 26 kwa vyama vitano katika Wilaya ya Mbozi pekee yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maafisa Ushirika na Mrajisi Msaidizi, Tume ilibaini mapungufu makubwa katika utendaji

wao na kuwataka kuimarisha ukaguzi, usimamizi na udhibiti wa vyama vya ushirika katika hatua nyingine. Waziri wa Kilimo alipokuwa akihitimisha mjadala wa bajeti ya Wizara ya Kilimo Bungeni Tarehe 09 Mei, 2023 alieleza kuhusu uchunguzi uliofanywa na matokeo na mapendekezo ya Tume hiyo. Hata hivyo, Wizara haijaweza kuchukua hatua za nidhamu kwa sababu za kimuundo. Waziri alitoa maelekezo Bungeni kuwa, vyama vya ushirika visikope fedha na kuwabebesha riba wanachama, jambo ambalo limetokea tena katika maeneo yaleyale na Maafisa Ushirika na Mrajisi Msaidizi wameridhia ukopaji huo, licha ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, changamoto za ushirika zilizobainishwa na Tume. Kabla ya uchunguzi uliofanyika katika Vyama vya Ushirika 2023 mwanzoni na mwanzoni mwa mwaka 2022, Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliwasilisha mbele ya Waziri wa Kilimo changamoto inayopata Tume katika kuwasimamia Maafisa Ushirika wa Wilaya nchini. Changamoto hizo ambazo zinagusa nchi nzima ni pamoja na:-

(a) Baadhi ya Halmashauri kuwa na Maafisa Ushirika wengi kuliko uhitaji;

(b) Baadhi ya Halmashauri kukosa kabisa Maafisa Ushirika;

(c) Baadhi ya Maafisa Ushirika kukaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu;

(d) Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutokuwa na mamlaka ya kuajiri, kuwapangia vituo au kuwachukuliwa hatua za kinidhamu Maafisa Ushirika;

(e) Baadhi ya Maafisa Ushirika waliopo Sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Mitaa kupangiwa majukumu mengine tofauti na ushirika; na

(f) Mamlaka ya uteuzi wa Maafisa Ushirika wa kusimamia ushirika katika ushirika kutokuwa wazi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuhamishia Maafisa Ushirika chini ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Tume ilipendekeza kwa Waziri wa Kilimo mbinu za kutatua changamoto hizo. Tume ilipendekeza kuwa:

(a) Maafisa Ushirika waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wahamishiwe Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuwa mamlaka hizo sasa hazina majukumu ya msingi ya kushughulikia ushirika na badala yake zibakie na utaratibu na uhamasishaji;

(b) Kuwe na Maafisa Ushirika Mfawidhi katika Wilaya ambae atateuliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika;

(c) Tume ipewe kibali cha kuajiri Maafisa Ushirika wa kutosha kufikia idadi ya Maafisa Ushirika 662 wanaohitajika; na

(d) Tume iendelee na jukumu la kutoa Miongozo ya namna bora ya usimamizi na uhamasishaji wa ushirika katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ushirika na ugani. Kumekuwa na haja ya kuimarisha muunganiko wa shughuli za ugani na shughuli za ushirika pamoja na jitihada zingine zilizopo katika ngazi ya Halmashauri hususan umwagiliajia. Umwagiliaji una maeneo makuu mawili: Kwanza ni eneo yabisi hususan miundombinu; na Pili, ni eneo la uenezaji kuhusu kanuni bora za kilimo ambazo hutolewa na Maafisa Ugani. Kutounganika kwa maeneo hayo ya umwagiliaji ndiko kunakoleta kuwepo kwa mchango mdogo wa huduma za ugani katika uchumi na usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuhamishia Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani kwenda Tume ya Umwagiliaji kutodhoofisha utekelezaji wa ugatuaji wa madaraka. Marekebisho ya Sheria yanayopendekezwa yatasababisha Maafisa Ushirika waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhamishiwa katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika kama nilivyoeleza awali. Mamlaka za Serikali za Mitaa ziondolewe majukumu ya msingi ya kushughulika ushirika badala yake zibaki na utaratibu na uhamasishaji. Marekebisho hayo, yanalenga kuongeza ufanisi katika kutekeleza ugatuaji wa madaraka na siyo

kudhoofisha, kwani hatua hiyo itaimarisha mifumo ya kufikisha huduma kwa wakulima wote nchini na kuboresha utendaji wa Maafisa Ushirika.

Mheshimiwa Spika, huduma za umwagiliaji na huduma za ugani hutolewa na wataalam wa kilimo wenye taaluma za agronomia, kilimo mseto, mazao ya bustani, uchumi kilimo, uhandisi kilimo, ufundi sanifu kilimo, afya ya mimea, uhandisi umwagiliaji, ufundi sanifu umwagiliaji na ufundi sanifu usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo, uchumi wa nyumbani na sayansi ya chakula, ugani na huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayopendekezwa yataimarisha muunganiko wa shughuli za umwagiliaji na huduma za ugani kwa kuwa hayo ni masuala yanayotegemeana katika kuwezesha kilimo chenye tija. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa shughuli za uzalishaji mazao hususan kupitia huduma za ugani unahitaji kutumia taaluma mbalimbali zinazoratibiwa kwa pamoja ili kuongeza uzalishaji na tija. Utaratibu huu utafanyika vizuri ikiwa mageuzi ya uboreshaji wa huduma za ugani na maendeleo ya umwagiliaji unaratibiwa na taasisi moja ambayo kwa muktadha huu ni Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa suala hili linalopendekezwa limewahi kujitokeza kwenye sekta ya ardhi, barabara na maji. Serikali ilichukua hatua ambazo zimeonesha kuzaa matunda. Mamlaka ya uwajibikaji kwa Maafisa katika Idara ya Ardhi ya Halmashauri yalihamia kwenye Wizara ya Ardhi na kumpa Waziri wa Ardhi na Katibu Mkuu katika Wizara ya Ardhi fursa ya kuwapangia vituo, kuwahamisha na kuwawajibisha kinidhamu Maafisa waliopo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Maafisa hao wameendelea kuwa na vyeo vilevile, majukumu yaleyale na kutumia majengo yaleyale na vitendea kazi vya Halmashauri zao isipokuwa sasa Waziri na Katibu Mkuu wa sekta wanaweza kuwafikia na kuwahoji juu ya utendaji wao. Hali hii inasaidia kuleta ufanisi kwani Wizara ya kisekta inafahamu kuhusu taaluma yao, majukumu yao na sera zilizopo kwenye eneo hilo vema zaidi kiasi cha kutambua utendaji unaofaa na usiofaa wa Maafisa wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara na maji zilianzishwa Wakala zinazojitegemea za *TARURA* na *RUWASA* mtawalia ili kuimarisha ufanisi na kuweka mtiririko mmoja wa maelekezo kwa wataalam. *RUWASA* ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019. Katika utendaji kazi, *RUWASA* imefungua ofisi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya zinazoongozwa na Mameneja wa Mkoa na Wilaya ambao wanawajibika kutoa taarifa za kiutendaji kwenye vikao mbalimbali, ikiwemo Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* na Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, wanawajibika kuwasilisha mipango na taarifa za utekelezaji katika Baraza la Madiwani kwa taarifa. Taasisi hiyo hushiriki katika vikao na shughuli mbalimbali za Halmashauri kwa mwaliko maalum kutoka Mkurugenzi Mtendaji. Muundo huo umeboresha ugatuaji wa madaraka na kuimarisha utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ushirika ipo Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo inasimamia ushirika na kwa mujibu wa muundo wao ni mabadiliko machache tu yanahitajika kuweza kupata mtiririko wa usimamizi unaotarajiwa na unaofaa hususan kuiwezesha Tume kuwasimamia Maafisa Ushirika wote na kuwa muunganiko katika utaratibu kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, naomba kutoa hoja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Maafisa Ushirika ni kiungo muhimu katika kuendeleza kilimo cha mazao ya ushirika kwa kuvisimamia Vyama vya Ushirika nchini na pia ugani ni kiungo muhimu katika utoaji wa maarifa na kueneza teknolojia na kanuni bora za kilimo kwa wakulima katika skimu za umwagiliaji;

Na kwa kuwa, katika utekelezaji wa majukumu yao, Maafisa Ushirika wanapata ugumu wa kutekeleza maelekezo ya Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika na maelekezo ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa wengine wa Ofisi ya Rais TAMISEMI;

Na kwa kuwa, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ndio wasimamizi wa ushirika na wanashindwa kuwasimamia kikamilifu Maafisa Ushirika wa Wilaya, hivyo kusababisha kulegalega kwa ushirika katika maeneo mengi nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge lako tukufu linaazimia kwamba Serikali ibadili mfumo uliopo sasa na kuwafanya Maafisa Ushirika wa Wilaya na Maafisa Ugani waliopo kwenye Halmashauri zote nchini kuajiriwa, kusimamiwa na kuwajibika kwenye Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Tume ya Umwagiliaji mtawalia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu hoja kama hii inaweza kufika hapa Bungeni kwa njia mbili, moja ni kama hii tuliyoitumia na ya pili ni hoja kama hii kuipeleka kwenye Kamati halafu ikipelekwa kwenye Kamati ikishapitiwa kwenye Kamati, akisoma mwenye hoja anakuja Mwenyekiti wa Kamati kutoka mawazo ya Kamati, lakini hii njia tuliyoitumia leo maana yake tumetumia njia ambayo mtoa hoja ameleta moja kwa moja hoja ambayo haijapita kwenye Kamati, kwa hivyo, Mwenyekiti wa Kamati hawezi kuja kutoa mawazo yake, lakini tutaoa nafasi baadaye upande wa Serikali baada ya michango kutoa mawazo yao kuhusu hoja hii, halafu baadaye Bunge litahojiwa na kufanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, wanaotaka kuchangia tutatoa nafasi tatu pekee halafu tutawapa upande wa Serikali. Mmesimama wengi na kwa sababu nimeshasema tatu, kwa sababu ya hayo mazingira, nitachagua wale niliowaona kwanza.

Mheshimiwa Justin Nyamoga Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Josephat Kandege na sasa inabidi nichague mwanamama, huko wako wanamama na huku. Nilikuwa nimemwona wa huku kwanza lakini sasa kwa sababu ya uwakilishi. Mheshimiwa Agnes Hokororo na Mheshimiwa Kunti Majala. Upande wa Serikali Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naona watu wanaondelewa kwako na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa hiyo orodha niliyoitaja hapa naomba nisaidiwe kuletwa hapa. Haya, nilikuwa nimemtaja kwanza Mbunge wa Kilolo, Katibu wakati analeta hapa mbele orodha ya Wabunge niliowataja. Mbunge wa Kilolo atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege.

Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza wa hoja hii.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ugatuaji wa madaraka ulipangwa kulenga kuendelea kuzipa nguvu Halmashauri kujisimamia na kusimamia shughuli zake. Kumekuwa na utaratibu wa kunyofoa vipande mbalimbali ndani ya Mamlaka za Halmashauri. Ilianza Ardhi kidogo, *TARURA* ikatolewa, ikaja Ardhi imetolewa, Maji imetolewa na kila moja inatolewa kwa namna yake kwa hoja mbalimbali zinazoletwa hapa ndani, ikiwa utaratibu huu utaendelea maana yake ni kwamba mwisho Halmashauri zitabaki bila Idara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kukawa na mapungufu katika utekelezaji, nadhani ni vema tukaangalia namna bora ya kuimarisha Halmashauri zetu na usimamizi wake, hata hizi zilizotolewa zikaangaliwa jinsi gani Halmashauri zinaweza zikawa na udhibiti badala ya kuendelea kunyofoa kila kipande na mwisho tukaacha Halmashauri hazina kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja iliyowasilishwa inaweza ikawa na mashiko, udhaifu kwenye Ushirika unaweza ukawepo, kwa hiyo

siyo kwamba napinga kwamba kwenye Ushirika kuna changamoto, najua zinaweza zikawepo lakini suluhisho lake si kuendelea kunyofoa Idara katika Halmashauri na mwisho wake kuacha Halmashauri hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tuna mashaka na jinsi tulivyofanya ugatuaji wa madaraka ni bora tufute sasa hizo Halmashauri zisiwepo kuliko kila siku unatoa kipande hiki, unatoa kipande hiki, mwisho unaimaliza Halmashauri kwa hiyo itakuwa na Mkurugenzi tu.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba…

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kwezi.

**TAARIFA**

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpatie taarifa mzungumzaji kwamba hata baada ya kuwa wamechukua baadhi ya watumishi kwenye Idara hizo alizozitaja, kwa maana ya Ardhi, Maji na *TARURA* imetuwia vigumu sana Madiwani. Kwanza imekuwa ni kama hisani kwa hiyo utendaji wa kazi wa Madiwani ambao ndio wanatakiwa kutafsiri miradi na mambo yote yanayoendelea kwa faida ya nchi yamekuwa magumu sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nimpe taarifa hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Kwezi ulikuwa unatoa taarifa siyo unachangia. Mheshimiwa Nyamoga unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa na mimi hoja yangu kwa kweli kwenye hili nafikiri tujenge mifumo mizuri ya ugatuaji wa madaraka, tuimarishe Halmashauri

na hata hizi ambazo tumezitoa tutafute namna bora ya kujenga uhusiano na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, maji, barabara na zingine zisimamiwe vizuri lakini Halmashauri ziwe na uwezo lakini tusiendelee kunyofoa moja baada ya nyingine.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Manonga.

**TAARIFA**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kumpata taarifa mchangiaji, tumeona ugatuaji katika Halmashauri zetu kwa mfano *TARURA* toka ilipowekwa mamlaka yake, sasa hivi inafanya vizuri zaidi tofauti na ilivyokuwa mwanzo. Kwa hiyo, hawa Maafisa wetu wakati mwingine wakiwa Halmashauri hata mafuta hawana. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga unapokea taarifa hiyo.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, hata sijaelewa, kwa hiyo sitapokea. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa ukisema hujaelewa, hujamsikia ama hoja yake huikubali? Kwa sababu sasa…

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, sijamsikia.

**SPIKA:** Basi wacha nikueleweshe, anasema hivi: Imetolewa mifano ya *TARURA*, *TARURA* ilivyoondolewa Halmashauri yeye kwa taarifa anayokupa ni kwamba ufanisi umeongezeka. Kwa hiyo, unaipokea taarifa hiyo? Ndiyo taarifa ya Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ufanisi kuongezeka napokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba kuna haja ya kuboresha Halmashauri zetu ziwe na usimamizi, ziwezeshwe, hata kwenye hilo suala la ushirika ukiangalia changamoto utaenda kukuta si kwamba kwa sababu iko kwenye Halmashauri, utakuta kuna matatizo ya kibajeti, utakuta kuna matatizo ya kiutawala na utakuta kuna matatizo mengine na siyo suala la kiutawala. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Kengele ni moja, samahani kengele imegonga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Shukrani.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, kwa hili siwezi kuunga mkono hoja iliyowasilishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Kunti Majala, ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoletwa mbele yako.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze *outright* kwa kusema kwamba siungi mkono hoja iliyotolewa. Naomba wenzangu watanikumbusha katika mahojiano ambayo Hayati Baba wa Taifa aliwahi kufanya na kujutia kati ya maamuzi ambayo aliyafanya katika uongozi wake alisema kwamba ni kitendo cha kuua Halmashauri na kurudisha Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika hoja ambayo imeletwa ni kama vile tunataka turudie makosa, ile *sense of ownership* ya watu wetu tuanze kuinyang'anya kwa *style* ambayo inaonekana

kwamba hakuna *performance* nzuri, kwa hiyo, tuanze kuinyofoa. Maana yake itafika mahali hata vikao vya *WDC* ambavyo vinaketi vitakuwa havina maana yoyote na watu wetu kwa ushiriki…

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, muda mchache sana.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Inatokea wapi taarifa? Mheshimiwa Kandege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kasalali Mageni. *(Kicheko)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji ya kwamba ili halmashauri zetu ziendelee kuwepo na kutekeleza majutio na kauli ya Baba wa Taifa, kinachopaswa kufanyika sasa ni kuimarisha mfumo wa halmashauri zetu na kurudisha vitu vyote ambavyo viliondolewa halmashauri ikiwemo maji, barabara na ardhi na siyo kuondoa kilimo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege, unapokea Taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa kwa maana ya kuboresha. Hii inaonesha jinsi ambavyo sisi kama Taifa tulivyoamua kwamba *D by D* iwepo tulikuwa tunamaanisha kwamba wananchi lazima wakiri na wamiliki Serikali yao ili wawe sehemu ya maamuzi ambayo yanaenda kufanyika kule *Central Government*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hii *style* ambayo imeanza kuja, hiwezekani tukachukua labda udhaifu wa Halmashauri *X then* tuka-*conclude* kwamba halmashauri zote hazifanyi vizuri. Kwa hiyo, tuhangaike *case by case;* hata hizi taasisi ambazo zimeanzishwa, cha kwanza kulikuwa na *budget constraint* ambayo inatibiwa, ndiyo maana *TARURA* inafanya vizuri kwa sababu ina bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali mtuambie: Je, ni kweli mmeshindwa? Katika hizi taasisi ambazo wanataka zihame, mmeshindwa kiasi kwamba kwenye halmashauri haiwezekani, mmefanya michakato yote imeshindikana mpaka mnasema mna *give in* ili watu wetu wasipate nafasi ya kushiriki na liwe linatoka *Central Government* kushuka kule chini? Hakika naamini inahitaji *research* ya kutosha. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aliyekuja na hoja…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** …kwa *research* ambayo amefanya upande wake tu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege kuna taarifa na kengele imegonga. Sasa acha niwape dakika moja mmalizie. Mheshimiwa Getere, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tuko kwenye mapinduzi makubwa sana ya kilimo. Mimi sidhani kama kuwatoa ushirika na kujipanga vizuri katika kutafuta mazao ambayo washirika watajipanga vizuri na wakapata utaratibu mzuri ili waweze kuongeza mapato ya halmashauri kwa mazao hayo, eti itakuwa ni kosa. Tuwe nao na mazao hayap. Wakisimamia vizuri pamba, wakisimamia vizuri kahawa na tunahitaji ushirika, mimi naomba hiyo iondoke, irudi kwenye Wizara ya Kilimo mapato yapatikane. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Kandege unaipokea taarifa hiyo? Muda wako ulikuwa umeisha, kwa hiyo, sekunde 30.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa iko *against* na mtazamo wangu. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile hakuna namna ambavyo naweza nikaipokea ikanisaidia. Sana sana imsaidie yeye kwa upande wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kadiri ninavyosikiliza michango, natafakari, wale waliosimama kuunga mkono hoja, sijui walikuwa ni akina nani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Agnes Hokororo atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nianze kusema kwamba siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 145 na ibara ya 146 kwa ruhusa yako sijui nirejee ama muda hautoshi? Muda hautoshi, lakini Serikali za Mitaa imeandikwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kurekebisha kwa mtindo huo. Kama kuna udhaifu wa Sheria Na. 6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013, sehemu ya kuyafanyia marekebisho ni kuileta hiyo Sheria irekebishwe lakini siyo kwa kunyofoa vipande kwa vipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya mtoa hoja yamejieleza vizuri sana kwamba Mrajisi Msaidizi wa Ushirika wa Mkoa kwa sasa ni sehemu ya TAMISEMI, halikadhalika Maafisa Ushirika waliopo kwenye halmashauri zetu ni TAMISEMI. Tatizo liko wapi? Usimamizi unawezekana, warajisi wasaidizi wa mkoa ni sehemu ya TAMISEMI, wawasimamie vizuri hao Maafisa Ushirika kutoka kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiniuliza, iko changamoto kubwa ambapo upungufu uko kwenye hiyo Sheria Na. 6 iliyoanzisha vyama vya ushirika ya 2013 iletwe Bungeni, tuifanyie marekebisho ili warajisi waweze kufanya kazi yao vizuri na Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani kwenye ngazi za vijiji na kata waweze kufanya kazi

zao. Hatuwezi kuacha wazururaji wasimamiwe na Tume ya Ushirika kutoka Makao Makuu, kwenye Tawala za Mikoa hakuna, kwenye Halmashauri Mkurugenzi hawajui, Madiwani hatuwajui, watakuwa wanafanya kazi za nani? Ugatuaji *(D by D)* lazima iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Muda wake umekwisha Mheshimiwa. Kwa hiyo, ameshaketi, hawezi kupewa taarifa tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kunti Majala, atafuatiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu. La kwanza, naomba kuunga mkono hoja iliyoletwa Mezani. Kwa nini naunga mkono hoja hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ugatuaji wa madaraka, suala la uwajibikaji haujaanza leo wala jana. Suala la watu wa *TARURA* au *RUWASA* tumekuwa humu ndani, tulianza kupiga kelele. Wakati wakiwa wanasimamiwa na halmashauri, halmashauri zetu zilikuwa haziwapi nafasi watumishi wetu wa kwenye hizi idara ili ziweze kutekeleza wajibu na majukumu yao. ndiyo maana Bunge likafikia maamuzi ya kuwatoa *RUWASA* pamoja na *TARURA* wawe taasisi wanaojitegemea waweze kupata fedha lakini pili waweze kutekeleza wajibu na majukumu yao.

Mheshimiwa Spika…

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, wahandisi wa *TARURA* ama *RUWASA* walikuwa wameishia kwenye ngazi ya wilaya. Kuna wilaya ambazo walikuwa wana mmoja, wawili na halmashauri nyingine hazikuwa hata na mmoja. Unapozungumzia Maafisa Ugani unawazungumzia wataalamu ambao wako kwenye ngazi ya kijiji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Kunti Majala unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, suala la wahandisi na suala la watu wa maji kuishia wilayani, hilo siyo suala la Bunge wala halmashauri, ni suala la Mpango ambao mmepanga ninyi wenyewe Serikali. Mlikuwa na sababu ya kuwapeleka mpaka mikoani. Tunachoangalia hapa, ni namna gani Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani wanatekeleza majukumu yao kwenye halmashauri zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, leo tumegawa pikipiki kwa Maafisa Ugani kwenye halmashauri zetu. Uliza zile pikipiki leo zinafanya nini kwenye halmashauri zetu? Wabunge mko humu ndani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaheshimu sana mchango wa Mheshimiwa Mbunge

anayezungumza, na nimeridhia alivyosema kwamba masuala ya ugatuaji hayajaanza leo. Tulivyoanza uhuru Serikali yetu ilikuwa *highly centralized,* mwaka 1972 tukafanya *deconcentration* kwa madaraka mikoani.

**SPIKA:** Sawa, mpe taarifa nitakupa muda wako wa kuchangia. Mpe taarifa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kama nitapata muda, lakini taarifa ninayotaka kumpa ni kwamba mwaka 1982 Mwalimu Nyerere aliulizwa, katika vitu anavyoumia ambavyo amekosea akiwa madarakani ni yapi? Alitaja mambo mawili. Moja ilikuwa ni kuua ushirika; na la pili kuua Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimpe taarifa kama ataipokea. Ndiyo maana mwaka 1984 ikarudishwa kwenye Katiba, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, siipokei. Laiti kungekuwa na uwezekano wa Hayati Baba wa Taifa kufufuka, akaja akasimama hapa mbele, akaona ubadhirifu unaofanywa na Maafisa Ushirika pamoja na ushirika kwa ujumla wake, tungelaaniwa sisi Wabunge humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sisi wote tumekula kiapo cha kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Ibara ya 146 inasema, "Madhumuni ya kuwapo kwa

Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi na vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki, kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapeleka madaraka karibu na wananchi. Kimsingi, natoa ushauri kwamba pendekezo lako la jambo hili kwenda kwenye Kamati na baadaye lirudi kwenye Bunge zima itakuwa jambo la maana ili tuje tushauriane, turudishe shughuli zote zilizoondoka kwenye Serikali za Mitaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Naam Mheshimiwa Spika. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane. Spika akishafanya maamuzi huwezi kuyahoji hapa ndani. Unaruhusiwa kuyahoji kwa kutumia Kanuni ya tano kwa kuandika kwa Katibu wa Bunge. Mimi nimefanya maamuzi ya kuileta hapa ndani, hoja itaamuliwa hapa ndani, haitaenda kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kunti unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu hata *TARURA* leo wanafanya kazi chini kule kwa wananchi wetu wakishirikiana na halmashauri hizo hizo. Kwa hiyo, ninachokisema hapa, hawa Maafisa Ugani na Maafisa Ushirika warudi kwenye Wizara ili tuipe fursa Wizara kufanya maamuzi ya kiuwajibikaji wanapokosea Maafisa Ushirika wetu kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani wakifanya makosa…

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Nyie tulieni jamani. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**SPIKA:** Sawa. Sasa nimempa sekunde 30, halafu inatakiwa kutoka taarifa hapo. Basi sekunde 15 kwa 15. Haya Mheshimiwa Kunti kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba yale maeneo yote muhimu kwa mfano utafiti, masuala ya mbegu, masuala ya umwagiliaji ambayo Waziri wa Kilimo anasimamia, mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampa taarifa kwamba anachokisema ni sawa. Tukifanya hivyo mambo yatakwenda vizuri zaidi kama ilivyo kwenye hizo sehemu nilizochangia. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya. Sasa inaonekana jamani macho yangu yaliona wapinga hoja, halafu wakubali hoja wote inaonekana sikuwaona. *(Kicheko)*

Haya Mheshimiwa Kunti unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa unyenyekevu mkubwa kwa maslahi mapana ya Taifa letu na wakulima wetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe hivi. Tunachohitaji hapa siyo nani anawahudumia akina nani? Sote sisi watumishi, sote sisi wawakilishi tunawatumikia Watanzania wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kujali utakuwa Wizarani ama bila kujali utakuwa wapi? Tunachotaka ni uwajibikaji na utumishi uliotukuka kwa Watanzania wenzetu.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja iliyoko Mezani mimi naiunga mkono, watumishi hawa; Maafisa Ugani na Maafisa Ushirika warudi Wizarani ili Wizara iweze

kuwasimamia watu wake vizuri na iweze kuleta tija, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, atafutatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kuruhusu hoja hii ijadiliwe na pengine fursa hii inaweza ikawa imetokea katika wakati ambao imechelewa kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kinachoelezwa hapa juu ya namna ambavyo ugatuzi umekuwa ukiathiri dhana ya *D by D* ni jambo ambalo limekuwa likiendelea kwamba tumeondoa barabara, tumeondoa maji na tunaendelea, na pengine tunafikiri utaratibu huo uendelee na mwisho wake itakuwa tumeondoa vitu vyote. Kwa hiyo, kwanza tutakuwa tunaenda kinyume na Katiba. Ibara ya nane ya Katiba inaweka msingi wa madaraka ya umma, madaraka kwa wananchi, lakini ibara ya 145 na ibara ya 146 zitakuwa zinakiukwa, kama Mheshimiwa Ole-Sendeka alivyosoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni tofauti sana miradi ya maji, ni tofauti sana miradi ya barabara na jambo linaloitwa ushirika. Ushirika ni zao la wajamaa. Ushirika ni jambo la wananchi wenyewe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, pamoja kwamba tunarejesha madaraka kwa wananchi, mbona hata kule kwenye Serikali za Mitaa kwenye vikundi vya 10% kama lengo ni kurudisha

madaraka kwa wananchi, kwa nini wale wanaiba pesa za wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunaomba jambo hili lirudi kwa Waziri mwenye dhamana ili aweze kuwasimamia Maafisa Ugani na Maafisa Ushirika ili kumsaidia mkulima wa nchi hii maana anateseka sana, na ndiyo huko tutakuwa tumemsaidia mwananchi, ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya mwanangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema hivi, kwa maneno machache, kwamba ushirika ni mali ya watu wenyewe. Yaani hata ushiriki wa Serikali ni kwa sehemu sana kwa sababu washirika wanakubaliana wao, wanapanga mambo yao wao. Ndiyo msingi. Huwezi ukauondoa ushirika kwa wananchi wenyewe. Kwa hiyo, mahali sahihi unapotakiwa kukaa ushirika ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya Serikali na Wizara za Kisekta ni ku-*facilitate,* ni kupeleka rasilimali kule chini. Kinachokosekana hata tukafikia hapa, ni kwamba Tume kwa mujibu wa Sheria hii tuliyoipitisha, Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, Tume wajitahidi kufika kule chini kupeleka fedha, kupeleka ujuzi, kupeleka wataalamu, wapeleke kule wataona matokeo yanaendelea, lakini siyo kunyang'anya uwa-*centralize* washirika ushirika huo uta…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kweli dhamira ya ushirika ni kupeleka tija na ni ushirika wa watu wenyewe kule chini, lakini kinachohitajika ni maendeleo yao kule chini. Maafisa Ugani pamoja na Maafisa Ushirika, iwapo hakutakuwa na mpango wa kuwaendeleza kitaaluma *(on job training)* kule halmashauri, hakuna, hakuna kitu chochote kinacholeta umuhimu wa kuwafanya wawe bora zaidi ili kuwahudumia wale watu wa chini; je, tunapelekaje tija kwenye jamii? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiuliza maswali kwenye taarifa ni kama unataka sasa aanze kujibu swali lako badala ya kuendelea na mchango wake.

Mheshimiwa Simbachawene, unaipokea taarifa hiyo? Ile sehemu ya taarifa ili usilazimike kujibu swali lake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni sehemu ya swali, nitamjibu tukitoka hapa, lakini kwa hapa nataka niendelee hivi... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba tutafute nchi zenye mfumo mzuri wa utawala na uongozi kama nchi yetu ni vigumu sana kuipata. Huu mfumo ambao tunauona una upungufu huu mdogo, umeifikisha nchi yetu hapa, na pengine hata sababu ya amani na utulivu wa nchi yetu unatokana na mfumo huu tulionao. Tuulee vizuri, tuutunze vizuri mfumo huu wa kuhakikisha kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaendelea kuwa na nguvu kama zilivyotakiwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendelea kutohoa na kuondoa nguvu zake kule tunadhoofisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sekta zetu zote zijiulize kabla ya kuamua kuchukua kitu chochote kutoka kule chini kama je, wametimiza wajibu wao sawa sawa?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Muda wake umekwisha Mheshimiwa Sophia.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wa Kilimo ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nitambue dhana iliyoibuliwa yenye dhamira ya kuchangamsha fikra za maamuzi mbalimbali katika Taifa letu na nikushukuru kwa kuridhi dhana hii kujadiliwa. Kama ambavyo kaka yangu aliyekaa muda huu amezungumza hapa. Nchi hii ni ya wananchi, msingi wa Serikali katika kuamua mambo yoyote ni lazima yaamuliwe na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Simbachawene amezungumzia Ibara ya 8 lakini ukienda Ibara ya 21 inazungumza misingi ya maamuzi mbalimbali ambayo inawashirikisha wananchi kupitia wawakilishi wa wananchi, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza hapa ni utekelezaji wa wajibu wa kila mmoja wetu. Hata ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge, malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge ni namna gani wale walioko kule chini wanashindwa kutekeleza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana ya ugatuzi wa madaraka huu ni msingi ambao wa Baba wa Taifa ameturithisha kabla ya kuondoka kwake. Imeingizwa kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 ambayo Mheshimiwa Sendeka ameizungumza hapa. Huko tunakoelekea leo pengine tuna miezi 11 twende kwenye chaguzi na pengine baada ya mwaka mmoja tuna Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza hivi leo, maeneo mengi ambayo yameondolewa kutoka TAMISEMI, kutoka kwenye Serikali

kule chini yanatuletea matatizo makubwa sana. Hasa ukiangalia kwa mfano tuna migogoro mingi sana ya ardhi eneo hili. Tumekwisha kaa tumezungumza na Waziri wa Ardhi tumekubaliana kwamba hili pia tulipitie na tuone uwezekano wa kuirudisha TAMISEMI. Leo hii… *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, leo hii…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante namuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Kimsingi sio tu kupoka madaraka kwa wananchi kinachokwenda kutokea ni *failure* ya hawa wanaopelekwa kwenye Wizara ya Kisekta, mfano mzuri Wizara ya Ardhi leo hii hatutatatua migogoro ya ardhi kamwe nchi hii kama hatujarejesha watumishi wa ardhi TAMISEMI, ahsante.

**SPIKA**: Sina uhakika nimesikia vizuri, umesema nchi hii hatutatatua?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi, naomba kurejea; nchi hii kama kuna kosa tulifanya ni kutwaa watumishi wa ardhi kutoka TAMISEMI kwenda Wizara ya Ardhi ambayo ni ya Kisekta.

**SPIKA**: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa hii kwa mikono miwili, ni makosa makubwa yalifanyika katika eneo hili na

tumekubaliana na Waziri wa Ardhi kwamba suala hili tunakwenda kulifanyia kazi ili hawa watu waje kwangu niwashughulikie vizuri. *(Makofi)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA**: Mheshimiwa Mchengerwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunti Majala.

**TAARIFA**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nataka nimpe mzungumzaji anyezungumza kwamba hawa maafisa ardhi walikuwa TAMISEMI tangu enzi hizo na migogoro ilikuwa imekithiri. Wakati huo kumbuka wewe ndiyo ulikuwa Wizara ni hiyo hiyo moja. Vijiji na vitongoji mnapanga ninyi lakini mkitoka hapo suala la ardhi wako kwako mkienda mnawaambia wananchi wamevamia na ninyi ndiyo mlikuwa mnapima mipaka. Kwa hiyo, hiyo haiwezekani kwamba hao watu kutolewa kupelekwa kwenye Wizara ya Kisekta eti mmepunguza migogoro. Hamjapunguza wala hamja… nakushukuru.

**SPIKA**: Mheshimiwa Mchengerwa unapokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakuomba unilindie muda, ni vema…

**SPIKA**: Mheshimiwa ngoja, muda wa taarifa ni sehemu ya muda wako kwa sababu anaboresha mchango wako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni vema Waheshimiwa Wabunge wakatofautisha masuala ya kiutawala na masuala ya kisera lazima tutofautishe. Lakini… *(Makofi)*

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, taarifa niko hapa.

**SPIKA**: **SPIKA**: Hii ni taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba siku zote chakula ili kinoge ni lazima kiwe na chumvi. Kilimo kiko kwa wananchi wa chini kabisa kwenye kitongoji utakapokiondoa kilimo kwa maana ya afisa ushirika ukamtoa pale kijijini kilimo kitakufa. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa mtoa taarifa kwamba maafisa ushirika wabaki katika eneo la halmashauri ili wasimamie vizuri kilimo chetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa Sekunde 30 kengele ya pili imeshagongwa, samahani kengele imeshagongwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa lakini jambo hili ni kubwa na niwaombe pamoja na dhana njema ya kulileta hapa Bungeni watuachie Serikali tukalijadili kwa kina na tutaangalia sehemu yenye mapungufu tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, juzi tulichukua maamuzi ya kuwaondoa baadhi ya watendaji kule Mbeya Mjini walioshiriki kwenye ubadhilifu fulani baada ya maamuzi kutolewa na madiwani lakini kama hao pia wangeenda kwenye sekta husika.

**SPIKA:** Hapo nakuongezea sekunde 30, Waheshimiwa Wabunge humu ndani si huwa tunazungumzia watu wanaofanya kazi vibaya na vizuri? Sasa kama Mkurugenzi wangu wa jiji anafanya kazi vizuri msifie kidogo Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na nia njema ya kuleta jambo hili. Tukumbuke kwamba tuna changuzi mbele yetu, siku chache

tuna chaguzi mbele yetu. Nawaomba sana mridhie jambo hili mliache kama lilivyo ili tuweze kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba tunawasimamia hawa vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba jambo la usimamizi lakini nichukue fursa hii kumpongeza mkurugenzi wa Jiji la Mbeya kwa kazi kubwa na kazi nzuri na niwaombe wakurugenzi wengine kwenye maeneo mbalimbali wachukue maamuzi kama haya itatusaidia sana Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba miradi yetu inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumuomba mtoa hoja aridhie jambo hili linbaki ndani ya Serikali na sisi tutakaa na Wizara ya Kilimo tuone ni namna gani tunaweza ku…

Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Muda wake umekwisha, Mheshimiwa Waziri weka nukta hapo. Muda umekwisha Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jumanne Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niseme kwamba nimetumika kwenye sekta ya TAMISEMI miaka 12 nimetumika Serikali Kuu miaka 18 na kote tuliona changamoto. Wakati niko miaka 18 kwenye Wizara ya Elimu tulibaini kwamba elimu inaweza ikasimamiwa kwa ufanisi kama kila kitu kitafanyika makao makuu lakini ilikuja kuthibitika vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadae tulifanya utafiti mdogo wakati ule Wizara ya Utumishi. Tulikuta mwalimu ameacha kazi miezi sita au zaidi Wizara haina habari inamlipa mshahara kwa sababu usimamizi wake ulikuwa unafanywa na Katibu Mkuu wa Wizara

wakati ule Dar es Salaam kwa shule zilizotapakaa nchi nzima lakini achia mbali utoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, haya maamuzi ya *D by D* nadhani Tanzania hayajaeleweka vizuri. Kama itakupendeza najitolea kuwa mwalimu katika kipindi kimoja tujielimishe *D by D* kule kulikofanikiwa walinya nini. Kwetu hapa tutazilaumu sana halmashauri lakini ule uwezeshaji haujafanyika ipasavyo. Nitoe elimu kidogo kwenye nchi zilizofanya vizuri sana kwenye ugatuaji wa madaraka kuna *principle* moja wanayoi-*apply* inasema *"The principle of subsidiarity*" maana yake pale ambapo shughuli zinafanyika…

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatokea wapi?

**MJUMBE FULANI:** Kwa Sophia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Sagini kuna taarifa kutoka kwa Sophia Hebron Mwakagenda.

**TAARIFA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwanza amesema kwamba amefanya kazi miaka 12 ya uzoefu na 18 ya uzoefu. Bado ni Waziri wa Serikali hii, kwa nini hajafanya hili suala? Kwa sababu mtoa hoja baada ya kuleta hiyo hoja yake ni baada ya mambo kutokwenda sawa. Kwa hiyo, nampa taarifa ni vema wakatengeneza kutumia uzoefu alionao na vitu ambavyo amevifanya ni labda itasaidia Taifa hili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jumanne Sagini unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu tu hana ufahamu na nilichofanya, nimefanya mengi sana kwenye sekta hii. Hata ukatibu mkuu pale miaka saba, minne ya unaibu na mitatu ya Ukatibu Mkuu nilifanya haya. Sasa nasema hivi *principle* ile inasema hivi, unaposimamia

jambo ambalo linafanyika pale ulipo, ufanisi wake unakuwa mkubwa zaidi kuliko ukisimamiwa kutoka mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tabia ya ubinadamu naomba niseme kwa Kingereza kwa sababu nimeitoa huko *normally people do what you inspect not what you expect*. Ukiwa makao makuu ya Wizara ukamsimamia mwananchi aliye kwenye kijiji ufanisi wake uko ndugu wapi ndugu zangu. *(Makofi)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kilichokosekana kwenye mfumo wetu wa ugatuaji…

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** …kilichopungua kwenye mfumo wetu wa ugatuaji ni nafasi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Sagini kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunti.

**TAARIFA**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, leo maafisa ushirika na maafisa ugani wako TAMISEMI na wako hapo kwenye miguu na ndiyo wanafanya vibaya kuliko kitu kingine chochote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sagini unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naipokea anakosa Subira tu, nilikuwa nataka nimwambie ni kwa nini tunaona huo udhaifu. Moja, baada ya uamuzi huu wa kupeleka madaraka karibu na wananchi, wizara za sekta na watendaji kwenye *local government* walipaswa wafanye *realignment* moja kwenye *attitude* na *perception* kwa sababu wizara hizi zilizoea kutekeleza. Leo ukiwaambia washiriki kwenye sera wafanye *M and E, mentoring and evaluation* wafanye *capacity development* ya watu kule hayo hayafanyiki. Peleka *resources,* peleka vifaa… *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kengele imeshagongwa Mheshimiwa Sagini ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe Waziri wa Kilimo na mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, cha kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi na nianze kwa kusema mambo mawili makubwa. Changamoto ambazo mtoa hoja amezitaja ni changamoto ambazo zipo lakini changamoto hizi msingi wake ni changamoto zinazotokana na *administration* ni suala la utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana ya *D by D* Wizara ya Kilimo haina mkulima Wizarani. Mkulima yuko wilayani na kule wilayani aliko anatakiwa asimamiwe na Afisa Ugani aliyeko wilayani. Kama Wizara na Bunge lako tukufu lilitielekeza hapa kwamba tulete mabadiliko ya sheria ya ushirika ambayo tunaifanyia kazi ili tuweze kutatua changamoto zilizopo kwa sababu hoja siyo kwamba nani amsimamie nani? Hoja iliyoko ni kwamba afisa kilimo aliyeko katika ngazi ya halmashauri atimize wajibu wake na kufanya kazi inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi sasa hivi kama Wizara tukishirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tunapitia Sheria ya Tume ya Ushirika ambayo itayapitia mapungufu yote ya kiutawala yaliyoko na ya usimamizi katika sekta ya ushirika. Vilevile, tunapitia upya Sheria ya Tume ya Umwagiliaji ambayo inatupa mamlaka ya kwenda kuanzisha ofisi za umwagiliaji katika ngazi ya wilaya na kuweza kuwasimamia maafisa kilimo walioko katika ngazi ya wilaya na vijiji bila kuathiri *D by D. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge watupe nafasi wasubiiri tulete mabadiliko ya sheria hizo halafu tutatoa ushauri kutokana na jambo…*(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani anataka kutoa taarifa? Sawa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji amechangia vizuri. Shida iliyopo ukienda kwenye kata zetu kama mtendaji kata hayupo hachukuliwi mwalimu mkuu akawe mtendaji wa kata wala hachukuliwi mganga mkuu akawe mtendaji wa kata anachukuliwa afisa kilimo ndiyo anaenda kukaimu mtendaji kata kwa maana wanaonekana kwamba maafisa kilimo wa kata hawana shughuli. Halafu hoja nyingine inakuja wanasema hawa maafisa kilimo…

**SPIKA:** Mheshimiwa taarifa huwa ni moja tu Mheshimiwa. Mheshimiwa Bashe unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake ni suala la utawala tu ni suala la usiamamizi, ni suala la maafisa kilimo kutokusimamiwa na kutokufanya kazi na ni suala la maafisa kilimo kutokuwezeshwa. Kwa hiyo, ninachotaka ni-*appeal* kwa mtoa hoja na ni-*appeal* kwa Waheshimiwa Wabunge kama Waziri wa Kilimo ninaesimamia sera na masuala ya uratibu wa shughuli za kilimo ninatambua changamoto zilizoko katika ngazi ya halmashauri, ninatambua matamanio ya Waheshimiwa Wabunge na ninatambua matamanio ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge mtuache tumalizie kazi tunayoifanya ndani ya Serikali ili kutatua changamoto zilizoko zinazowakabili maafisa ugani na zinazokabili suala la ushirika ambazo… *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** na maafisa ushirika ambazo zitatuliwa… nimalizie, ambazo zitatuliwa tutakapoleta mabadiliko ya sheria ya Tume ya Ushirika…

**SPIKA:** Haya ahsante sana kuna taarifa…

**WAZIRI WA KILIMO:** lakini tutakapoleta mabadiliko ya sheria ya Tume ya Umwagiliaji bila kuathiri…

**SPIKA:** Kuna taarifa Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Ole-Sendeka

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa niungane na mawazo mazuri sana ya Mheshimiwa Bashe. Naunga mkono hoja ya kutungwa kwa sheria inayowadhibiti hawa maafisa wa ushirika. Mheshimiwa Bashe ni shahidi alipokuja Njombe alikuta ufisadi wa vyama vya ushirika na tukalazimika kuwakamata wale waliohusika ambvapo baadae tulikusanya shilingi bilioni 5.5 kutoka kwa mafisadi wa vyama vya ushirika na *SACCOS.* Sheria ilikuwa vibaya tulipokuwa tunaomba ushauri wanasheria. Kwa hiyo, sheria ibadilishwe bila kuathiri *D by D*.

**SPIKA:** Haya huyu nadhani yeye hajatoa taarifa ameunga mkono unachosema na kengele imeshagongwa, sekunde 30 malizia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kumuomba mtoa hoja kama Serikali tunafahamu tatizo linalokabili Sekta ya Ushirika na tunafahamu tatizo linalokabili Sekta ya Ugani. Watupe nafasi tumalizie michakato hii ya kisheria ambayo itaenda kutatua masuala ya utawala na ugatuaji lakini vilevile itatatua tatizo la upelekaji wa rasilimali na usimamizi wa maafisa ugani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, sawa sasa nafikiri Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mnafatilia mchango wa Mheshimiwa Waziri nilikusudia kusema mwisho akiwa amemaliza. Hapo mwisho

nadhani jambo amelisema vizuri mwanzoni alisema mtuache Serikali tufanye hivi. Sasa Bunge haliwezi kuwaacha Serikali mfanye lakini mwishoni amesema tuwape muda kwa hiyo nafikiri hoja yake imeeleweka. Mtoa hoja Mheshimiwa George Mwenisongole uje uhitimishe hoja yako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yangu. Moja ya urithi alioniachia marehemu baba yangu Askofu Mwenisongole alioniachia ni kusema ukweli hata kama huo ukweli unakuathiri. Leo hii tunaweza tukajibu hoja hii kwa ushabiki na tunaweza tukatoa hii hoja kama hatuoni tatizo lakini ukweli utabaki kama ukweli tuna matatizo makubwa ya ushirika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa ni ndogo, anayetoa maono, sera na mipango ni Wizara ya Kilimo lakini yule afisa wa chini ambaye anapaswa kutekeleza maono, mipango na yote yuko chini ya TAMISEMI. Iwapo mipango hiyo itaenda vyovyote Waziri wa Kilimo hana uwezo wa kumhoji au kumuwajibisha na mifano iko wazi kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu Afisa Ushirika alikamatwa anapora kwa bastola, lakini mpaka leo yupo kazini kwa sababu tu TAMISEMI wameshindwa kumshughulikia, licha ya Tume ya Ushirika kusema huyu mtu hatufai. Tukija Mbozi ni madudu matupu pale ushirika, ukienda Mbinga hivyo hivyo, Mwanza kila mahali na hatuoni huko TAMISEMI kuwachukulia hatua ndiyo maana tukaomba kwamba hawa Maafisa Ushirika warudi Wizarani ambayo inajua taaluma zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa ni hiyo, siyo kwamba tulitaka kuharibu *D by D* bali tulitaka kuiimarisha kuwafanya hawa Maafisa Ushirika wawajibike kwa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, wakati anahitimisha Bajeti, Waziri wa Kilimo alitoa agizo hapa Bungeni kuwazuia Vyama vya Msingi kukopa. Kwa masikitiko, Vyama vya Msingi bado vinachukua mikopo na Maafisa Ushirika wanawasainia hiyo mikopo na hiyo mikopo haiendi kwa washirika

badala yake viongozi wa ushirika wanakula kwa kushirikiana na washirika na Mheshimiwa Bashe hana uwezo wa kuchukua hatua kwa sababu wale wako TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo uende kwa Mheshimiwa Mchengerwa uanze kumwambia habari za ushirika, haelewi kitu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, anayejua hayo ni Mheshimiwa Bashe. Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa hapo, kuwaomba hawa Maafisa Ushirika wawe chini ya Wizara ya Kilimo hata tunapozungumza Bajeti ya Kilimo tunajua hawa watu tumekukabidhi, Maafisa Kilimo, Maafisa Ushirika ambao unawasimamia. Hata hivyo, namshukuru Waziri kwamba ametambua changamoto na ametuomba tumpe muda aje na hiyo Sheria. Kwa hiyo usiku wa deni hauchelewi kuisha, sisi wakati wa Bajeti tutamkamata, ametuomba muda na mimi kama mtoa hoja nipo tayari kutoa muda kwa Serikali kulichakata hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote tunajenga nyumba moja na wote tunataka mkulima wetu afaidike na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hoja gani?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, namalizia, naomba kutoa hoja kukubaliana na maombi ya Serikali kwamba tuipe muda itimize wajibu wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja kwanza, Waheshimiwa Wabunge. Subirini kwanza Waheshimiwa…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja iliyoko mezani, kwa sababu ni lazima Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa. Hoja iliyoko Mezani na ambayo iko mbele ya Bunge ni Hoja ya Kuwahamishia Maafisa Ushirika katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa Ugani chini ya Wizara ya Kilimo. Hiyo ndiyo hoja iliyoko mbele ya Bunge. Kama Mbunge nataka nikuongoze vizuri ili ujue ni hoja gani unaitoa.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Ukisema unatoa hoja na ulikuwa unasema unaungana na Mheshimiwa Bashe hiyo kutoa ina sura mbili. Moja, unaiondoa hii hoja yako?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** Ama unaitoa, yaani umebadilisha hii hoja yako tuichukue ile hoja ya Serikali ndiyo tuiweke, ndiyo unayotaka Bunge lihojiwe kwa hiyo. Kwa sababu kama unaiondoa hoja maana yake Bunge hatutalihoji. Kama hoja yako bado ipo hii ndiyo tuliyonayo hapa mezani…

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo hiyo ipo.

**SPIKA:** Kama unaibadilisha ndiyo useme sasa umebadilisha hii hoja kwa sababu…

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo kwa sababu mambo haya kama halijawahi kutokea siyo jambo rahisi sana kujua ule utaratibu. Sasa kama hoja yako hii unairekebisha ili uchukuliane na ile hoja iliyotoa Serikali ya kwenda kutengeneza sheria maana yake hapa hii ya kwako unaiondoa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge hoja hii itakuwa ni ile pale, yaani ni ya kwako bado lakini umeibadilisha kwamba Serikali sasa ika…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, nadhani Mheshimiwa Mbunge umenielewa ili ujue ninapoitoa kwa Wabunge kuwahoji ili hoja hii ifungwe, nataka nijue niwahoji hoja ipi? Hii uliyoleta mwanzo ama iliyorekebishwa na Serikali ambayo bado itakuwa ni ya kwako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hoja yangu ni hii, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Kilimo amesema kwamba wanaandaa Sheria kwa kushirikiana na TAMISEMI kuweka mazingira mazuri ya kuwasimamia hawa Maaafisa Ushirika na hii ndiyo ilikuwa ndiyo lengo la msingi la hoja yangu kwamba hawa Maafisa Ushirika wawajibike rasmi kule chini. Kwa maana hiyo ni kwamba nipo tayari kuipa muda Serikali, hoja yangu ni hiyo, kukubaliana na hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nitakapowahoji Mheshimiwa mtoa hoja ameirekebisha hoja yake ya mwanzo. Badala ya kuwa hoja ya kuwahamishia Maafisa Ushirika katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Maafisa Ugani chini ya Wizara ya Kilimo, sasa hoja yake pamoja na kwamba maelezo ni haya haya, hoja yake iliyoko mezani ambayo inaletwa Bunge liamue ni hoja inayohusu Serikali kutunga Sheria ili kuleta ufanisi kwenye utendaji kazi wa Maafisa Ushirika. Ndiyo hoja itakayotolewa kwenu. Sasa Mheshimiwa Mbunge baada ya kusema hayo sema unatoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa George Mwenisongole imeungwa mkono. Unaweza kurejea kuketi Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji Wabunge kuhusu hoja iliyorekebishwa ya Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa sababu marekebisho yale yamefanywa kwa kuangalia maelezo yako uliyoyatoa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na mimi ili nisichanganye maneno mtaenda mtazame kwenye *Hansard* hoja iliyorekebishwa kwa kadri nilivyoisema hapa. Ndiyo maamuzi ya Bunge kuhusu hoja hii halafu nyinyi mtaenda kuifanyia kazi kwa kadri Bunge lilivyofanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba yetu punde, lakini nina tangazo hapa linalotoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania Mheshimiwa Zainab Katimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ameniletea mimi taarifa ambayo naileta kwenu. Wabunge vijana ambao wana umoja humu ndani na wako zaidi ya 70 na wana umri wa chini ya miaka 45 walikutana jana na kufanya uchaguzi wa viongozi wa kudumu wa umoja huo kwa nafasi za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina na Wajumbe.

Waheshimiwa Wabunge matokeo ya uchaguzi huo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Zainab Katimba alichaguliwa kuwa Mwenyekiti; Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan alichaguliwa kuwa Katibu na Mheshimiwa Alfred Kimea alichaguliwa kuwa Mweka Hazina. *(Makofi)*

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji; Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya alichaguliwa kuwa Mjumbe; Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali alichaguliwa kuwa Mjumbe na Mheshimiwa Maryam Omar Said alichaguliwa kuwa Mjumbe. *(Makofi)*

Kamati ya Umoja wa Wabunge Vijana tunawapongeza kwa uchaguzi huo na pia tunawapongeza kwa kubadilisha jambo ambalo pengine huwa linaonekana ni utaratibu kwamba mwanamke ndiyo anakuwa Katibu. Safari hii Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ni wanawake na Katibu ni mwanaume, hongereni sana. *(Makofi)*

Haya Waheshimiwa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge Waheshimiwa.

## TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge zimemalizika.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Hoja ya Kuahirisha Bunge, sasa namuita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aje atoe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuhitimisha

shughuli zote za Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyopangwa. Hivyo basi, tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atupe hekima na nguvu ya kuweza kutekeleza Maazimio yote yaliyopitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada za kutekeleza dhamira yake ya dhati ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. Sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa uongozi wake makini na busara alizonazo zinaendelea kuchagiza maendeleo ya haraka ya uchumi wa nchi yetu pamoja na ustawi wa Mtanzania mmoja mmoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Nawasihi Watanzania wote tuendelee kumuunga mkono ili aweze kutimiza dhamira yake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutelekeza majukumu yake ya kuwatumikia Watanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa jitihada anazozifanya, ama kwa hakika busara zake zimekuwa chachu katika kuleta maendeleo ya haraka ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote natumia nafasi hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge ya Dunia *(IPU)* katika Kikao cha Baraza la Uongozi kilichofanyika tarehe 23 hadi 27 Oktoba huko Luanda, nchini Angola.

Vilevile nakupongeza sana kwa kuwa Rais wa Tatu mwanamke kushika nafasi hiyo ambayo imeshawahi kushikwa na Mheshimiwa Najma Heptulla kutoka India kati ya mwaka 1999 hadi mwaka 2002 na Mheshimiwa Gabriela Cuevas kutoka Mexico aliyeongoza kipindi cha mwaka 2017 mpaka mwaka 2020. Kipekee nakupongeza sana kwa kuwa Rais wa kwanza Mwanamke kutoka Afrika kuchaguliwa kushika nafasi hiyo kubwa ya Rais wa Mabunge Duniani.

Mheshimiwa Spika, narudia kukupongeza sana kwa ushindi huo ambao kwa hakika umetuletea heshima kubwa sana Watanzania kwani umeithibitishia dunia nzima kuwa Watanzania tunao uwezo mkubwa wa uongozi na tunaaminika sana. Natumia fursa hii kukutakia kila la heri Mheshimiwa Spika katika kutekeleza majukumu yako na niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote tuendelee kumwombea heri Mheshimiwa Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kukushukuru na kukupongeza sana kuendelea kuliongoza vema Bunge hili tukufu na kusimamia vema mijadala yote iliyoendeshwa katika Mkutano huu wa 13 tutakaouhitimisha hivi punde. Mwenye macho haambiwi tazama, hekima, ukomavu na weledi wako umeendelea kuongezeka siku hadi siku. Hongera sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. Ushindi huo wa kishindo ni kielelezo tosha kuwa wananchi wa Jimbo la Mbarali, bado wana imani kubwa kwako wewe Mheshimiwa Ndingo, kwa Chama chako Cha Mapinduzi na kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninampongeza sana Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi. Natumia fursa hii kukukaribisha sana na kwa upande wetu, sisi Wabunge tunakukaribisha pia na tunakuhakikishia kuwa tutakupa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yako ya kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa mliyoifanya. Mmeshiriki kikamilifu kutoka Kamati, mijadala ambapo hoja mbalimbali ziliwasilishwa wakati wa Mkutano huu. Michango yenu ni muhimu sana katika kuimarisha ustawi na huduma kwa Watanzania. Hivyo basi, nawahakikishia kuwa Serikali imepokea michango yote, maoni pamoja na ushauri wenu ambao kimsingi umekuwa ukisaidia sana katika kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Septemba hadi Novemba, 2023, wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali yakiwemo ajali za barabarani, moto na mengine yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Kwa masikitiko makubwa natoa salamu nyingi za pole kwa wahanga wote wa majanga hayo. Aidha, natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao kutokana na masahibu hayo. Kwa wale majeruhi tuzidi kuwaombea uponyaji wa haraka na kwa marehemu tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu ili azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge, Mkutano huu wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu, ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka kwa Kamati za Kudumu za Bunge, maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Serikali sambamba na kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali 154 ya msingi na mengine 452 ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika, maswali manne ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu baada ya kuwa ametoa taarifa kuhusu Kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepokea Miswada nane ya Sheria kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023];*

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 *[The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023];*

(iii) Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2023;

(iv) Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2023;*

(vi) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023;

(vii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Affairs Laws (Ammendment) Bill, 2023;* na

(viii) Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, tunapowasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Miswada hii mitatu ya mwisho; Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, leo hii natumia nafasi hii kuwashukuru sana wadau wa demokrasia na Viongozi wa Vyama vyetu vya Siasa hapa nchini ambao wapo kwenye jukwaa letu hapa leo kama walivyotambulishwa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walitambulishwa kwa sababu wameungana nasi katika kushuhudia tendo la uwasilishwaji wa

Miswada hii ya Sheria mitatu ambayo inapelekea kuwa na mwelekeo mpya wa kuendesha siasa za ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya kuimarisha demokrasia nchini, leo tunashuhudia Viongozi wetu wa Vyama vya Siasa wakipigania maendeleo ya nchi yetu huku wakisimamia Sera zao zinazoleta maendeleo ya pamoja. Tunawashukuru sana viongozi wetu wa vyama vya siasa kwa umoja wenu, kwa kuja Bungeni kushuhudia tendo hili ambalo limewasilisha Muswada hii kwa mara ya kwanza. Tutaendelea kutekeleza dhana ya *4R* hatua kwa hatua ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Nawashukuru sana kwa kututembelea kuja hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 na 107 hadi 112 za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali, Bunge lako Tukufu limepokea, kujadili na kupitisha Maazimio mawili kama ifuatavyo:-

(i) Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023;

(ii) Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kufunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu la mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Maazimio haya yamepokelewa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge kwa ustadi wa hali ya juu huku wakionesha nia njema ya kujenga mustakabali mwema wa Taifa letu. Kwa dhati nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kukubali kuridhia kupitisha Maazimio haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa za Serikali Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa Kumi na Tatu lilipokea Taarifa ya Serikali kuhusu Kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Tolea la 2023 na Mitaala ya Elimu ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu

niliyoitoa mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya Tarehe 03 Novemba, mwaka huu 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya Kamati ya *PAC* na *LAAC* kuhusu hesabu zilizokaguliwa na *CAG* kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na taarifa ya Kamati ya *PIC* kuhusu Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mkutano huu wa 13 wa Bunge lako ulipata nafasi pia ya kupokea na kujadili kwa kina taarifa za Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambao umeishia Tarehe 30 Juni, 2022. Taarifa hizi za Kamati zinatokana na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Kamati hizi tatu zimechambua kwa kina hoja mbalimbali za ukaguzi zinazohusu matumizi ya fedha za umma kwa hesabu za Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma pamoja na Mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Uliofanywa na Taasisi za Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioiishia tarehe 30 Juni, 2022. Jumla ya Maazimio 117 yaliyotokana na hoja 14 yameweza kutolewa na Bunge, ambayo kimsingi ni maelekezo mahsusi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia kutoa pongezi za dhati kwa Ndugu Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuendelea kuwa Taasisi yenye kuaminika inayotoa Huduma za Ukaguzi kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa. Nyote ni mashahidi kwamba, Ofisi hii imendelea kujipambanua kwa namna inavyojenga, inavyokuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi yake ndani ya Serikali, kama inavyoidhinishwa na Bunge katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweza kuwahakikishia Watanzania na jamii yote namna ambavyo nchi yetu inavyoweza kupata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za umma na namna ambavyo mali za umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Maafisa Masuuli pamoja na Watendaji wote wa Serikali kwa namna ambavyo wameweza siyo tu kujibu hoja za ukaguzi ambazo zilibainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini pia kuweza kutekeleza takwa la Kikatiba la kufika mbele ya Kamati husika za Bunge kwa ajili ya ufafanuzi wa kina. Aidha, natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Mawaziri kwa michango yao katika kutoa majibu ya Serikali kwa baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Ni ukweli ulio bayana kwamba hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi, muhimu na zote zinahitaji majibu na utekelezaji wa haraka. Nasema tu kuwa Serikali yenu ni sikivu na itatekeleza mapendekezo hayo kwa kutoa majibu sahihi na utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na majibu yaliyotolewa na Serikali, mturuhusu tufanyie kazi masuala yote yanayohitaji mabadiliko ya kisera na kisheria. Mabadiliko haya yote tutalishirikisha kikamilifu Bunge hili ili kutimiza ndoto na malengo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali baada ya kupokea hoja na Maazimio yote, tayari imeandaa Bangokitita ambalo linaainisha jukumu la kila Wizara kwa ajili ya kufanyia kazi maelekezo ya Bunge hili ili kurahisisha uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji kwa Waheshimiwa Wabunge rejea yao. Hivyo basi, ninaziagiza Wizara zote ziandae kwa wakati Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio yote kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa upande wake, itaandaa taarifa ya Serikali ambayo itawasilishwa kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Pamoja na hoja za Kamati za Bunge zilizopokelewa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, Serikali iliwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Maandalizi

ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ambapo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuchangia hoja hii moja kwa moja na kwa maandishi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao katika Mpango huu pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mipango ya maendeleo ya kila mwaka ni nyenzo muhimu ya matumizi bora ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Mipango hii huhakikisha malengo ya Dira 2025 yanafuatiliwa na kusimamiwa kila mwaka ili kuweza kukuza uchumi na kuondoa umaskini hapa nchini. Mapendekezo ya Mpango yameainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa kuzingatia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika mwaka 2024/2025 msisitizo utawekwa katika kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi, kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na maendeleo. Vilevile, msisitizo utawekwa katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika maandalizi na utekelezaji wa mipango, uwekezaji na uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imewasilisha Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/2025. Mwongozo huu kimsingi ni maelekezo ya jumla na maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli katika hatua zote za uandaaji, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu umejikita katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mpango wake wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano, ule ulioanza Mwaka 2021/2022 na kufikia mwaka 2025/2026 ambavyo ni pamoja na kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao kwenye hoja hizi mbili ambazo kwa pamoja zinatoa mwelekeo wa wapi nchi yetu inataka kufika kwa kuangalia kule tulikotoka. Hivyo, natoa rai kwa Maafisa Masuuli na watendaji wote wa Serikali kutafsiri kwa vitendo na kwa umakini mkubwa maelekezo yote yaliyotolewa na Bunge hili ikiwa ni sehemu ya kutimiza ndoto za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Masuala ya Utabiri wa Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa, mvua zimeanza kunyesha katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Tayari Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeshatoa utabiri wa mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli kwa kipindi cha Mwezi Oktoba hadi Desemba, mwaka huu 2023. Utabiri huo umebainisha uwepo wa hali ya *El Nino* ambayo itaambatana na mvua kubwa na kusababisha mafuriko ambayo yanaweza kuleta athari mbalimbali zikiwemo madhara ya kiafya, kiuchumi, kijamii, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utabiri wa hali ya hewa inaonyesha mvua hizo zitakuwa juu ya wastani katika maeneo mengi ya Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Kusini mwa Mkoa wa Simiyu, Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikiwemo visiwa vya Mafia) na Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro. Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kuzuia na kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na uwepo wa *El Nino* sambamba na kujiandaa kukabiliana na mvua hizo kubwa. Kwa msingi huo, natumia fursa hii kuzielekeza Wizara, Mikoa na Taasisi za Serikali kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kuainisha na kuandaa rasilimali za kujiandaa, kuzuia na kukabiliana na maafa endapo yatatokea;

(ii) Kuelimisha na kuhimiza wananchi kuhama kwenye maeneo hatarishi na kuchukua tahadhari ili kuokoa maisha na mali;

(iii) Idara na Taasisi zinazohusika na mazingira na miundombinu zihakikishe barabara zinapitika wakati wote, mitaro na makalvati yanazibuliwa, yanaimarishwa na kusafishwa ili kuruhu maji yapite kwa urahisi;

(iv) Sekta za maji, umeme na mawasiliano ziweke mipango ya kuzuia madhara na kuhakikisha uharibifu katika huduma hizo unapewa ufumbuzi mapema;

(v) Kushirikisha wadau wa maafa ikiwemo wananchi wenyewe, taasisi za umma na sekta binafsi katika mipango yote ya usimamizi wa maafa;

(vi) Kutoa taarifa haraka kwa mamlaka husika inapotokea maafa katika sekta husika;

(vii) Kamati zote za Maafa katika ngazi ya Kijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa zianze kujipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto za *El Nino* endapo zitajitokeza kwenye maeneo yetu;

(viii) Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri ziandae mipango ya utekelezaji katika maeneo yao kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya *El Nino*.

Mheshimiwa Spika, nawasihi wananchi wote kujenga utamaduni wa kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na Viongozi na Mamlaka ya Hali ya Hewa ikiwemo kuhama kwenye maeneo hatarishi na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo salama. Kwa upande mwingine, wananchi waendelee kuweka akiba ya chakula na kutumia mvua hizi nyingi kulima mazao yanayostawi katika mazingira ya maji hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la Ukusanyaji Wa Mapato. Uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ikiwemo kuwezesha uwekezaji wa kimkakati katika sekta za uzalishaji, huduma za jamii na miundombinu. Ukuaji huo wa uchumi

umechangia kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta rasmi na isiyo rasmi na hivyo kuiwezesha Serikali kukusanya mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024, mapato kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje yalifikia shilingi trilioni 9.06, sawa na asilimia 89.6 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi trilioni 6.94 sawa na asilimia 96.2 ya lengo la kipindi hicho. Mapato ya ndani yanajumuisha shilingi trilioni 6.15 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi bilioni 491 za mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi na shilingi bilioni 299 kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa mapato kunatokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, ikiwemo kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kurahisisha ulipaji wa kodi. Katika hatua nyingine, kuimarika kwa mapato kumewezesha Serikali kuendelea kuwahudumia wananchi kupitia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa hospitali na vituo vya afya na Sekta ya Elimu vilevile.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mapato hayo yamewezesha ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, uboreshaji wa miundombinu ya barabara na reli, mpango wa Elimumsingi na Sekondari bila ada, kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania, usambazaji umeme vijijini na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa malengo ya makusanyo na utekelezaji wa bajeti kwa ujumla yanafikiwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato, kuimarisha doria maeneo ya mipakani, kutoa elimu kwa walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari, kuhimiza matumizi ya stakabadhi za kielektroniki za *EFD* na kuendelea kuboresha mazingira ya kuvutia uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo inalenga kuhakikisha taasisi zenye sura za utoaji wa huduma kwa pamoja zinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kuwezesha kutoa namba ya malipo jumuishi ili

kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji kodi na kuendelea kusimamia na kutekeleza kikamilifu sera za bajeti na fedha.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuondoa mianya ya uvujaji wa mapato. Aidha, mamlaka hizo ziimarishe ushirikiano na taasisi nyingine za umma kwenye ukusanyaji wa mapato ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nawashukuru wananchi kwa kushirikiana na Serikali katika ukusanyaji wa mapato ambayo ndiyo msingi wetu wa maendeleo yetu. Vilevile, nawapongeza kwa dhati watumishi wa taasisi zenye dhamana na ukusanyaji wa mapato zikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufanikisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Aidha, nawasihi watumishi wote waliopewa dhamana hiyo kutekeleza jukumu hilo kwa uadilifu na kuendelea kutoa elimu ya mlipakodi ili kufanikisha ulipaji wa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Usimamizi wa Sekta ya Elimu hasa Elimumsingi. Sote tunafahamu kuwa mojawapo ya malengo ya elimu nchini Tanzania ni kutoa elimu bora itakayowajengea uwezo wahitimu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Hatua hiyo itawezesha Taifa letu kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Serikali katika kutekeleza azma hiyo, imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu, kutekeleza Mpango wa Elimumsingi na Kidato cha Tano na Sita bila ada, kuongeza ajira za walimu na wakufunzi wenye sifa, kutoa ufadhili na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na maboresho ya sera na mitaala yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia uandikishaji wa wanafunzi kuanzia ngazi ya elimu ya awali bila kusahau watoto wenye mahitaji maalum, ambapo zoezi ambalo huanza mwezi Oktoba kila mwaka. Kwa mwaka 2024, Serikali inatarajia kuandikisha watoto wa Elimu ya Awali 1,877,484 wenye rika lengwa wakiwemo wavulana 934,560 na wasichana 942,924

na Darasa la Kwanza watoto 1,729,180 wakiwemo wavulana 860,870 na wasichana 868,310.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya watoto wa elimu ya awali 407,138 sawa na asilimia 21.7 wakiwemo wavulana 201,244 na wasichana 206,253 wamekwishaandikishwa. Kati ya watoto wa elimu ya awali walioandikishwa, watoto wenye mahitaji maalum ni 960, kati yao wavulana ni 488 na wasichana ni 472.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaotarajia kujiunga darasa la kwanza walioandikishwa ni 593,452 sawa na asilimia 34.3 wakiwemo wavulana 293,728 na wasichana 299,724. Kati ya wanafunzi wa darasa la kwanza walioandikishwa, wenye mahitaji maalum ni 1,365 wakiwemo wavulana 733 na wasichana 632.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa yote nchini kusimamia zoezi la uandikishaji katika maeneo yao ambalo itakuwa vema likihitimishwa Tarehe 30 Desemba, 2023 ili kuwezesha watoto hao wenye rika hiyo ya kuandikishwa shule waweze kuanza endapo wakati wa masomo utakapofika Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa wadau wote wa maendeleo zikiwemo Taasisi za Kidini na Taasisi za Kiraia kushiriki katika kutoa hamasa kwa Watanzania nchi nzima ili watoto wote wenye rika lengwa waweze kuanza masomo mwezi Januari, 2024. Jitihada hizo zinaendelea sambamba na kukamilisha maandalizi yote muhimu ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2024 ikiwemo ujenzi wa miundombinu. Jumla ya wanafunzi 1,206,995 sawa na asilimia 86 waliofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2023 wanatarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari Januari, 2024.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote nchini wahakikishe kuwa ujenzi wa miundombinu yote katika Shule za Sekondari unakamilika kabla ya tarehe 30 Novemba, 2023. Serikali itachukua hatua kali kwa wote watakaoshindwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika Shule za Sekondari. Wakuu wa Mikoa fanyeni ufuatiliaji, Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya

ujenzi katika Halmashauri zote nchini, hivyo hakuna sababu wala visingizio vya kutokamilisha ujenzi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikopo ya Elimu ya Juu, Serikali inaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya kati na ya juu kwa kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata mikopo ya wanafunzi. Katika mwaka wa masomo 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 786 kwa ajili ya mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vya kati. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 731.3 zitatolewa kama mikopo kwa wanafunzi 220,376 wa shahada mbalimbali; shilingi bilioni 6.7 kwa wanafunzi 1,200 wanaofadhiliwa kwa mpango wa *Samia Scholarship*; na shilingi bilioni 48 kwa wanafunzi wa stashahada zenye uhitaji mkubwa wa rasilimali watu nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza wigo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi ambapo katika mwaka wa masomo 2023/2024 utoaji wa mikopo umehusisha wanafunzi wa stashahada. Dirisha la kupokea maombi ya mkopo kwa wanafunzi wa stashahada lilifunguliwa tarehe 7 Oktoba, 2023 na kufungwa tarehe 29 Oktoba, 2023. Hadi dirisha linafungwa jumla ya waombaji 12,910 walikuwa wamewasilisha maombi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande shahada, hadi tarehe 5 Novemba, 2023 jumla ya wanafunzi 169,180 sawa na asilimia 77 ya lengo walikuwa wamepangiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 555.8. Kati yao, wanafunzi 73,078 ni wapya wa shahada za kwanza na wengine 96,102 ni wanufaika wanaoendelea na masomo ambao matokeo yao ya ufaulu wa mitihani na kuendelea na masomo yamepokelewa na Bodi ya Mikopo. Nitumie nafasi hii kuiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi ya Teknolojia kusimamia kikamilifu zoezi la utoaji wa mikopo na kuhakikisha kuwa zoezi hilo linakamilika kwa wakati sambamba na kushughulikia kwa wakati changamoto za utoaji wa mikopo kwa wanafunzi pale zinapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa fedha nyingi kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu, bado kuna baadhi ya waajiri na wanufaika wa mikopo ambao hawatimizi wajibu wao wa kurejesha fedha waliokopeshwa ili

mfuko uweze kusomesha vijana wengine zaidi. Hivyo basi, nitoe wito kwa waajiri na wanufaika wote kutimiza wajibu wao wa kisheria wa kurejesha mikopo hiyo kwa hiyari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara. Serikali yetu imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuimarisha na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Sote tumeshuhudia mabadiliko ndani ya Serikali yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais, kwa kuanzisha Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ili kuimarisha uratibu na kuongeza imani zaidi kwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuimarisha uwekezaji nchini, naomba nitumie nafasi hii kusisitiza masuala yafuatayo: Moja, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kupitia Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC)* kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *NIDA*, *BRELA*, *TRA*, Idara ya Kazi, Idara ya Uhamiaji, *NEMC*, *TANESCO*, *TBS*, *OSHA* na *TMDA*, iboreshe mwongozo wa uwekezaji ili kubainisha fursa kulingana na mazingira ya sasa na kuzingatia taratibu za kuwatambua na kuwasajili wanaotaka kuwekeza hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC)* kiimarishe matumizi ya TEHAMA ili kutangaza fursa nyingi za uwekezaji zilizopo nchini na kuwawezesha wawekezaji kutumia *TIC* kama kiungo cha kupata taarifa muhimu kutoka kwenye taasisi za Serikali hapa nchini; na tatu, *TIC* yenyewe ihakikishe kuwa mwongozo wa uwekezaji unapatikana kwa urahisi kwa wawekezaji wa ndani na wale walioko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Masuala ya Maendeleo ya Vijana. Serikali inaendelea kuratibu shughuli za Maendeleo ya vijana sambamba na kuandaa mfumo wa kitaifa wa uratibu wa afua zinazotekelezwa na wadau mbalimbali. Mfumo huo utasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati na kuwawezesha vijana kutumia fursa zilizopo kujikwamua kiuchumi. Aidha, Serikali kupitia Programu ya Ukuzaji Ujuzi imetoa mafunzo kwa vijana 121,898. Katika kipindi cha 2017 hadi 2023 vijana 91,106 wamepata ujuzi kwa njia ya uanagenzi. Vilevile vijana 22,296 wamerasimishiwa ujuzi uliopatikana katika mfumo usio

rasmi. Licha ya hayo, vijana 6,300 wamepata mafunzo ya uzoefu kazini na vijana 2,196 waliokuwa kazini wameongezewa ujuzi. Pia kupitia Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora vijana 812 wamedahiliwa na wanashiriki mafunzo ya kilimo biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imetoa mikopo ya shilingi bilioni 1.88 kwa miradi 85 yenye vijana 595. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imeendelea kutoa mikopo ambapo hadi kufikia Oktoba, 2023 shilingi bilioni 1.27 zimetolewa kwa miradi 56 yenye vijana 392.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Baraza la Taifa la Biashara. Kwa kutambua umuhimu wa Sekta Binafsi, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi na kutengeneza fursa ya majadiliano kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kupitia Baraza la Taifa la Biashara. Baraza hilo huandaa vikao vya majadiliano rasmi kufikia muafaka kati ya sekta hizo kuhusu maboresho ya mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi kwa ujumla wake. Kutokana na jitihada hizo, baraza limeongeza ushiriki wa Sekta Binafsi kupitia mfumo rasmi na jumuishi wa majadiliano katika ngazi zote za utawala. Vilevile, Baraza limewezesha mikoa 11 kuratibu na kufanya mikutano ya mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya zake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maazimio ya Baraza umewezesha kufanya mapitio sera, sheria, kanuni, taratibu na mifumo mbalimbali; kuunganisha majukumu ya taasisi yanayoingiliana; kuimarisha vituo vya huduma za mahali pamoja; kuanzisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA na kuimarisha na kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za kiuchumi hususan miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Mkakati wa Kuendeleza Wananchi Kiuchumi. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ikiwa ni sehemu ya uwezeshaji kwa wananchi wetu, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuwaendeleza wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(NEEC)* ambalo limeanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004: Sambamba na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004, limepewa dhamana ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi ambazo ni mtambuka na zenye kuhusisha wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Septemba, 2023, mifuko na programu za uwezeshaji ilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 743.7 kwa wanufaika wapatao 6,064,957 ambapo wanawake ni asilimia 54. Aidha, kwa mwaka 2022/2023, mifuko na programu za uwezeshaji ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 743.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 713.8 zilizotolewa mwaka 2021/2022. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.02.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la Uhusiano wa Kidiplomasia. Katika kuimarisha na kuchochea shughuli za maendeleo nchini, Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano wa kikanda na kimataifa kwa lengo kufungua fursa mbalimbali ikiwemo uwekezaji na mitaji katika sekta za utalii na uchukuzi. Katika hili, nimpongeze kwa dhati Mwanadiplomasia namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kuimarisha diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala yanayozingatiwa kwenye diplomasia ya uchumi ni pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa tulizonazo, kutafuta fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali, fursa za elimu, mafunzo, utaalamu na ujuzi pamoja na ajira nje ya nchi na kuifanya bidhaa (kuibidhaisha) lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2022/2023, Serikali iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mikataba 13 na Hati za Makubaliano 37. Mikataba na hati hizo zinagusa sekta za kiuchumi na kijamii ikiwemo ulinzi na usalama, kilimo na uvuvi, viwanda, biashara, uwekezaji, TEHAMA na utalii. Nyingine ni afya,

elimu, uchukuzi, mawasiliano, utamaduni, sanaa na michezo, sayansi na teknolojia, mazingira na uchumi wa bluu.

Mheshimiwa Spika, ziara zinazofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine zimekuwa chachu ya kuimarisha uhusiano wa kimataifa. Vilevile, ziara hizo zimeibua fursa zenye manufaa ya kiuchumi nchini. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni ongezeko la watalii, ongezeko la wafanyabishara na wawekezaji, miradi mikubwa na ya kati, na uwekezaji na kufungua masoko ya bidhaa mbalimbali. Kipekee, nimpongeze tena Mheshimiwa Rais wetu ambaye kupitia ziara zake na nchi jirani, aliweza kutatua changamoto za kibiashara kwenye mipaka hasa kwenye nchi Jirani za Kenya na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu na kufanikisha ziara za kikazi na kitaifa za Viongozi Wakuu kutoka mataifa mengine kuja hapa nchini. Baadhi ya viongozi hao waliotoka nchi za nje ni kutoka Ujerumani, Indonesia, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Rwanda, Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Uswisi na Marekani. Serikali itaendelea kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa nchi nyingine wanaozuru Tanzania ili kuimarisha mahusiano na uhusiano wetu wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi hizo. Ziara hizo zitaimarishwa ili nchi yetu iendelee kunufaika na fursa za kiuchumi na kijamii, lakini pia iweze kung'ara kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu, naomba sasa niweke msisitizo katika masuala muhimu yafuatayo ambayo ni utaratibu wa upatikanaji wa pembejeo, udhibiti na utatuzi wa migogoro ya ardhi, uhifadhi wa mazingira, na kuimarisha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa pembejeo muhimu kwa wakulima wetu zikiwemo mbolea. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2023, wakulima zaidi ya milioni 3.6 walikuwa wamesajiliwa na kupata namba za utambulisho za kununua mbolea ya ruzuku. Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Wakuu wa Wilaya ambao pia ni Wenyeviti wa Kamati za Pembejeo za Wilaya

wawahamasishe wakulima kujisajili na kutoa taarifa sahihi sasa kuhusu mazao waweze kusajili, kutoa taarifa za mazao wanayoyalima na ukubwa wa mashamba yao kwenye madaftari ya wakulima ambayo yamesambazwa kwa watendaji wa vijiji na mitaa ili taarifa zao ziweze kuingizwa kwenye mfumo na wapatiwe namba za kununulia mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuielekeza Wizara ya Kilimo ihakikishe mbolea inapatikana kwa wakati na ishirikiane na Wakuu wa Wilaya kusimamia kwa karibu usambazaji wa mbolea kwa wakulima. Hatua hii iende sambamba na kutatua changamoto zinazojitokeza wakati wa usambazaji wa pembejeo hiyo muhimu. Vilevile, kampuni na taasisi zinazozalisha mbegu bora ziongeze kiwango cha uzalishaji na kuweka utaratibu mzuri na wa kufikisha mbegu hizo kwa wakulima katika maeneo yao ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kushirikisha Wizara za kisekta. Mikakati hiyo ni pamoja na kuunda kamati maalum za kushughulikia migogoro, kuendesha kliniki maalum za ardhi ambapo wananchi wamekuwa wakisikilizwa malalamiko yao na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kufanya vikao na wadau mbalimbali kuhusu usimamizi bora wa ardhi, kufanya kaguzi za milki, kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa na kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha huduma zinazotolewa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwachukulia hatua watumishi wanaochochea migogoro na kutozingatia sheria na kanuni na taratibu ikiwemo kujihusisha na vitendo vya rushwa. Vitendo hivyo havikubaliki kwani ni kinyume cha maadili ya utendaji wa utumishi wa umma. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kumwagiza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuendelea kuwachukulia hatua kali watumishi wa idara za ardhi wanaokiuka sheria. Hivyo basi, kila mmoja akafanye kazi kwa weledi, uadilifu na kwa kuzingatia taaluma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitoa maelekezo kwamba kampuni zote zilizopewa kazi za upimaji wa viwanja kwenye Majiji, Manispaa na Mikoa na zimeshindwa kukamilisha kazi yao, zilizokuwa na mikataba ama hazikuwa na mikataba ziendelee kuchukuliwa hatua kali za kisheria. Ikumbukwe kuwa, kampuni nyingi zilizopewa kazi za kupima maeneo ya wananchi kwa lengo la kutoa hati miliki kote nchini, hazifanyi kazi hizo kikamilifu licha ya wananchi kulipa fedha kwa muda mrefu. Nasisitiza kuwa kampuni hizo ziendelee kuchukuliwa hatua, tena hatua za kisheria zinazokomesha udanganyifu wa aina hiyo kwa wananchi wetu ikiwemo pia kuziachisha nafasi hiyo kama hawataweza kutekeleza sheria na kanuni zilizowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilielekeza pia kwamba Halmashauri zote kama mamlaka za upangaji ziongeze udhibiti na usimamizi wa maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya umma na yale ya hifadhi ya mazingira, yakiwepo maeneo ya ukanda wa kijani, maeneo ya wazi, viwanja vya michezo, makaburi na mengineyo ili kuzuia uvamizi na mabadiliko ya matumizi ya maeneo hayo. Mfano halisi ni Jiji la Dodoma na Manispaa ya Kigoma ambako maeneo mengi ya wazi yameshagawiwa kwa wananchi kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yaliyotengwa na kuhifadhiwa yasiruhusiwe kufanyiwa mabadiliko. Ni vema mabadiliko hayo yawe yamerishiwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kabla ya kuwasilishwa kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye maeneo wanayopendekeza kuyabadilisha matumizi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Michezo**.** Kipekee kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono mapana aliyonayo katika kuinua Sekta ya Michezo hapa nchini. Mheshimiwa Rais, katika vipindi mbalimbali amekuwa akitoa miongozo ambayo imekuwa na tija na hatimaye kuleta mapinduzi makubwa kabisa katika ya sekta ya michezo hapa nchini. Sina shaka, mtakubaliana nami kuwa kupitia maono yake, tasnia ya michezo nchini inaendelea kuthaminiwa na

tumeendelea kushuhudia matunda mazuri kwa timu zetu zikiwemo zile za Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa ili timu zetu za Taifa ziweze kushiriki katika michuano ya Kimataifa, maandalizi ya kutosha yanahitajika ambayo yanagharimu fedha nyingi. Natoa pongezi kubwa sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Jemadari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kufanya maamuzi sahihi ya kuiwezesha timu ya Taifa ya Tanzania kufuzu katika fainali za *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa akiridhia ujumbe maalumu wa Serikali kuambatana na *Taifa Stars* katika michezo yao ya ugenini ili kuongeza hamasa kwa wachezaji na matokeo ya kweli tumeyaona. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa motisha kwa wanamichezo wetu ambazo zimekuwa zikiongeza ari na hamasa kwa wanamichezo wetu. Licha ya kuendeleza mpango wa Goli la Mama, mtakumbuka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, siku ya tarehe 4/10/2023 alinituma nikatekeleze ahadi yake ya kuwatunuku Timu ya *Taifa Stars* fedha kiasi cha shilingi milioni 500 kwa kufuzu kushiriki mashindano ya Mataifa ya Afrika yatakayofanyika nchini Ivory Coast Januari, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, mafanikio katika sekta ya michezo hapa nchini yamechagizwa pia michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imekuwa ikitolewa ili kuboresha sekta ya michezo hapa nchini. Sote tu mashuhuda, jamii sasa imehamasika na ushiriki katika michezo na umeongezeka. Michezo imekuwa zaidi ya burudani, kwani sasa ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi kusaidia kutatua changamoto mbalimbali, pia michezo imeendelea kuimarisha afya za washiriki. Hii inaenda kuimarisha pia kwenye sekta ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Baraza la Michezo la Taifa katika kutekeleza mikakati ya maendeleo ya michezo hapa nchini. Ushirikiano unaotolewa kwa taasisi za michezo umekuwa chachu ya kufanikisha kutimiza malengo yetu ya kuendeleza michezo. Mfano mzuri ni ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya michezo kwa

sekta ya umma na binafsi. Kwa mfano, *Azam Complex*, ni uwanja mzuri wa kisasa, taasisi za ulinzi, zimekuwa zikiimarisha viwanja kama *Golf* na mpira wa miguu na michezo ya *basketball,* taasisi za elimu kwa mfano shule, vyuo na taasisi nyinginezo, zimefanya vizuri sana katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kutoa pongezi nyingi kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kwa uzinduzi wa mashindano ya ligi ya soka ya Afrika yaliyofanyika Jijini Dar es salaam Tarehe 20 Oktoba, katika Uwanja wa Benjamini William Mkapa ambao haujawahi kutokea katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa miaka mingi, katika mechi iliyochezwa siku hiyo ya uzinduzi Klabu ya Simba ilichuana na Klabu ya Al Ahly ya Misri na kutoka sare. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuipongeza sana Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake chini ya umri wa miaka 20 almaarufu *Tanzanite Queens* kwa ushindi wa mabao saba kwa bila dhidi ya Djibouti katika mchezo wa kufuzu kombe la Dunia ambao umechezwa Uwanja wa Azam *Complex* Tarehe 11 Oktoba, 2023 kwa ushindi huo *Tanzanite Queens* watachuana na Nigeria katika pambano litakalofanyika nchini Colombia Mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia Timu ya Twiga *Stars* kwa kusonga mbele katika hatua ya kufuzu Mashindano ya *WAFCON* 2024. Ushindi huo umepatikana baada ya kupata ushindi wa *penalty* nne kwa mbili baada ya kuifunga Timu ya Ivory Coast kwenye shindano lililofanyika. Pia katika Uwanja wa Azam *Complex* pale Chamazi Jijini Dar es salaam. Aidha, ninawapongeza pia Timu ya Twiga *Stars* kwa kufuzu Mashindano ya *Olympic* 2024 baada ya kuibwaga Botswana kwa bao moja bila katika mchezo uliofanyika nchini Botswana.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Timu ya Wanawake ya JKT *Queens* kwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa ya Wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati *(CECAFA)*. Ubingwa huu umewawezesha kushiriki Ligi ya Mabingwa Wanawake Afrika inayoendelea nchini Ivory Coast. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya mchezo wa mpira wa miguu nawapongeza pia vijana wetu Ramadhan *Brother's* wanasarakasi mahiri walioshiriki katika mashindano maarufu ya *American Got Tanzania Talent.* Vijana wetu hawa wameonyesha vipawa na uwezo wa hali juu katika mchezo huu wa kukonga mioyo ya watazamaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, washiriki wetu katika mchezo wa ngumi wameendelea kunga'ra sana katika mashindano ya ndani na nje ya nchi yetu. Nampongeza sana Mwanamasumbwi wetu Ibrahim *Class* kwa kushinda mkanda wa *TPBRC* baada ya kumshinda mpinzani wake Xiao Tau Su kutoka Jamuhuri ya Watu wa China. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kumpongeza Mwanamasumbwi Pius Mpenda kwa kushinda ubingwa wa *WBC Peace Champion* baada ya kumshinda Mrusi Dauren Yeleussinov. Vilevile, nampongeza sana Nahodha wa Timu ya Taifa ya Ngumi Ngorongoro *Black Rhinos* Yusuf Lucas Changalawe kwa kufanikiwa kuingia katika fainali ya mashindano ya *Olympic* ya Paris Mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo ya mashindano ya mbio, napenda nimpongeze sana mwanariadha wetu Magdalena Shauri kwa kushinda medali ya shaba katika mbio za *BMW Berlin Marathon* baada ya kushika nafasi ya tatu baada ya kusinda mbio hizo. Lakini vilevile, nipongeze mwanariadha Alphonce Felix Simbu kwa kushika nafasi ya pili kwenye Mashindano ya Majeshi yanayojulikana kama *The World CISM Half Marathon* yaliyofanyika huko Uswisi. Ninawapongeza sana wanariadha wetu kwa ushindi huo mkubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba muendelee kuwa watulivu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Rais. Jitihada zenu zinaonekana kwani Tanzania inazidi kung'ara katika medani za kimataifa. Sote tuendelee kushuhudia maendeleo haya makubwa na tuunge mkono maendeleo haya makubwa hasa katika sekta hii na

kuchangia Pato la Taifa na kukuza uchumi kwa ujumla. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninapomaliza kuelezea habari za michezo sitaki kuzungumzia suala la Ligi Kuu ya Tanzania *(NBC)*. Inaonekana Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanasubiri hii ambako vilabu vyetu vikubwa nchini Simba na Yanga vinaendelea kuhamasisha michezo hapa nchini. Matokeo ya michezo yao katika Ligi Kuu tumeendelea kuishuhudia na matokeo ya michezo ni ya kawaida. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kushuhudia mafuriko yaliyotokea Bonde la Mto Msimbazi, mafuriko yaliyotokea Bonde la Mto Msimbazi na kuwaua watu watano. Matokeo haya ni ya kawaida kwa sababu hata Mwaka 1977 yaliwahi kupita pia kwenye Mtaa wa Jangwani na kubeba watu sita na Mwaka 2012 pia yalipita huko huko Jangwani yakabeba watu watano na Mwaka 2020 yalipitia kwenye Bonde hilo hilo la Jangwani yakabeba watu wanne. Kwa hiyo, hali hiyo ni ya kawaida na basi niipongeze Timu ya Yanga kwa kushinda mchezo wa juzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Msemaji Ndugu Ahmed Ally anasema jambo hili halitojitokeza tena na wategemee makubwa kwenye mzunguko wa pili ambao utafanyika mwezi Aprili mapema mwaka 2024. Kwa hiyo niwatakie kila la kheri na niwape Simba pole nyingi kwa tukio hilo ambalo limepokelewa kwa huzuni na furaha pia kwa upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kufanya mjadala wa Bunge hili kwa kuzingatia manufaa makubwa ya ustawi wa Taifa letu. Kama ambavyo mnafahamu uwepo wa Bunge hili ulikuwa ni muhimu sana ili kuweza kupata maoni na ushauri kutokana na hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, ninawashukuru Watumishi wa Serikali kwa kuendelea kufanyia kazi masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yakiwezesha uwasilishaji wa hoja mbalimbali zilizotokana na mijadala ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri waliyotupatia katika kipindi chote cha Bunge hili. Kipekee, nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi yenu nzuri kwa maana tumeishi kwa amani na utulivu katika kipindi chote cha Mkutano huu wa Kumi na Tatu wa Bunge hili ambalo leo tutalifunga muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Wanahabari kwa kuendelea kuuhabarisha umma juu ya Shughuli zote za Bunge letu Tukufu toka siku ya kwanza mpaka siku hii ya leo tunapoelekea kuhitimisha Mkutano wetu. Pia natambua mchango mkubwa wa huduma unaotolewa na madereva wetu waliotuhudumia wakati wote, vilevile ninatoa shukrani kwa watoa huduma wengine mlioshiriki kutuhudumia muda wote tukiwa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie kukushukuru sana, wewe na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Katibu wa Bunge na Watumishi wa Bunge, niwaahidi kuwa tutaendelea kutekeleza yale mliyoyashauri na kuyatolea maoni katika kipindi chote cha Mkutano wa Bunge hili, kwani ushauri na maoni yenu ndio msingi wa kuiwezesha Serikali yetu kutimiza majukumu yake ipasavyo. Nami niwatakie Waheshimiwa Wabunge wenzangu safari njema na mnaporejea majimboni kwenu na mkaendelee kuwahakikishia wananchi dhamira njema ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake katika kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka, na hatutakuwa na Mkutano wa Bunge tena kwa mwaka huu wa 2023, nitumie nafasi hii kuwatakia Watanzania wote na waumini wote wa Kikristo kwenye Sherehe Njema ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 30 Januari, 2024 saa tatu kamili asubuhi tutakapokutana tena katika Ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, sasa, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi kwa muda kidogo. Waheshimiwa Wabunge wakati tukihitimisha Mkutano wetu huu pamoja na mambo mengine imefanyika kazi kubwa sana kabla sijaenda kwenye hiyo kwa kifupi. Wakati tukihitimisha hoja iliyokuwa imeletwa hapa mbele na Mheshimiwa George Mwenisongole na namna ilivyobadirishwa na Bunge limehojiwa na kukubaliana na hoja hiyo, wakati tukiiambia Serikali ikalifanyie kazi jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, hatujatoa muda lakini naamini kwamba Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itafuatilia kwa karibu jambo hili wakati watakapokuwa wanaleta taarifa zao, kwenye Bunge ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameishatutangazia tarehe hapa, basi watakuwa wanatupa mrejesho kwamba wamefikia wapi katika huo mchakato.Wao watakuwa wakiendelea huko kushauriana na Serikali lakini tunaamini mwakani, mwaka hautapinduka kabla hiyo sheria

haijaja hapa kwa ajili ya kuboresha hayo mazingira ya ufanyaji kazi wa Maafisa Ugani na Maafisa Ushirika na tunawakia kila la kheri katika hilo, kwa sababu nanyi ni sehemu ya Bunge kwa muktadha huo na wote tumefanya maamuzi haya kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine linahusu michango ambayo jana tulipata ugeni hapa wa Profesa Jay na Waheshimiwa Wabunge nikawa nimetoa ruhusa kwamba wasaidizi wapite kwenye viti vyenu huko ili muweze kuchanga. Sasa nataka niwatangazie mchango ambao umeishakusanywa mpaka sasa na huu mchango hauhusishi mchango wa humu, sijaliona jina la Mheshimiwa Naibu Spika, humu hayumo Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, Naibu Waziri Mkuu na Waziri Mkuu wenyewe watatafuta utaratibu mzuri wa kumfikia Profesa Jay, lakini na Wabunge wengine ambao hawajapata nafasi ya kuchanga pengine ni kwa sababu ya majukumu mbalimbali basi na wao wajitahidi kufikisha michango yao kwa kadri tulivyoletewa hiyo hoja na Mheshimiwa Aida Khenani na Mheshimiwa Musukuma na wote hapa mkawa mmepiga makofi.

Waheshimiwa Wabunge, makusanyo yaliyopatikana ni shilingi milioni 5,740,000. Kwa hiyo fedha hii atakabidhiwa lakini wale ambao bado hawajachanga basi wanaweza kutafuta utaratibu mzuri wa kumfikishia Profesa Jay mchango huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nitumie fursa hii kumshukuru sana Katibu wa Bunge kwa kazi nzuri aliyoifanya yeye na Watendaji chini yake. Wamelifanya Bunge letu lifanye kazi kwa ufanisi tunakushukuru sana Katibu wa Bunge pamoja na Watumishi wote wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana nyinyi kwa kazi nzuri mlioifanya kipindi chote hiki. Mmefanya kazi nzuri ngazi ya Kamati lakini pia humu Bungeni, michango yenu mmesikia Serikali ikiwa ina jibu hapa na pale ikiwa inasema michango yenu wanaithamini na wanaichukua. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote ninawashukuru sana kwa ushirikiano mlioutoa ambao umeonyesha namna ambavyo Bunge tunaweza kufanya kazi vizuri ya kuishauri na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia niwashukuru Viongozi wetu sasa wa Wabunge ngazi mbalimbali kwa maana ya Wenyeviti wetu na Makamu Wenyeviti wamefanya kazi nzuri sana, ninawapongeza sana. Wasaidizi wangu Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa namna ambavyo umefanya kazi nzuri ya kunisaidia mambo yameenda vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, ahsante sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya hapa mbele lakini pia na kwenye vikao vingine na Mwenyekiti wetu mwingine ni Mheshimiwa Daniel Sillo Baran tunakushukuru sana kwa kazi nzuri uliyoifanya pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niishukuru pia Serikali kwa ushirikiano ambao mmeuonyesha katika kipindi chote hiki cha Bunge mmejitokeza kwenye Kamati, malalamiko yalikuwepo lakini siyo mengi kama kipindi kingine. Kwa hiyo, mmejitahidi sana Serikali, hasa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwenda kwenye Kamati, ninawashukuru sana kwa ushirikiano mliouonyesha, lakini hata pale zilipojitokeza changamoto basi tutaendelea kuwasiliana ili tuboreshe mahusiano hayo, kwa sababu Kamati haziwezi kufanya kazi bila Serikali. Tunawashukuru kwa ushirikiano mzuri ambao mmeuonyesha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru kwa kuwa mnahudhuria humu Bungeni, maana maswali na majibu jamani wakati mwingine mpaka nasema maswali ni mengi, Naibu Mawaziri wanalazimika kujibu hapa na Mawaziri saa nyingine hata kama haipendezi sana lakini Wajumbe hapana Wabunge samahani wanahitaji kujua hoja nyingi sana kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo, pale ambapo mmeulizwa maswali mengi sana mkiwa mmesimama hapa tuchukuliane Wabunge ni wengi na muda ni mchache kwa hiyo lazima tuwape fursa ya kusema yale ambayo yanatoka kwa wananchi. Kwa hiyo, tunawashukuru pia kwa kujibu maswali mengi sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia ninawashukuru wananchi mbalimbali ambao wameweza kulitembelea Bunge letu nao ni watu muhimu sana wakitutembelea tumefurahi na tunawakia kila la kheri katika yote na wale ambao wametutembelea

tukihitimisha Bunge, nao tunawashukuru kwamba, leo hatukuwa peke yetu humu ndani nanyi mpo kwa hiyo karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kuwashukuru Wananchi wote wa Tanzania, sisi kama Wawakilishi wao tumejitahidi kufanya kwa sehemu yetu yale ambayo wametutuma na sasa kwa sababu leo tunahitimisha Mkutano wetu huu, tunarejea huko Majimboni basi kama kuna mahali ambapo mngetamani Wabunge wenu waboreshe zaidi, Wabunge wanapokuja huko Majimboni wataarifuni watakapokuja huku wataleta mawazo ya namna Bunge lenu mnataka lifanye kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nami niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa yote yale aliyoyasema. Kuwapongeza aliowapongeza lakini pia kuwahurumia wale aliowahurumia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nawatakia sikukuu njema za Krismasi lakini pia nawatakia Mwaka Mpya wale ambao hatutaonana kabla ya mwaka kujitokeza na wote tuombeane kheri sote tuonane kwa tarehe ambayo nitaisema hapa punde.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Siku ya tarehe 30 Januari, 2024 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 9.42 Alasiri Bunge Liliahirishwa hadi Siku Jumanne, Tarehe 30 Januari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*